

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 8 Novemba, 2019**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini (*State of the Environment Report, 3*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2018/2019 (*The Annual Performance Evaluation Report on Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2018/2019*).

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza linalekezwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Linaulizwa na Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini.

Na. 40

#### **Kuwa na Uchaguzi Mdogo wa Serikali za Mitaa**

**MHE. JUSTIN J. MONKO** aliuliza:-

Inapotokea Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji amefariki au kupoteza sifa ya kuwa Mwenyekiti wa Mtaa au Kijiji husika huongozwa na Kaimu Mwenyekiti:-

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuwepo uchaguzi mdogo kama ilivyo kwa Madiwani na Wabunge?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MIAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019 yaani Kanuni ya 43(1) – (4) na Kanuni ya 45 zinatoa fursa ya kufanya Uchaguzi Mdogo kujaza nafasi iliyoachwa wazi endapo Mwenyekiti wa Kitongoji, Kijiji, Mtaa atafariki au kupoteza sifa za kuendelea

kuwa katika nafasi hiyo kutokana na sababu zilizoainishwa kwenye Kanuni ya 44(1) na (2). Uchaguzi Mdogo hautafanyika endapo muda uliosalia kabla ya muda wa Mwenyekiti kuwa kwenye madaraka kukoma ili kupisha uchaguzi ni miezi sita au pungufu yake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Monko.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza; kwa kuwa Serikali inakirii kwamba, sheria na taratibu zinaruhusu uchaguzi huo; na kwa kuwa, wanatambua kwamba, maeneo mengi yalikuwa pia yana makaimu na chaguzi hizo hazikufanyika. Je, Serikali sasa inatoa maelekezo gani kwa watendaji wanaohusika ili wawe wanachukua hatua zinazostahili kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utaondoa kabisa makaimu hawa ambao wamekuwa ni kero kwa maeneo mengine na tumesikia chama kikuu cha upinzani, CHADEMA, wametangaza kujitoa katika uchaguzi huu na kuwakosesha wananchi haki yao ya Kimsingi ya kuchagua viongozi wanaowataka kwa mujibu wa Katiba yetu na Serikali ya Vyama Vingi. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kadhia hii ambayo inaendelea nchini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MIAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la kwanza anataka kujua kwa nini nafasi hizo ziliikuwa hazijazwi kama ambavyo inatakiwa na kanuni. Ni kweli kwamba, kumekuwa

na nafasi wazi mpaka tunaingia kwenye uchaguzi wa mwaka huu na hii ilitokana na aidha, watendaji wetu katika ngazi zile kutokuwa na uelewa mkubwa wa kanuni zetu, lakini vilevile tumeshaelekeza sasa kwamba, tunacho chuo hapa cha Serikali za Mitaa cha Hombolo. Baada ya uchaguzi huu Wakurugenzi na sisi Wabunge tunaomba tushiriki kuhakikisha kwamba, viongozi wetu watakaopatikana wa vijiji, vitongoji na mitaa wapate mafunzo pamoja na watendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko sababu mbalimbali zimeainishwa ambazo Mwenyekiti wa Mtaa au Kijiji au Kitongoji anaweza kupoteza nafasi yake, mojawapo ni kwamba, kama Mwenyekiti kwenye Kijiji hajasoma mapato na matumizi kwa muda wa miaka mitatu mfululizo inaweza ikamfanya akapoteza nafasi yake. Vilevile Mwenyekiti huyo kama atakuwa hajaitisha mikutano mara tatu mfululizo bila sababu za msingi, au inaweza ikaaitisha mikutano ya kisheria ye ye Mwenyekiti asihudhurie katika hii mikutano, sababu nyingi ambazo zimetolewa ikiwepo kufukuzwa na chama au kufariki au kuijuzulu mwenyewe. Kwa hiyo, tunaomba tutoe wito kwamba, baada ya uchaguzi huu basi viongozi wetu ngazi husika hasa Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri zetu na Miji watoe elimu, watoe maelekezo na Waheshimiwa Wabunge wakati wowote ikitokea nafasi wazi au ukahisi, tuwasiliane tutachukua hatua kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anazungumzia habari ya CHADEMA kujiondoa katika nafasi za kugombea. Ni kweli na sisi kama ofisi tumepata taarifa kwenye mitandao labda huenda wakatoa tamko rasmi, lakini Kauli ya Serikali ni kwamba, uchaguzi huu unaendelea kama kawaida kama ulivyopangwa kwenye ratiba. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika tarehe 24 Novemba, mwaka huu 2019, wananchi wote ambao wamejandikisha na vyama vile ambavyo viro kwenye mchakato waendelee na mchakato wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wametoa tamko jana kwenye mitandao, lakini itakumbukwa kwamba, kwenye taratibu zetu ni kwamba, wale ambao walikuwa na

malalamiko wameandika mapingamizi yao na kesho ndio siku ya mwisho, wao jana ndio wametoa tamko. Kwa hiyo, kama wamejiondoa hawana sababu yoyote ya kulalamika kwamba, hawakutendewa haki, tulieleza tukarudia mara kadhaa kwamba, watu wenye sifa ya kutoa mapingamizi ni wale ambao ni wagombea. Wenzetu walitaka watoe kauli Bungeni, kwenye mitandao, mtaani na Serikali iamue, Serikali inafanya kazi kwa karatasi kwa mawasiliano, hatuna *document* mezani hatuvezi kujadili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito, yale maagizo ya kuhamasisha wananchi wasishiriki shughuli za maendeleo bahati nzuri Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amefanya kazi kubwa Watanzania wanamuunga mkono. Mwenye mamlaka ya kutoa maelekezo nchini Tanzania ni Rais wa Jamhuri ya Muungano pekee na sio kiongozi wa chama cha siasa. Kiongozi wa chama cha siasa atatoa maelekezo kwenye chama chake kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya ambao ni Wenye viti wa Kamati za Ulinzi na Usalama, tumepata taarifa kwenye mitandao wanahamasisha watu, wanaharibu mazao ya watu na wanatishia watumishi wa umma. Wakuu wa Wilaya popote mlipo kama kuna mtu anahisi hakutendewa haki kwenye uchaguzi huu na anafanya fujo mtaani, sheria stahiki zichukue mkondo wake. Hatujawahi kutunga sheria katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema ukigombea ukinyimwa haki au ukahisi kunyimwa haki ukafanye fujo. Ukigombea ukinyimwa haki au ukahisi kunyimwa haki ziko taratibu za kisheria wazifuate, wasipofuata vyombo vya usalama vitashughulika nao na Watanzania wawe na amani, uchaguzi uko palepale, amani na tulivu, tunachapa kazi na hakuna ambaye atawaambia wananchi wasishiriki shughuli za maendeleo, sisi TAMISEMI tupo pale kila mahali, ukishiriki kuhamasisha fujo na viongozi wetu wachukue taarifa mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii, atakayebainika tusilaumiane mbele ya safari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza. Kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu Katiba inatambua uwepo wa Serikali za Mitaa na uwepo wa Serikali Kuu. Serikali za Mitaa kwa juu zinaanzia kwenye ngazi ya Halmashauri. Je, Serikali haioni kwamba, umefika wakati sasa wa kuunganisha uchaguzi wa Madiwani na uchaguzi wa vijiji, vitongoji na mitaa ili Serikali za Mitaa wafanye uchaguzi pamoja na Serikali Kuu kwa maana ya Bunge na Rais, uchaguzi wao uwepamoja?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MIAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, hili jambo ni jambo la kisheria. Tunayo Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 287 na Sura Namba 288, lakini pia tuna uchaguzi wa Serikali Kuu, Wabunge na Madiwani na Mheshimiwa Rais; tupokee wazo hili tulifanyie kazi, ni jambo la mchakato, kama itawezekana kufanya hivyo ni jambo jema tutalifanyia kazi, lakini hili ni jambo la kisheria tunalipokea na kulifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu zetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi kuuliza swalii la nyongeza. Kutokana na jibu la msingi la pili alilotoa Naibu Waziri, mimi binafsi jana nimemtoa mpangaji Polisi kwenye nyumba yangu kwa sababu, sioni umuhimu wa kushirikiana naye na nyumba ni yangu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Vedastus Mthayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini; bado tuko Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Na. 41

**Viongozi Wanaozua Mabango ya Wananchi Wakati wa Ziara ya Mheshimiwa Rais**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Ikiwa lengo la Serikali ni kuhakikisha inawahudumia na kutatua kero za wananchi, kero hizo zisipotatuliwa katika ngazi za Mitaa, Kata, Wilaya na Mkoa wananchi hao hulazimika kuandika na kushika mabango kila Mheshimiwa Rais anapofika majimboni ili kupaza sauti zao:-

(a) Je, ni kwa nini Viongozi wa Wilaya na Mkoa huzuia mabango hayo yasioneokane na kusomwa na Mheshimiwa Rais?

(b) Je, wananchi watumie njia gani kufikisha ujumbe wao kwa Mheshimiwa Rais pale matatizo yanaposhindwa kutatuliwa katika ngazi ya chini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Serikali kwa ujumla inaanini katika uwazi na uwajibikaji na kwamba, ni haki ya msingi ya wananchi kueleza

matatizo yao kwa sauti au kwa maandishi pindi wanapotembelewa na Viongozi mbalimbali wa Kitaifa ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais. Kama kuna Viongozi wa Mikoa au Wilaya wanawazuia wananchi, hayo sio maelekezo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI wala Serikali na wanapaswa kuacha mara moja tabia hiyo kwa kuwa, wananchi wana haki ya kueleza changamoto zao kwa Viongozi wa Kitaifa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao utaratibu na mfumo wa kuhakikisha kero za wananchi zinatatuliwa na viongozi. Mfumo huo unaanzia ngazi ya Kitongoji hadi Taifa, utaratibu ambao unawawezesha wananchi kufikisha kero zao kwenye ngazi mbalimbali kwa ajili ya kuzitafutia utatuzi. Nazielekeza Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kuimarisha madawati ya kupokea kero na malalamiko katika maeneo yao ili kuwawezesha wananchi kufikisha kero na changamoto zao kwa wakati. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vedastus Mathayo.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni kwa nini sasa hawa viongozi ambao mara kwa mara maana huwa tunashuhudia, klongozi akifika mahali wanawapiga wakinyanya mabango yao, wanapigwa, wanafukuzwa na kwa tamko hilo sasa ni kwa nini hawa viongozi wanaofanya mambo haya ya kunyanyasa wananchi wasichukuliwe hatua za kinidhamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mara nyingi huu utaratibu wa kutatua kero za wananchi, unakuta hata leo mfano Waziri wa TAMISEMI akifika pale ziko kero nyingi za wananchi yeye ndio anazitatua, au Waziri wa Ardhi akifika pale zinaonekana ziko wazi ambazo labda Mkurugenzi angeweza kuzitatua, lakini ameshindwa kuzitatua mpaka kiongozi afike pale. Hali hii sasa inaonesha dhahiri kwamba, leo baadhi ya kero nyingi zinaweza kutatuliwa tu pale

ambapo viongozi wa Kiserikali au viongozi wakuu wanaenda pale. Serikali inao mpango gani wa kuhakikisha kwamba, hayo matatizo yanaisha na matatizo ya wananchi yanatatuliwa kule kwenye ngazi za wilaya?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MIAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini, ndugu yangu, kaka yangu Vedastus Mathayo Manyinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua ni kwa nini kuna baadhi ya watu wanazuia wananchi kutoa kero zao au kuonesha mabango ambayo yamejaa hisia za changamoto zao katika maeneo yao na amesema kwamba, wanapigwa. Tunachojua ni kwamba, Mheshimiwa Rais na viongozi wengine wakifanya ziara wamekuwa wakiruhusu maswali kujibiwa na wananchi kutoa kero zao. Tukumbushane kwamba, pia kwenye mikutano ile ambayo kiongozi hasa Mheshimiwa Rais anapokuwepo ni mkusanyiko mkubwa sana. Sasa wakati mwagine ni watu wa usalama wanaangalia mazingira yalivyo, bahati mbaya sana yale mabango hayaratibwi, kwa hiyo, wao wanachukua tihadhari kwanza ya kiusalama halafu wakigundua kwamba, ni ya hoja *genuine*, wana lengo la kupeleka kero, inaruhusiwa na wamekuwa wakifanya mara kadhaa tumeshuhudia sisi wenyeewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nitoe wito kwamba, viongozi wetu hawa kwenye maeneo yetu ya mikoza na wilaya, tunao ugatuvi wa madaraka katika nchi hii kutoka ngazi ya kitongoji mpaka ngazi ya kitaifa na hii itaenda sambamba na kujibu swali lake la msingi, kimsingi Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo, tumeeleza kwamba, viongozi wetu watoke ofisini, kama ni Mkuu wa Mkoza awe na utaratibnu wa kusikiliza wananchi wake katika eneo lake husika. Kwanza akutane na Wakuu wa Wilaya kwenye mkoza

wake husika na watendaji wake, anapokea changamoto katika mkoa wake, wanaweka mikakati namna ya kutatua zile changamoto, halafu badae anafanya ziara kwenda kusaidia yale ambayo yameshindikana ngazi ya wilaya wasaidiane kama mkoa kuyamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi maana yake ni kwamba, jambo ambalo lipo kwenye ngazi ya kitongoji limalizwe na viongozi wa kitongoji kwa tatizo husika. Jambo likitoka kwenye kitongoji kuja kwenye kijiji au mtaa liwe na uwezo huo walimalize, kwenye kata vivyo hivyo na kwenye ngazi ya wilaya na mkoa. Tukifanya kazi kwa pamoja kila mtu akaenda *site*, watu wasikilizwe, kero zitatuliwe, hakuna sababu ambayo itakuwepo tena Mheshimiwa Rais au Viongozi wa Kitaifa Mawaziri kwenda mahali mbalimbali kutatua kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitoe wito kwa viongozi wetu kimsingi ni kuonesha kwamba, mtu huyo kwenye mkoa au kwenye kata ameshindwa kufanya kazi. Kama kuna changamoto inatolewa mbele kiongozi wa Kitaifa akiwa kwenye ziara wakati pale kuna mtu ambaye ni wa kisiasa mwakilishi, lakini pia kuna mtu ambaye ni mteuliwa wa Rais au mamlaka nyingine halafu kuna watendaji wa Serikali. Tukifanya kazi kila mtu kwa ngazi yake hii habari ya kupeana mabango wakati viongozi wamekuja haitakuwepo, tutakutana na viongozi watafanya mambo ya jumla makubwa ya Kitaifa na tutaenda na maendeleo yetu kama kawaida. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Asante. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumuuliza Naibu Waziri swalidogo la nyongeza. Kwa kuwa ma-DAS na Wakuu wa Mikoa na wateuliwa wa Rais wengi wao wengine hawataki kufuata taratibu kusikiliza kero za wananchi na hata pale wananchi wengine wanapodhulumiwa haki zao hawatatu kwa wakati, mpaka wanasubiri msafara wa Rais na kwenda kulalamika mbele ya Rais wale wananchi ambao wamedhulumiwa haki

zao. Je, Serikali ina mkakati gani hawa ma-DAS na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wasiowajibika katika nafasi mbalimbali walizoteuliwa ili kuwahakiki na kuchukuliwa hatua za kisheria?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa nataka majibu yawe mafupi, maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna baadhi ya maeneo kumekuwa na malalamiko, lakini Mheshimiwa Rais alipokuwa anahutubia katika eneo la Mbarali, Mkoani Mbeya alitoa maelekezo mahususi kwamba, kila Mkuu wa Mkoa, kila Mkuu wa Wilaya, kila mteule wa Serikali na mamlaka yake mpaka ngazi ya chini waweke ratiba ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua. Zile ambazo zitakuwa zimeshindikana kwenye ngazi yao wapeleke ngazi ya juu, lakini tumeenda hatua mbele zaidi tunafuutilia, Mheshimiwa Maryam na Wabunge wengine kama kuna maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ataenda au viongozi wengine watu wananyanya mabango kulalamikia kero ambazo zipo ndani ya uwezo wa viongozi wale, hao watu ndio wanapaswa kimsingi kuondolewa katika nafasi hiyo kwa sababu, wameshindwa kutimiza wajibu wao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki.

Na. 42

**Ujenzi wa Barabara ya King'ori – Uwiro – Arumeru**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO aliuliza:-**

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya King'ori kutoka Malula Kibaoni hadi King'ori Madukani, Maruvango, Leguruki, Ngaranyuki hadi Uwiro?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) Wilaya ya Meru imekamilisha usanifu wa barabara ya Malula-King'ori-Leguki-Ngarenanyuki yenyeye urefu wa Kilomita 33 ili kuijenga kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.259 ili ipitike majira yote ya mwaka. Serikali inaendelea kutafuta fedha za kukamilisha ujenzi huo. Aidha, ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ni mpango wa muda mrefu ambaao utekelezaji wake utategemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara hiyo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha shilingi milioni 221 kilitumika kufanya matengenezo ya kawaida katika barabara hiyo. Vilevile mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha Shilingi milioni 35.7 kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Barabara hii inapita kata nane huko kuna wananchi ambaao wanafanya shughuli nyingi sana za

kiuchumi lakini pia kuna taasisi hata shule iliyokuwa ya kwanza kitaifa iko eneo hilo.

Je, ni kwanini Serikali isione kwamba kuna umuhimu sasa wa kuipandisha hadhi ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami? Kwa sababu pia iko kilomita mbili kutoka mpaka wa Kilimanjaro na Arusha.

**MWENYEKITI:** Ahsante jibu kwa swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hii barabara ina changamoto lakini Mheshimiwa Mbunge hapa anaomba kama barabara inaweza ikapandishwa hadhi, kupandishwa hadhi ni mchakato maana yake unaitoa barabara kutoka TARURA kwenda TANROAD ambayo ni Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge jambo hili inabidi lianzie kwenye halmashauri yake liende kwenye ngazi ya mkoa kwenye kikao cha halmashauri cha barabara halafu walete kwenye ngazi nyingine ya kitaifa tutaona namna ya kufanya kama inakidhi vigezo basi itapewa hadhi hiyo ili iweze kupata fedha za kutosha na iweze kutengenezwa na wananchi wa eneo hilo waweze kupata huduma kama ambavyo ndiyo matarajio Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante bado tuko Ofisi ya Rais TAMISEMI swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga, kwa niaba Mheshimiwa Mollel.

Na. 43

### **Hitaji la Shule ya Sekondari ya Viziwi - Mwanga**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE (MHE. AMINA S. MOLLEL)** aliuliza:-

Shule ya Viziwi Mwanga hutoa Elimu ya Msingi kwa Watoto wasiosikia na wasioongea kwa Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Arusha; wanapohitimu Elimu ya Msingi, Wanafunzi hao hujinga na Shule za Sekondari za kawaida ambazo hazina Walimu wenye Taaluma Maalum, vifaa na mazingira rafiki kwa Watoto wenye ulemavu:-

Je, ni lini Serikali itajenga Shule ya Sekondari Maalum kwa Watoto Viziwi (wasiosikia na wasioongea)?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa wanafunzi viziwi inatolewa katika Shule maalum 17 za Msingi na vitengo maalum 120. Shule hizi za Msingi zina jumla ya wanafunzi 7,212 na jumla ya walimu 885 wataalam wa kufundisha wanafunzi viziwi. Vilevile, ipo Shule maalum moja ya Sekondari na vitengo maalum 23 vya sekondari. Shule hizi za sekondari zina jumla ya wanafunzi viziwi 1,778 na jumla ya walimu 302 wataalam wa kufundisha wanafunzi viziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari Maalum ya Viziwi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru katika eneo la Tengeru (Patandi), ambayo mwaka 2020 kwa mara ya kwanza itaanza kudahili wanafunzi viziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kutoa wito kwa wadau wote wa elimu wenye nia ya kujenga Shule za Watoto wenye ulemavu wakiwemo viziwi, wafanye hivyo,

Serikali itatoa vibali husika kwa kuzingatia taratibu na sheria husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza kabla ya kuuliza swali la nyongeza ninaomba kutoa ufanuzi kwamba hawaitwi wasiosikia au wasioongea kwa ujumla wao wanaitwa viziwi kwa hiyo, ni vizuri zaidi kuwa makini na haya majina ili kuepuka wakati mwingine kuonekana kwamba kwasababu neno asiyesikia ina maana ni mtu mtukutu. Asante naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu tatizo hili ni kubwa maeneo mengi na kwa namna moja au nyininge wanaochagua hawazingatii kwa kujua kwamba huyu mtoto ana mahitaji pengine maalum au asiye na mahitaji maalum. Sasa je, ni lini Serikali itaweka mchakato maalum kwa kuzingatia kwamba katika kila mkoa angalau kuwepo na shule zitakazosaidia watoto wenyewe mahitaji maalum wakiwemo viziwi?

Swali la pili uhaba wa waalimu ambao hawana ujuzi wa kufundisha wanafunzi kwa maana kwamba wanafunzi wote wanachanganywa pamoja hata wale viziwi.

Je, sasa upi mkakati maalum wa Serikali katika kuhakikisha kwamba walimu wenyewe mahitaji maalum wanasantazwa katika shule zetu za msingi ili basi waweze kusaidia wanafunzi wetu hasa wenye mahitaji maalum? Ahsante

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunao upungufu wa shule hizi katika maeneo mbalimbali ya nchi na kama nilivyosema

kwenye jibu langu la msingi tumeanza na hizo na kuna baadhi ya maeneo kuna shule zingine uwezo wa Serikali ukiruhusu basi tutajenga karibu kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa hao watoto wapate huduma ya taaluma katika yao ya karibu bila kupata usumbufu ili kwasababu pia kuna kuwa na shida hata kuwatoa nyumbani na kuwapeleka hata kwenda kuwaangalia wanapata matatizo ya magonjwa na mambo mengine hiyo ndiyo shida. Lakini tunatoa wito pia kwenye jibu letu kwamba hata wale wadau ambao wanaweza wakajenga shule kama hizi tumeshuhudia shule nyingi zipo Tanzania hapa za *private* na za watu binafsi na wadau mbalimbali lakini nyingi zinalenga watoto hawa ambao wanauelewa wa kawaida na hawana aina yoyote ya ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukipata mdau mwingine pia ambaye anaweza akajenga shule za aina hii za mahitaji maalum tutampa *support* kama Serikali ili shule iweze kufunguliwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia swali lake la msingi anaulizia kama kuna namna ya kuweza kupeleka walimu katika kila mahali. Ni kweli kwamba kuna upungufu lakini kila tunapokuwa na ajira ya walimu tunazingatia pia walimu wa mahitaji maalum. Na swali lake anapozungumza hapa kwamba tusaidiane pia namna ya kutambua watoto katika kila eneo iliokea pia kwamba tunatoa taarifa kuwatambua watoto hao katika maeneo yao lakini pia maeneo mengine wanafichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa kuwaomba pia Waheshimiwa Wabunge na watanzania wote inapotokea kuna mwanafunzi wenyewe ulemavu katika eneo hilo lakini pia tukasema hawa watoto ukiwatenga wenyewe wenyewe pia imekuja hoja inaitwa elimu jumuishi ili watoto hawa waanze kuzoeana wanasaídiana ili hata mtoto akizaliwa katika jamii yetu kwenye familia ni mlemavu asitengwe hiyo ni nia ya Serikali tuwe na elimu jumuishi lakini

wanapokuwa na ulemavu mkubwa zaidi wanapata mahitaji mahsusini na usimamizi mahsusini ili waweze kupata huduma vizuri sana. Ahsante!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniona sambamba na majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali wilayani Moshi Vijiji kuna shule ya viziwi ya Vona wamejitali kwa muda mrefu sana kupata ushirikiano na Serikali lakini imeshindikana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kufuatana na mimi mpaka Vona ili aone ni jinsi gani Serikali itaisaidia shule hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwa kifupi jibu hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari sana kuambatana na mwalmi tukatembelee watoto wetu hao wazuri tukaone mazingira hayo na ni kuhakikishie Mheshimiwa Mbunge huo ushirikiano uliokosekana sasa utapatikana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** ahsante, Waheshimiwa tunaendelea tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Pauline Phillipo Gekul Mbunge wa Babati mjini

Na. 44

**Kuboresha Barabara Zinazoelekeea Hifadhini**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Miundombinu mibovu ya barabara zinazoelekeea Hifadhini husababisha Watalii kuwa wachache Mathalan; barabara inayotoka Iringa Mjini hadi Hifadhi ya Ruaha kilometra 104 ni ya vumbi na vilevile barabara ya kutoka Babati Mjini hadi Tarangire kilometra 20 ni ya vumbi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hizo kwa kiwango cha lami ili kuwavutia Watalii wengi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu ya swali hilo, namuona Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kanyasu.

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Iringa Mjini kuelekea Hifadhi ya Taifa Ruaha ambayo inajulikana kama barabara ya Iringa – Msembe ni barabara ya Mkoa inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Iringa. Barabara hii ina urefu wa kilomita 104 kati ya hizo kilomita 18.4 ni za lami na kilomita 85.6 ni za changarawe. Barabara hii inapitia katika maeneo muhimu ya makumbusho ya Mtwa - Mkwawa (Kalenga), maeneo yenye kilimo cha Mpunga na Mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, TANROADS imefanya Upembuzi yakinifu, Usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Kazi hii imefanywa na Mhandisi Mshauri M/s ENV Consult (T) Ltd wa Dar es Salaam na tayari imekamilika. Ambapo jumla ya shilingi billioni 4.22 zimetengwa Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Taasisi zake imekuwa ikishirikiana na Mamlaka zingine kuhakikisha kwamba barabara mbalimbali zinazoelekeea maeneo ya Hifadhi zinapitika wakati wote kwa kufanya ukarabati wa mara kwa mara. Kwa mfano, Hifadhi ya Taifa Tarangire imeshirikiana na TARURA kurekebisha barabara ya kutoka

Minjingu kwenda Tarangire yenyе urefu wa kilometra 7 na barabara ya kutoka lango la Sangaiwe kwenda kijiji cha Usole – Mwada – Sangaiwe kwa kufanya matengenezo ya kuchonga na kuweka moram.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, usanifu wa barabara ya Minjingu – Tarangire kilometra saba kwa kiwango cha lami umekamilika na sasa inatafutwa fedha kwa ajili ya ujenzi. Barabara kutoka Babati Mjini hadi Hifadhi ya Taifa Tarangire kilometra 20 inafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara kila mwaka kwa ushirikiano kati ya TARURA na Hifadhi ya Taifa Tarangire.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi niulize maswalli mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri nikushukuru pia kwa majibu ya Serikali ambayo ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mheshimiwa Waziri, Serikali haioni kwamba sasa badala ya barabara hii inayotoka Babati mjini hizi kilometra 20 kuendelea kuwekewa fedha za *maintenance*, ni vizuri wakatenga fedha za kuweka lami hizo kilometra 20 hadi lango la Tarangire ili watalii wanapofika Babati wasafiri vizuri mpaka hapo Hifadhini kuliko ambavyo sasa ni *rough road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali la pili mionganoni mwa vitu ambavyo vinachochea utalii wetu ni pamoja na miundombinu mizuri barabara pamoja na viwanja vya ndege uwanja wetu wa Mkao wa Manyara ambao uko pale Magugu sasa haujawahi kutengewa fedha na watalii wamekuwa wakilazimika sasa watue Arusha na watembee umbali mrefu.

Je, Serikali iko tayari kututengea fedha haraka iwezekanavyo kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mkao wa Manyara ili watalii waweze kufika mapema hifadhini Tarangire?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo ya nyongeza, kwa ufupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu barabara hii ya Babati kwenda Tarangire kwenye lango niseme iko kwenye mipango na sasa kama kinachofanyika ni kuhakikisha kwamba inakuwa vizuri ndiyo maana Bunge lako imetutengea fedha kwa ajili ya kufanya maboresho makubwa ili kuondoa usumbufu kabisa ili wananchi wakati tunafanya harakati za ujenzi watalii waweze kupita bila shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu ujenzi wa uwanja wa ndege kwanza nipongeze Serikali ya mkoa, kupata eneo hill la Mbuyu wa Mjerumani kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege na nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla ni kwamba Wizara yangu kuititia *TIA* inaendelea na usanifu ili sasa tuweze kujua namna uwanja utakavyokuwa na gharama zake na hatimaye tuweze kujenga uwanja huu wa ndege. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Yusuf Salim Hussein Mbunge wa Chambani.

Na. 45

### **Chuo kwa ajili ya Utalii wa Baharini**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN** aliuliza:-

Utalii wa baharini (*Diving* unakua kwa kasi sana na hakuna chuo kinachotoa elimu hiyo hapa nchini):-

Je, Serikali haioni kuwa tunapoteza ajira nyingi kwa vijana wetu?

## **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya Uzamiaji kwenye Maji kwa kutumia vifaa vyta kupumulia ndani ya maji (*Self Contained Underwater Breathing Apparatus – SCUBA Diving*) yanatolewa nchini na Chuo cha Wakala wa Mafunzo ya Uvubi Tanzania – FETA, Kampasi ya Mbegani, iliyopo Bagamoyo. Kwa sasa chuo kinakabiliwa na uchache wa watumishi wenye utaalalm kwenye fani hiyo. Aidha, wakufunzi watatu (3) wapo nje ya nchi (Uingereza wawili na Uturuki mmoja) kwa ajili ya mafunzo katika fani hizo ambapo wanatarajiwa kurejea nchini mwaka 2020/21. Baada ya kurejea kwa wakufunzi hao, chuo kitaendelea kutoa mafunzo hayo mwakani. Aidha, vyuo vyote vina kozi ya lazima ya *Swimming na Snorkelling* ambayo inahusisha kipengele cha *diving* kwa wanafunzi wanaochukua masomo ya Sayansi ya Viumbe Maji (*Aquatic Science*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvubi kuititia taasisi yake ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu inaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha vituo vya uzamiaji (*Diving Centres*) ambapo sambamba na vituo hivyo kutoa elimu ya uzamiaji kwa wananchi katika maeneo ya fukwe za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Hatua hii itawezesha kuhudumia watalii wa ndani na nje ya nchi pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi na pia kusaidia kuimarisha aina hiyo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vituo vya Sekta binafsi vinavyotoa huduma ya uzamiaji pamoja na elimu ya uzamiaji nchini vinapatikana katika maeneo ya Hifadhi ya Bahari ya Mafia, Mkoani Pwani (Big Blue, Shamba Kilole na Mafia Island Dive); Maeneo tengefu ya Mkoa wa Dar es Salaam (Yatch Club na White Sands); Hifadhi ya Bahari ya

Silikanti Tanga (Kasa Dive na *Fish Eagle Point*) na Fukwe za Mkoa wa Mtwara (*Mikindani Diving Centre*).

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yusuf Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nashukuru pia majibu ya Waziri kwamba amekiri kwamba Serikali haina Chuo inachotoa haya mafunzo, mafunzo yanayotoa ni ya *swimming* na *snocking* mafunzo haya ni muhimu sana kwa maisha ya watu wetu nchi yetu imezungukwa na bahari na maziwa na watanzania wengi wanatumia bahari na maziwa na mito kwa ajili ya kutafuta riziki zao.

Je, Serikali sasa haioni ni muda muafaka wa kuanzisha chuo na kama hawana walimu kutafuta walimu kuja kufundisha ili kupusha maafa kama haya yaliyotokea Kilindini Kenya mtu amezama kwa siku saba hajatolewa katika bahari?

Swali la pili nchi yetu kama nilivyosema imezungukwa na bahari na mito na watu wetu asilimia kubwa ndiyo wanatumia bahari na mito kwa ajili ya kutafuta riziki zao.

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muda muafaka kutafuta vijana wakawafundisha *risk who divers* kwa ajili ya uokoaji zinapotokea ajali za baharini? Nakushukuru

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo mawili ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kweli kwamba kama nchi hatuna chuo maalum kinachofundisha *diving* peke yake lakini vyuo vyetu vyote vya uvuvi ukianzia Nyegezi, Mbegani, Kunduchi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa wanafunzi wote wanaosoma masomo ya uvuvi au masomo ya sayansi ya majini lazima wasome somo hilo kama sehemu ya masomo ya lazima ya

kufaulu na katika jibu langu la msingi nimesema kutohana na uhaba wa wataalamu Serikali ilikwisha chukua hatua ya kipeleka wataalamu watatu nje ya nchi ili wataalam hao watakoporejea waweze sasa kulichukulia somo hilo kama somo muhimu kwa ajili ya kwanza shughuli ya utalii lakini pili kwa ajili ya uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba umefika wakati ambapo suala hili tunalichukulia kwa uzito mkubwa na mara wataalam hawa watakoporejea watatoa mafunzo kwa vijana wetu na kwa watu wote wanaoshughulika na kuongoza watalii

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba Kisiwa cha Mafia ni maarufu na ni eneo zuri sana kwa ajili ya *snorkelling, scuba diving* na aina nyingine za uzamiaji:-

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuleta hicho chuo ikakiweka Mafia ili wananchi wa Mafia wanufaiké nacho? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo la nyongeza Mafia au Mwanza.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dau, Mbunge wa Mafia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Yusuph; baada ya wataalam hao kurejea; na kwa sababu wataalam hao wametumwa na Serikali kwenda kuchukua masomo hayo maalum kuititia vyuo ambavyo viro; ninachowea

kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba katika maeneo ambayo tutayapa kipaumbele ni pamoja na Kisiwa cha Mafia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea. Tunahamia Wizara ya Kilimo. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo. Linalekezwa kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 46

### **Changamoto Zinazomkabili Mkulima wa Tumbaku**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Licha ya juhudi kubwa za Serikali kumsaidia Mkulima wa zao la Tumbaku, bado zipo changamoto anazokabiliana nazo ikiwemo kutopata makisio na pembejeo kwa wakati, masoko ya uhakika na wanunuzi wengi wa Tumbaku ili kuleta ushindani wa bei:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa changamoto hizo ili Mkulima ajiedeleze kiuchumi?

(b) Je, Serikali inashirikianaje na Wakulima wa Urambo ili wawe na Kiwanda cha Tumbaku Urambo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukuwa hatua mbalimbali ili kuondoa changamoto kwenye tasnia ya tumbaku zinazohusiana na baadhi ya wakulima kutopata makisio ya uzalishaji, upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na Masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msimu wa kilimo wa 2019/2020 makisio ya uzalishaji wa tumbaku ya jumla ni kilo milioni 42 yalitolewa mwezi Julai na Kampuni tatu ambazo ni *Alliance One, Japan Tobacco International Leaf Services* na *Premium Active Tanzania Limited*. Kutolewa mapema kwa makisio hayo kumewezesha Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa Tumbaku kuagiza mbolea kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya mbolea kwa zao la tumbaku nchini ni tani 14,951 za mbolea ya *NPK* na tani 3,000 za mbolea ya kukuzia. Mbolea yote imeshapokelewa nchini na usambazaji unaendelea kwenye Vyama vya Msingi. Kwa Wilaya ya Urambo hadi kufikia tarehe 31 Oktoba jumla ya tani 1,774 zimesambazwa katika mahitaji ya tani 2,160 ya mbolea sawa na asilimia 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha tumbaku inayozalishwa hapa nchini inapata soko la uhakika, Serikali inaendelea na mazungumzo ili kufungua soko la tumbaku katika nchi wanachama wa *COMESA* (Algeria, Misri na Sudan), ambao niwateja wakuu wa tumbaku ya Moshi inayozalishwa nchini. Serikali ilituma ujumbe wa wataalam watano kwenda nchi ya China kujifunza namna bora ya uzalishaji wa tumbaku inayohitajika kwa soko la China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufutia mafunzo hayo, aina tano za mbegu za tumbaku zimeingizwa nchini kwa ajili ya kufanyiwa majoribio katika maeneo ya uzalishaji wa tumbaku nchini. Tayari majoribio kwenye jumla ya eneo la ekari 10 yanaendelea nchini chini ya usimamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku (*TORITA*) na Bodi ya Tumbaku. Aidha, Serikali imefanya mazungumzo na Kampuni ya *British American Tobacco Ltd* ambayo imeonesha nia ya kununua jumla ya kilo milioni nane ya Tumbaku inayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba wawekezaji wa tumbaku waliopo nchini wanaendelea kuongeza uwekezaji, mwezi Septemba, Wizara ya Kilimo ilikutana na Kampuni za wanunuzi wa tumbaku kwa lengo la kujadili na kupata ufumbuzi wa changamoto zilizopo.

Kutokana na kikao hicho, ilikubalika kuondoa kesi zilizofunguliwa na Tume ya Ushindani na kufanya makubaliano ya kiraflki nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, matatizo yanayohusiana na sula la kodi ya VAT, mchakato wa kuweza kupitia *VAT returns* kwa taasisi hizo nne unaendelea; na pale ambapo madai yao ya halali yataonekana, basi Serikali itawalipa kufuatana na utaratibuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Urambo imetoa ekari 20 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kusindika tumbaku. Taratibu za umilikishwaji wa ardhi kisheria kwa ajili ya kiwanda zinakamilishwa. Aidha, Serikali itashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Benki ya *TADB* na Chama Kikuu cha Ushirika cha Urambo ili kuhakikisha kuwa kiwanda hicho kinaanzishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kwa niaba ya wananchi wa Urambo, niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika jibu lake imekiri kwamba ilikuwa na kikao na hawa wanunuzi wa tumbaku wanaotaka kuondoka nchini:-

Je, Serikali inaweza kutuambia kwamba baada ya mazungumzo haya ya mwezi wa Tisa imefikia muafaka gani ili kampuni hizi ambazo zilikuwa zinanunua tumbaku nyingi hasa Urambo na Tabora kwa ujumla waendelee kununua tumbaku na pia kulinda ajira ya wale waliokuwa wakifanya kazi katika kampuni hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaotishia kuondoka, kama kweli hawatakubaliana na Serikali waondoke, Serikali itafanya nini kuhusu viwanda ambavyo walikuwa wamenunua kama kile cha Morogoro na pia

magodauni mengi ambayo walikuwa wamenunua sehemu nyingi sana kule ambapo wanunu tumbaku? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili ya nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo dhamira ya Serikali kuona kwamba kuna mwekezaji ye yote ambaye amewekeza anaondoka nchini. Kwa hiyo, dhamira yetu ni kuendelea kufanya maongezi nao; na kufuatia maongezi tuliyofanya mwezi Septemba, kampuni tatu za tumbaku zilirudi kununua tumbaku ambayo ni maarufu kwa jina la makinikia ambayo ni *un-contracted tobacco*. Wameenda kununua jumla ya kilo millioni saba kat i ya kilo millioni 12 ambazo zilikuwa zimebaki mikononi mwa wakulima. Kwa hiyo, tunaendelea kuongea na makampuni haya ili yaweze kuendelea kununua tumbaku na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kampuni ambayo imeonesha nia ya kuondoka na kufunga shughuli zake, Kampuni ya *TLTC*; hoja za *TLTC* zilikuwa ni tatu. Moja, ni suala la kesi iliyokuwepo kati yake na Manispaa ya Morogoro. Tumefanya kikao mwezi wa Kumi katika Mji wa Morogoro na makubaliano yamefikiwa na kesi hiyo kutolewa nje ya Mahakama; na wamefikia *settlement agreement* ambayo wanaweza kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, lilihusu *VAT returns*, nami nitumie nafasi hii kuishukuru Wizara ya Fedha kwa dhati kabisa na kuwashukuru *TRA*, wameonesha *commitment* na wame-deploy team kwa kampuni zote za *tobacco* kuweza kupitia *VAT returns* zao za muda mrefu na mwezi huu wa Novemba mwishoni ndiyo yalikuwa makubalino juu ya kusaini makubaliano ya *transfer pricing* na *VAT returns*. Hatua zinaendelea vizuri na wawekezaji wameonesha *positive results* kwa kuonesha kwamba hatua za Serikali zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya tatu ilikuwa ni suala la kesi za *FCC*. Tumefanya vikao na Serikali imewaa giza *FCC* kukaa na wafanyabiashara hawa ili kuweza kutafuta njia sahihi ya kuwa na suluju badala ya kuendelea kuwaadhibu kwa sababu inaathiri sekta ya kilimo na inaathiri Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali hatuna nia wala dhamira ya kuhakikisha kwamba kuna mwekezaji yeyote anaondoka, lakini akiondoka, ataondoka kwa mujibu wa sheria; na kwenye ubinafsishaji kulikuwa kuna mkataba na taratibu za kurudisha mali hizo ziendelee kubaki ndani ya nchi. Utaratibu upo katika mkataba waliobinafsishiwa *infrastructure* zote kuanzia kiwanda na magodauni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba mali zote za Watanzania zitaendelea kubaki kwa ajili ya maslahi ya Watanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wetu siyo rafiki. Mheshimiwa Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri; na kwa kweli nikiri kwamba huyu kijana ameanza vizuri na uendelee vizuri hivyo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulishughulikia suala hili la tumbaku kwa hasa huyu mwekezaji *TLTC* ambaye anaondoka; *TLTC* alikuwa anafanya biashara na vyama 97 hapa nchini. Katika hivyo 97, Chunya nina vyama sita au saba ambavyo vilikuwa vinafanya biashara naye na mpaka sasa hajatoa makisio. Kwa hiyo, kuna wasiwasi kwamba kwa msimu huu tunaoanza nao haviwezi kufanya biashara.

Je, Serikali itazibaje pengo hili ili vyama hivi 97 nchi nzima vifanye biashara mwaka huu? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwatoe hofu wakulima wa Chunya, Tabora na maeneo mengine, waendelee kuandaa mbegu zao, kwa sababu tuna maongezi na kampuni ya *British American Tobacco* ambao tumefanya kikao mwezi huu wa Novemba tukiwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha. Mchakato wa maombi hayo umeenda Wizara ya Fedha, unaendelea kuangaliwa. Vile vile wameonyesha nia ya kununua kilo milioni nane kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe hofu wakulima wa maeneo ya Chunya kwamba waendelee kufuata utaratibu wa *best practice* ya kuzalisha *tobacco*, wasiwe na hofu. Ni dhamira ya Serikali kumwongeza *player* mwingine ndani ya soko la *tobacco*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TLTC* hivi karibuni viongozi wao watakuja kuongea na Serikali; wameshaonesha nia ya kurudi sokoni. Kwa hiyo, tuendelee kuvuta subira na niwatoe hofu wakulima wa tumbaku kwamba suala la *TLTC* litafika mwisho, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo hili. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, muda wangu siyo rafiki. Swali linalofuata linaelekezwa kwa Waziri wa Nishati na linaulizwa na Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo kwa niaba...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Huku!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

Waheshimiwa Wabunge, niwaambie kitu kimoja, Kambi ya Upinzani mnanichanganya. Nina maandihi hapa, sitaki kumtaja aliyeniandikia kwenye uongozi huku.

Nimeandikiwa kwamba atakayeuliza kwa niaba yake ni Mheshimiwa Anatropia Theonest. Sina jina la mtu mwingine zaidi ya hapo. Uliza swali.

Na. 47

**Uwekezaji wa Viwanda kwa Kutumia Gesi Asilia**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST (K.n.y. MHE. SAED A. KUBENEAE) aliuliza:-**

Gesi asilia iliyogundulika nchini ni takribani ujazo wa trillioni feet 56:-

(a) Je, uwekezaji wa viwanda vinavyotumia gesi asilia kwa ukanda wa Kusini umefikia wapi na ni wa kiwango gani?

(b) Je, mpango wa kujenga kiwanda cha kuchakata gesi asilia bado upo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi asilia iliyogundulika nchini hadi sasa ni futi za ujazo trillioni 57.54. Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es Salaam ni maeneo yaliyonufaka na shughuli za uwekezaji katika viwanda vinavyotumia gesi asilia. Matumizi ya gesi asilia nchini yalianza tangu mwaka 2004 ambapo kufikia mwezi Oktoba, 2019, jumla ya viwanda 48 vimeunganishwa na mtandao wa gesi asilia. Viwanda hivyo vinatumia gesi asilia kama nishati na vingine vinazalisha umeme kwa matumizi ya viwanda.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (*LNG*) unaendelea. Kwa sasa utekelezaji wake umefikia hatua ya majadiliano ya

mkataba wa nchi husika (*Host Government Agreement*) kati ya wawekezaji na Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni wiki iliyopita tu tumepta taarifa ya kuvuja kwa bomba la gesi, suala ambalo ni la hatari lakini ni kudra za Mwenyezi Mungu hakuna madhara yaliyojitokeza. Sasa licha ya juhudzi za Serikali kuunganisha viwanda na gesi, nini hatua wanazochukua kunusuru hali ya namna hiyo isijitokeze kwa ajili ya kunusuru maisha ya wat? Swalii la kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; katika utawala wa Awamu ya Nne kazi kubwa ilifanyika ya kuhakikisha gesi inazalishwa na kusambazwa viwandani kama njia au nishati mbadala, lakini kwa sasa tunaona nguvu kubwa imewekwa kwenye *Stiegler's* na miradi mingine ya umeme wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swalii; Kwa kuwa mradi wa gesi ulikuwa haujatumika kwa asilimia mia moja na tunaona tumehamia mradi mwingine, ni nini mkakati uliopo kuhakikisha mradi wa gesi unazalishwa na unatumika kwanza katika *full capacity* kabla ya kuhamia miradi mingine? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili ya nyongeza, kwa ufupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatropia katika swalii lake la kwanza ameeleza namna ambavyo taarifa ilitolewa rasmi na *TPDC* kuhusu kuvuja kwa gesi kwenye maeneo ya Somanga Fungu. Kama anavyofahamu tangu imeanza kujengwa miundombinu ya gesi, tangu gesi imeanza kutumika kwa mara ya kwanza 2004 mpaka sasa ni tukio la kwanza. Kwa hiyo, ni wazi kabisa miundombinu iliyojenga taratibu zote za *precaution* juu ya masuala ya bomba yalizingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, taarifa rasmi imetolewa, wataalam wa *SONGAs* wakishirikiana na *TPDC* na Wizara ya Nishati walikuwa eneo la tukio na kila kitu kilifanyiwa kazi na kwa sasa kwa kweli hali imetengamaa na tutaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba matukio kama haya hayajitokezi na kama ambavyo inaonesha ni mara ya kwanza. Kwa hiyo, nataka nimtaarifu kwamba hatua zote zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la pili ameulizia namna gani tutaendelea kuwekeza katika miradi ya gesi na amehusisha kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza kwenye mradi wa *Mwalimu Nyerere Hydro Power*. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Anatropia kwamba katika suala zima la uwekezaji wa masuala ya nishati hususan ya umeme, vipo vyanzo mbalimbali; Serikali yoyote lazima itumie vyanzo mbalimbali mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaposema masuala ya gesi, umeme wa maji, umeme wa makaa ya mawe, umeme wa upepo na umeme wa nishati mbadala pia. Kwa hiyo, Serikali ilipoamua kujielekeza kwenye mradi huu wa *Mwalimu Nyerere Hydro Power*, ni kuhakikisha kwamba lengo la uzalishaji wa megawatt 10,000 ifikapo 2025 linafikiwa kwa mradi huu mkubwa ambao utazalisha *megawatt* 2,115.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepata kusema ndani ya Bunge chanzo hiki cha kuzalisha umeme wa maji kina nafuu, kinagharimu shilingi 36 tu kwa *unit*, lakini pia Serikali inaendelea na uwekezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa gesi. Kwa mfano, hata sasa hivi kuna mradi wa kuzalisha umeme wa gesi Mtwara wa *Megawatt* 300 lakini pia upo Mradi wa Somanga Fungu *Megawatt* 330.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara nchini Japan, aliambatana na Maafisa kutoka *TPDC* akiwepo Mkurugenzi Mtendaji lakini pia hivi karibuni ametoka Urusi, kote kule wamezungumza na wawekezaji

mbalimbali na amewaalika kwa niaba ya Serikali kuja nchini Tanzania hapa kuwekeza katika miradi ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kujielekeza kwenye miradi ya gesi na miradi mingine yoyote ili kupata *energy mix* ya uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa, muda wangu mnaouona hata ninyi. Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa matumizi ya gesi asilia siyo kwa viwandani tu, bali hata majumbani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba unapeleka gesi asilia kwenye majumba katika maeneo ya Ubungo, Manzese, Vingunguti, Mbagala, Gongolamboto, Tandika, Mwananyamala na Tandale; maeneo ambayo yana wakazi wengi ili kuwasaidia akina mama kupata nishati ya gesi kwa bei nafuu; pia katika kupunguza gharama za mkaa na uhifadhi wa mazingira?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, kwa kifupi sana. Maana ni kupeleka gesi kwenye maeneo hayo, mipango yenu; kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi anapozungumzia masuala ya usambazaji wa gesi majumbani, anamzungumzia mwanamke ambaye ndio mtumiaji mkubwa wa rasilimali ya gesi majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimtaarifu kwamba ni mkakati wa Serikali kwamba kwanza mpaka sasa zaidi ya kaya 500 zimeshasambaziwa gesi asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara. Kazi inayoendelea sasa kwa

mwaka 2019/2020 tuna matarajio ya kaya zaidi ya 1,000 kuzifika na kazi inaendelea na mpaka sasa vifaa vyote vya kuunganishia yakiwemo mabomba, mita za matumizi ya gesi vimeshafika na vimeshafungwa na vipo katika nyakati za majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maeneo aliyyataja ikiwemo Tandale, Mwananyamala, Mbagala na maeneo ambayo Mbunge anawakilisha, nataka nimthibitishie kwamba Serikali imedhamiria na ndiyo maana imetenga katika mpango mzima matumizi ya gesi, kiasi cha futi za ujazo trillioni 0.7 kwa ajili ya matumizi ya majumbani ili kuokoa mazingira pia. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Swali la msingi lilikuwa linaulizia mradi wa *LNG* wa Lindi. Napenda kufahamu kutoka Serikalini, ni lini Serikali italipa fidia wakazi wa Likong'o, Mto Mkavu na Mchinga ambao wapo tayari kupisha mradi huu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo kwa ufupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri, lini mtalipa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bobali, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza lini fidia italipwa kwa wakazi wa maeneo ya Likong'o, Mchinga na Mitwelo Mkoani Lindi ambao wamepisha eneo kwa ajili ya Mradi huu mkubwa wa *LNG*. Napenda nimaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba mwezi uliopita wataalamu wa *TPDC* na Wizara ya Fedha na Mipango walikuwa ziara katika Mkoa wa Lindi kuhitimisha zoezi zima la tathmini. Matarajio yetu ifikapo Disemba 2019 zoezi la kuanza kulipa fidia kwa wakazi wa maeneo hayo litaanza na litaendelea na hatimaye kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwathibitishie wakazi wa Mkoa wa Lindi ambao kwa kweli kwa muda mrefu

wamekuwa wakiulizia fidia hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano sasa iko tayari kuwalipa. Fidia iliyotengwa ni kiasi cha shilingi bilioni 56 na mambo yote yamekamilika na itaanza kulipwa na wakati huo sisi Serikali na wawekezaji tunaendelea na mazungumzo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, mambo mazuri hayo Mheshimiwa Bobali.

Tunaendelea Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kwa niaba yake Mheshimiwa Mwamoto.

Na. 48

**Ahadhi ya Ujenzi wa Barabara ya Mika – Utegi – Shirati**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais akiwa kwenye ziara ya kujinadi wakati wa kampeni Wilayani Rorya aliwaahidi wananchi wa Rorya kujenga barabara ya lami kutoka Mika-Utegi hadi Shirati;lakini hadi sasa ahadi hiyo haijatekelezwa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza ahadi hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali hilo linajibowiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mika – Utegi – Shirati hadi Ruari Port ni barabara ya mkoa inayosimamiwa

na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Mara. Barabara hii ina urefu wa kilometra 48.73. Kati ya hizo, kilometra 40.13 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na kilometra 8.6 zimejengwa kwa awamu kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza maandalizi ya kuijenga barabara hii (km 48.73) kwa kiwango cha lami kwa kuifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hiyo inafanywa na Makampuni ya *Cordial Solution Ltd.* na *Atkins Tanzania Ltd* yote ya Tanzania. Wakati makampuni hayo yakiendelea na kazi, yaliongezewa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya usalama na ulinzi kutoka Shirati – Masonga hadi mpakani mwa Tanzania na Kenya (km 16.4). Gharama ya kazi zote ni shilingi milioni 679.621 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika na fedha za ujenzi kupatikana. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii Serikali itaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2019/2020, barabara hii ya Mika – Utigi – Shirati imetengewa shilingi milioni 630.148 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa barabara ambayo inatoa Makao ya Wilaya kwenda Utigi inasumbua kwa muda mrefu na kwa muda mrefu imekuwa ni ahadi ambayo bado haijafanyiwa kazi. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kuiangalia wakati inasubiri hiyo ahadi ya Rais ya muda mrefu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa ahadi za Rais ziko nchi nzima na Wilaya ya Kilolo pia tulikuwa na

ahadi kama hiyo ambapo Rais alikuwa amesema barabara ya kutoka Kilolo - Iringa ingeanza kujengwa mara moja. Sasa tayari tunaelekea kwenye uchaguzi na ilikuwa ahadi ya kabla ya uchaguzi. Je, Serikali inasemaje ili wananchi wa Kilolo wajue umuhimu wa Serikali ya Awamu ya Tano? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Majibu kwa kifupi sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Eng. Kamwelwe.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme Serikali inatekeleza maagizo na ahadi zote za llani ya Chama cha Mapinduzi na pia itaendelea kutekeleza maagizo yote ya Viongozi wetu Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Utigi itajengwa kutokana na upatikanaji wa fedha ndiyo maana usanifu umeendelea. Kwa hiyo, tukishamaliza usanifu, tukapata fedha itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini barabara yako Mheshimiwa kama ambavyo tumeshaongea hata nje ya hapa kwamba barabara ile tayari imeingizwa kwenye Mpango wa Benki ya Dunia. Ni taratibu zinaendelea baadaye itajengwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kuna wengine wameuliza mara nydingi sana, Mheshimiwa Kigua Omari.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujenga daraja la muda la Nderema ambalo linaunganisha Wilaya ya Kilindi na Handeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipongeza Serikali, naomba niulize swalii la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mvua hizi hazikutegemewa na zimeharibu sana barabara kuanzia Handeni – Kibirashi - Songe – Gairo. Je, Serikali iko tayari kutuma wataalamu kwenda kuangalia hali ya uharibifu ili kuweza kurejesha mawasiliano katika eneo hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Kigua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitoe taarifa kwamba kwa mujibu wa usanifu wa barabara mvua zina *return period* tatu; kuna ya miaka kumi, hamsini na miaka mia moja. Mvua iliyonyesha juzi Tanga inaonekana ina *return period* ya miaka mia moja na ambayo *design* huwa hajumuishi *returned period* hizo lakini kwa mujibu wa swali lako Mheshimiwa Mbunge tuko tayari.

**MWENYEKITI:** Ngoja leo nicheze kidogo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeahidi kujenga barabara ya Kaliua - Chagu (km 48) na walituambia kwamba tayari walishapata mfadhili wa kujenga barabara hiyo. Ni lini sasa ujenzi wa barabara wa hiyo km 48 tu utaanza? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Lini utaanza?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza barabara hiyo siyo kilometra 48 ni kilometra 36, tenda tumeshatangaza wakati wowote tunasaini mikataba. Baada ya kusaini mikataba kuanzia tarehe ile tuliyosaini tutakwambia sasa tunaanza lini na tunakamilisha lini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara ya kutoka Mangamba - Kilambo - Msimbati itajengwa lini kwa kiwango cha lami kwa sababu ni Sera ya Serikali barabara zinazounganisha nchi kuzijenga kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni lini hiyo barabara inayounganisha nchi yetu na nchi jirani itajengwa?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba usanifu wa barabara hiyo ya kutoka Mtware Mjini - Kilambo tumeshakamilisha. Ni nia ya Serikali kuhakikisha tumeijenga kwa kiwango cha lami pamoja na daraja ili tuweze kuungana kwa daraja la pili kwa ajili ya kwenda Mozambique.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niulize swalilangu la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ziarani Wilayani Ruangwa alitoa maelekezo kwamba barabara kutoka Ruangwa - Nachingwea - Masasi na Ruangwa -Nachingwea - Nanganga zijengwe kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Rais akitoa kauli inakuwa ni maagizo. Je, lini upembizi yakinifu utaanza kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Upembuzi yakinifu lini utaanza?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii moja dogo la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Salma Kikwete ni kwamba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tumeshakamilisha. Ujenzi tumeshaanza na tayari tumeshajenga km 5. Kwa hiyo, maagizo ya Mheshimiwa Rais kama alivyosema ni sheria lazima tutayatekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Jimboni Ukerewe mwaka jana tarehe 5 Septemba, 2018, alitoa maelekezo ya ujenzi wa km 14 za lami kutoka Lugeze - Nansio mjini. Nataka kujua ni hatua ipi imefikiwa ili ujenzi huo uweze kuanza? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu barabara hii ameifuatilia muda mrefu na matokeo yake niseme kwamba usanifu wa barabara hii umeshaanza ukikamilika tutajenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

ahsante. Ahadi hizi za Rais ziko maeneo mengi na Vunjo

maeneo ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo iliahidiwa kujengewa barabara kwa lami km 7 na sasa kuna mafuriko eneo la *lower area* Kahe kuanzia Fungagate, Kahe, Kiomu mpaka maeneo ya Chekereni na Kilema *Hospital*. Barabara zote hizi ziliahidiwa na Mheshimiwa Rais kujengwa kwa kiwango cha lami na Serikali inajua. Ni lini watatekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais?

**MWENYEKITI:** Ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa nchi nzima.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme ni kweli ziko ahadi nyingi za Mheshimiwa Rais lakini katika barabara zimewekewa utaratibu wake. Tunaanza kwanza kukamilisha barabara kuu na zile zinazounga mipaka ya majirani zetu baadaye tutakwenda kwenye barabara za mikoa na tunarudi tena chini kwenye barabara hizo za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wewe tulia tu ni kwamba llani ya Chama cha Mapinduzi na ahadi za viongozi lazima zitekelezwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nangurukuru - Liwale ni ya vumbi na kokoto lakini naishukuru Serikali mwaka huu tumetengewa fedha shilingi milioni 300 kuanza usanifu wa kina. Hata hivyo, mvua zilizonyesha mwezi uliopita zimelaza watu siku tatu barabarani. Ni nini mkakati wa Serikali kuifanya barabara hii ipitike majira yote? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa ufupi tu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la  
Mheshimiwa Mbunge Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema  
mwenyewe tumetenga fedha kwa ajili ya kuifanya usanifu  
wa awali na usanifu wa kina, malengo ni kuijenga kwa  
kiwango cha lami ili haya matatizo ya mvua yanapojitokeza  
yasije yakaleta athari kwa wananchi. Hata hivyo kwa vile  
umetuambia tutafanyia kazi, hela ya *emergency* ipo ili  
tuweze kurudisha hiyo miundombinu wananchi waendelee  
kutumia barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
ahsante kwa kuniona. Barabara ya kutoka Iringa Mjini  
kwenda *Ruaha National Park* Iringa ni ahadi ambayo  
imetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
Awamu ya Nne na Awamu ya Tano na mpaka sasa ni  
upembuzi yakinifu tu unaendelea kwa miaka yote hiyo kumi  
na tano. Ni lini sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha  
lami ili kusaidia wale watalii wanaokwenda kule wawewe  
kwenda kwa ufasaha? (*Makofsi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la  
Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayoizungumza  
inaitwa jina Iringa - Msembe (km 104). Barabara hiyo ilikuwa  
imewekwa kwenye mafungu mawili; moja ni la ujenzi wa  
Uwanja wa Ndege wa Nduli ambao tumeshatangaza tenda  
na mkandarasi amepatikana wakati wowote tutasaini  
mkataba. Hizi km 104 tayari tumeshamaliza mpaka usanifu  
wa kina na tumeomba fedha kutoka Benki ya Dunia. Kwa  
hiyo, wananchi wa Iringa, tena ndiyo nimeoa kule, shemeji  
zangu wale, wala asiwe na wasiwasi barabara ile inajengwa.

**MWENYEKITI:** Swali la mwisho Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Serikali ina mpango gani wa kutenga pesa kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa barabara ya kutoka Njia Nne - Kipatimu (km 50)? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, lini mmatenga fedha kwa barabara hiyo ya Kipatimu, kwa ufupituu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la rafiki yangu Mheshimiwa Ngombale ,kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza mara nyingi juu ya barabara hii. Niombe tu tuwasiliane ili tuone kwa sababu kwenye Mipango Mikakati yetu katika Wizara tumeiweka katika Mpango ili tuweze kuendelea na hatua ya ujenzi wa lami. Kwa hiyo, tuonane na Mheshimiwa Mbunge ili nimpe taarifa za kukutosha ili aweze kutoa maelezo mengi kwa wananchi wake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nimewapa nafasi ya kutosha sasa naanza kazi. Bado tupo Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi.

Na. 49

#### **Tatizo la Mawasiliano ya Simu Kata ya Tura**

**MHE. MUSA R. NTIMIZI** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Tura katika Vijiji vya Mwamlela, Mmunyu na Nkongwa hawana kabisa mawasiliano ya simu licha ya umuhimu wa mawasiliano kiusalama na kiuchumi:-

Je, Serikali inatoa ahadi gani ya kupatikana kwa mawasiliano katika vijiji hivyo?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Eng. Nditiye. Waheshimiwa Wabunge, sasa angalieni muda.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Musa Ntimizi, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba uniruhusu nitoe ufanuzi wa Serikali kuhusu hoja iliyojadiliwa jana na baadhi ya wajumbe kuhusu sifa za mtu kuajiriwa kufanya kazi katika Shirika letu la Ndege la *ATCL*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la Ndege la *ATCL* na Serikali kwa ujumla limeainisha sifa mbalimbali zinazomruhusu Mtanzania kuweza kuajiriwa na Shirika hilo la Ndege. Sifa yetu ya kwanza kabisa ni Mtanzania ye yote mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea ambaye anafahamu kwa ufasaha lugha mbili za Kiingereza na Kiswahili. Pia Mtanzania huyo anatakiwa awe na Cheti cha Kuongoza Ndege au Cheti cha Kufanya Kazi ndani ya Ndege (*cabin crew*) ambacho kitakuwa kina mafunzo maalum ya usalama ndani ya ndege lakini na huduma kwa abiria ambao wanatumia ndege ile. Sifa nyingine ya tatu na muhimu kabisa ni lazima awe na leseni ya kuruka inayotolewa na Mamlaka ya Anga au *TCAA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ya ziada ni lazima awe na uelewa mkubwa wa masuala ya kitaifa, kidunia, utalii hasa nchini kwetu lakini awe ni mtu awe na hekima, ana *discipline* na *very ethical* na tutamchunguza katika hayo kuhakikisha kwamba anaweza kuajiriwa ndani ya Shirika letu la Ndege. Sifa nyingine zote zilizozungumzwa siyo ambazo zinazingatiwa na *ATCL* wala zinazingatiwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, nijibu swalii la Mheshimiwa Musa Ntimizi, Mbunge wa Igala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za mawasiliano kote nchini. Mwezi Julai, 2019, Mfuko ilitangaza zabuni ya awamu ya nne kwa ajili ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata 521 zenye vijiji 1,222. Kata ya Tura ilijumuishwa kwenye zabuni hiyo ikiwa na vijiji vya Karangasi, Mmunyu na Mwamlela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni hiyo ilifunguliwa na baada ya tathmini, tulipata wazabuni katika maeneo hayo. Utekelezaji utaanza baada ya mkataba kusainiwa mwezi Desemba, 2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kumekuwa na kawaida ya hawa *service providers* pamoja na ruzuku wanayopata kutoka Serikalini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote wanajikusanya kwenye maeneo ambayo tayari kuna mawasiliano badala ya yale madhumuni ya kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, kumekuwa na kawaida ya hawa *service providers* pamoja na ruzuku wanayopata kutoka Serikalini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote wamekuwa wanajikusanya kwenye maeneo ambayo tayari kuna mawasiliano badala ya yale madhumuni ya kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano. Mfano katika jibu

lake la swalı langu, katika Kata ya hiyo ya Tura, Kijiji cha Karangasi, tayari kuna mawasiliano lakini bado tena kumepelekwa mtandao mwingine, lakini yapo maeneo ambayo hayana mawasiliano. Je, kwa nini sasa hawa *Service Providers* wasipeleke mawasiliano kwenye maeneo yale ambayo hayana mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la pili, Kata ya Mmale yote haina mawasiliano; je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata hiyo ya Mmale? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Eng. Isack.*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Tura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hoja yako ulioizungumza ni kweli, kwamba *service providers*, watoa huduma za mawasiliano walikuwa wanajirundika kwenye maeneo machache, maeneo ambayo yana biashara kubwa au yana *population* kubwa ya watu. Baada ya kuliona hili, Bunge hili hili liliamua kuunda Mfuko wa Masiliano kwa Wote. Maana yake nini, ni kwamba ule Mfuko sasa unaenda kwenye maeneo yale ambayo, hawa wanaofanya biashara tu bila kujali utu wa mwanadamu Mtanzania, kwamba sasa tuwalazimishe waende kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu tayari, sasa hivi tunaenda maeneo yote bila kujali kwamba kuna faida kubwa na ndiyo maana hata kwenye maeneo anayoyahitaji Mheshimiwa Mbunge sasa, baada ya kutangaza hii tenda tutahakikisha kata zote, maeneo yote ili mradi yana Watanzania yanapata huduma ya mawasiliano. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swalı linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 50

## **Ujenzi wa Kituo Kidogo cha Polisi Sojo Nzega**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Kijiji cha Sojo katika Kata ya Isugule, Wilayani Nzega patajengwa Kituo kikubwa (*coating yard*) cha kuandaa mabomba yote ya mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga ambapo Kituo hicho kitakuwa na wafanyakazi zaidi ya 2,000; kutokana na ongezeko hilo la idadi ya watu mahitaji ya huduma za Jamii yatakuwa makubwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Kituo kidogo cha Polisi katika Kijiji cha Sojo ili kuhakikisha usalama kwa wananchi na mali zao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer Masauni*.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi iliona umuhimu wa kuwepo kwa Kituo cha Polisi katika Kijiji cha Sonjo ambapo ndipo kitakapojengwa kituo cha kuandaa mabomba ya mafuta toka Uganda kuja Tanzania. Aidha, juhudhi mbalimbali zimekwishaanza ambapo Uongozi wa Polisi Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega wanaendelea na utaratibu wa kupata eneo la kujenga Kituo cha Polisi kitakachokuwa na hadhi ya daraja 'C' ambacho kitakuwa na Askari kuanzia kumi na tano (15), pia eneo la ujenzi wa nyumba za kuishi askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa wananchi wa Sonjo wanapata huduma ya Polisi katika Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nzega.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zedi!

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kushirikiana na Mwekezaji anayejenga hii *Coating Yard pale* Sojo Igusule, Kijiji cha Sojo Igusule tumefaidika kwamba sasa tutapata maji kwa msaada wa huyu mwekezaji na pia tutapata umeme kwa haraka kuliko ulivyokuwa kwenye mpango, lakini pia kituo cha afya cha pale, kitakuwa *upgraded* kuwa kituo cha afya cha kisasa. Sasa swali langu ni kwamba, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufanya mazungumzo na huyu mwekezaji anayejenga hilo *coating yard pale*, kwa sababu atawekeza zaidi ya bilioni 600 na hivyo na yeye pia atahitaji masuala ya usalama? Je, Serikali iko tayari kufanya naye mazungumzo ili na yeye achangie ujenzi wa hicho kituo cha polisi kama ambavyo amechangia kuleta maji, umeme na kupandisha hadhi kituo cha afya?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Eng.* Masauni, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutumia fursa zilizopo ndani ya jimbo lake kwa ajili ya kuweza kueneza huduma mbalimbali za kijami katika jimbo lake. Kuhusiana na wazo ambalo amelitoa, pia ni wazo zuri, lakini nataka nimjishe kwamba, wazo hilo siyo geni, kwa mfano katika Mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao unaendelea kule Rufiji, tumefanikiwa kupata kituo, tupo katika mchakato wa ujenzi

wa kituo cha polisi, ambapo unatokana na mradi huo. Kwa hiyo, tutatumia mawazo yake pamoja na mbinu ambazo tumetumia kule *Stiegler's Gorge* kwa ajili ya kufanya mazungumzo na wawekezaji hao walipo katika jimbo lake wa mradi huo wa bomba la gesi ili tuone uwezekano wa wao kushiriki kusaidia ujenzi huo wa kituo cha polisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, swali linalofuata linalekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, linaulizwa na Mheshimiwa Khamis Yahya Machano, Mhunge wa Chaani. Kwa niaba, Mheshimiwa Jaku!

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Khamis Yahya Machano wa Jimbo la Chaani kwa kuona umuhimu wa swali hili na niombe....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe lijibiwe swali hili kama lilivyojieleza, kama lilivyojieleza na limeandikwa kiswahili, wala si kizungu!

Na. 51

### **Zanzibar Kupata *Scholarship***

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB (K.n.y. MHE. KHAMIS YAHYA MACHANO) aliuliza:-**

Tarehe 19 Agosti, 2019, zaidi ya wanafunzi 100 walisafiri kwenda masomoni China na India na ni ukweli kuwa elimu ya juu ni suala la Muungano:-

(a) Je katika wanafunzi hao ni wangapi wanatoka Zanzibar pamoja na majina yao?

(b) Je, ule utaratibu wa Zanzibar kupewa *Scholarship* bado unatekelezwa?

(c) Je, ni lini Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia atakutana na Waziri wa Elimu Zanzibar ili kuweka utaratibu mzuri wa masuala ya elimu ya juu?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ole-Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Yahya Machano, Mbunge wa Chaani lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi za ufadhili wa masomo kutoka nchi au mashirika rafiki huratibiwa kwa ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano. Mara baada ya kupokea nafasi hizo, Wakurugenzi wenyewe dhamana ya Elimu ya Juu kutoka pande mbili za Muungano hukutana kwa lengo la kubainisha sifa za waombaji. Matangazo kwa waombaji wote hutolewa kuititia tovuti za Wizara husika. Aidha, zipo nafasi za ufadhili wa masomo ambazo huratibiwa na nchi au shirika linalofadhili.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2019/2020 Serikali ya Watu wa China, kuptitia Wizara yangu ilitoa nafasi 61 za ufadhili wa masomo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, iliratibu zoezi la kuwapata waombaji wenyewe sifa. Jumla ya waombaji 82 kati ya 662 walioomba walikidhi vigezo na majina yao kuwasilishwa Ubalozi wa China kwa hatua za uchaguzi. Baada ya mchujo uliofanywa na Ubalozi waombaji 61 walipata ufadhili huo.

Kwa upande wa India, nafasi za ufadhili wa masomo kwa mwaka 2019/2020 zilitangazwa na kuratibiwa na Ubalozi wa India ambapo jumla ya Watanzania 24 wamenufaika. Nafasi za ufadhili wa masomo zinapatikana kwa njia ya

ushindani kwa kuzingatia sifa na vigezo na pasipo kujali mwombaji anatoka upande upi wa Muungano.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vikao vya Mawaziri, upo muongozo rasmi kuhusu vikao vya pamoja baina ya pande mbili za Muungano na vikao hivyo hufanyika kutokana na uhitaji. Vikao hivyo viro katika ngazi ya Kamati ya Pamoja, Kikao cha Mawaziri na Kikao cha Makatibu Wakuu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jaku!

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichouliza Mheshimiwa, Je, Kati ya wanafunzi hao ni wangapi waliotoka Zanzibar pamoja na majina yao. Swali hili limeletwa zaidi ya mwezi mmoja na, kwa maana hiyo wizara hajijawa tayari kutaka kujibu na ninaomba utumile kanuni yako swali hili lije tena. Baada ya hayo, tuendelee hivyo hivyo, kwa kuwa suala hili la Muungano wala siyo hisani wala fadhila, ni la Muungano, kwa mujibu wa Katiba ambayo umeisaini wewe bwana Chenge, ukurasa mwisho 124. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndio inayoshughulikia masuala yote ya elimu ya juu, Wizara ya Elimu ya Zanzibar kukosa fursa hii. Je, ni lini watakaa kuweka utaratibu huu Zanzibar vijana hawa wakapata masomo kuhusu Elimu ya Juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tokea kuanza Serikali ya Awamu ya Tano, kwa kweli karibu mwaka wa nne, vikao hivyo vimefanyika mahali gani na wapi, kama Mheshimiwa Waziri ni mkweli wewe. Tuwe wakweli, hii si fadhila wala hisani, kwa mujibu wa Katiba hii? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jaku kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba nafasi za ufadhilli zinazotolewa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutolewa kwa Watanzania wote bila kujali wanatoka upande gani wa Muungano. Wakati tunatangaza nafasi hizo, kawaida hakuna sifa au hakuna hitaji la wewe kusema kwamba unatokea upande gani wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anaponitaka mimi nije na orodha ya wanafunzi wangapi wamenufaika wanaotoka Zanzibar, ananipia kazi ambayo kawaida hatuifanyi, kwa sababu sisi tunachofanya tunapopata nafasi, tunakaa na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, kupitia sifa zile halafu tunawachagua wanafunzi wa Kitanzania, bila kujali wanatoka wapi. Kwa hiyo, hatuwaambii waandike kama wanatoka Zanzibar au wanatoka Bara. Kwa hiyo, orodha ambayo ananiomba sisi hatuna! Kwa sababu hatuchukui wanafunzi kwa kuzingatia sifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimhakikishie kwamba Wizara yangu inashirikiana vizuri sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na kila wakati tunahakikisha kwamba pande zote za muungano zinapata manufaa sawa bila ubaguzi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima afahamu kwamba nafasi hizi hutolewa na wale wanaoomba wanatakiwa washindane. Kwa hiyo, mara nyingine ukipema tuenze kukaa na kusema tuenze kuchukua watu kulingana na wametoka wapi, tunaweza tukashindwa kwa sababu kule wanakwenda kushindana na wanafunzi wa nchi zingine. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, asijenge ubaguzi kichwani, sisi hatuna ubaguzi, tunakaa na wenzetu na wala hakuna malalamiko yoyote ambayo yameshakuja kwamba kuna Wazanzibar ambao washindwa kupata nafasi hizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaedelea!

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Na. 52

**Fidia kwa Wananchi wa Nkwenda na Murongo - Kyerwa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Uwekezaji vya Nkwenda na Murongo?

(b) Je, ni lini ujenzi wa Vituo hivyo utaanza?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda na Biashara, Eng. Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa ujenzi unaotarajiwa kufanyika ni wa Masoko ya Kimkakati ya Kimataifa ya Nkwenda na Murongo na sio Vituo vya Uwekezaji kama alivyouliza swali lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inamiliki maeneo yanapojengwa masoko ya Kimkakati ya Nkwenda na Murongo kwa asilimia 100. Eneo la kiwanja cha soko la kimkakati la Nkwenda lilikuwa chini ya Serikali ya Kijiji cha Nkwenda na lilitumika kama shamba kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Kijiji (MFUMAKI). Eneo hilo liliendelea kutumika

kama shamba darasa (*Farmers Extension Centre Demonstration Area*) chini ya Wizara ya Kilimo, hivyo halihitaji fidia. Aidha, Eneo linapojengwa soko la kimkakati la Murongo ni mpakani mwa Nchi ya Tanzania na Uganda linalomilikiwa na Serikali, hivyo halihitaji fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masoko ya Kimkakati ya Kimataifa ya Nkwenda na Murongo ni masoko yaliyokuwa yanajengwa kama sehemu ya utekelezaji wa Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program-ASDP*) kuititia Mradi wa Uwekezaji katika sekta ya kilimo ngazi ya Wilaya (*District Agricultural Sector Investment Project- DASIP*). Ujenzi wa masoko hayo mpaka sasa umekamilika kwa asilimia hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Wizara ya Kilimo Inayoratibu Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, imetenga shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa masoko ya kimkakati. Katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa masoko hayo unakamilika na kuanza kutumika, Wizara ya Kilimo imetuma wataalam kutoka Wakala wa Nyumba (*TBA*) kwa ajili ya kufanya tathmini ya gharama za umalizaji wa ujenzi wa masoko hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niseme, taarifa za soko kukamilika kwa asilimia 50 siyo kweli, labda tuambiwe 20 mpaka 30, lakini pia soko hilo limesimama kuendelezwa tangu mwaka 2013. Swali la hivyo lilijitokeza Bungeni mwaka 2016 na taarifa iliyotoka ni kwamba, Nkwenda ilitengewa shilingi milioni 385....

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja, lakini pointi yangu ni kwamba, kumekuwepo na taarifa za kutenga fedha tangu mwaka

2016/2017 ambazo hazijaenda. Sasa swali, hizo bilioni 2.5 kama tumeahidiwa muda mrefu na hazijaenda, zitakwenda kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Kyerwa iko mpakani, inapata faida ya kuwa na Rwanda na Uganda, hakukuwa na juhudzi zozote za kujenga viwanda na kuifanya wilaya kuwa *damping place* ya bidhaa kutoka Uganda. Nini mkakati wa Wizara kujenga viwanda katika wilaya hii ili kuifungua?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili ya nyongeza kwa ufupi tu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, *Engineer Stella Manyanya*.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kama alivyokiri kwamba swali hili lilishawahidi pia kuulizwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Jimbo hilo na msisitizo wetu ni uleule, kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba tunayo dhamira ya dhati, kuhakikisha kwamba, masoko haya ya mpakani yanaimarishwa, ikizingatiwa kwamba hiyo ni sehemu ya kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka kwamba tarehe 6 Septemba, 2019 Marais wetu, kutoka Uganda pamoja na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, walifanya mukutano kupitia Baraza la Biashara wa kuimarisha biashara za mipakani. Kwa hiyo, suala hilo ni la kipaumbele na litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na kujenda viwanda, hiyo ni moja ya fursa ambazo ziliibuliwa katika kongamano hilo la wafanyabiashara na nimhakikishie tu kwamba, kadri muda unavyoenda, hayo yote

yatashughulikiwa kwa nia ya kuongeza tija ya bidhaa zetu na kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Afrika Mashariki na Tanzania wanafaidika kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, tunahamia Wizara ya Madini, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 53

### **Uwepo wa Madini- Kijiji cha Sakale- Muheza**

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA** aliuliza:-

Katika Kijiji cha Sakale, Kitongoji cha Kwempasi, Tarafa ya Amani katika Wilaya ya Muheza wananchi waligundua uwepo wa madini na shughuli za uchimbaji zillanza, lakini baada ya muda Serikali imefunga machimbo yale:-

Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu wa kufungua machimbo hayo ili wachimbaji wadogo hususan vijana wazawa waweze kunufaika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe! Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko!

### **WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (*GST*) ikishirikiana na wadau wa maendeleo ilifanya utafiti na ulibaini uwepo wa madini ya dhahabu katika Vijiji vya Mindu, Amani, Tengeni, Segoma, Mbambara, Sakale, Muheza na Korogwe. Pia Wilaya ya Muheza ina madini ya ujenzi kama vile mchanga na mawe katika Vijiji vya Magila,

Kilapula, Kwakifua, Mhamba, Furaha na Tanganyika na madini ya *garnet*, *ruby* na *sapphire* katika Kijiji cha Misozwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli machimbo yaliyokuwa yakiendelea katika Kijiji cha Sakale yalifungwa tarehe 2 Oktoba, 2018 baada ya timu ya watalaan kubaini uchimbaji huo kutokuzingatia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya mwaka 2017. Aidha, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni zake haziruhusu kufanya uchimbaji katika vyando vya maji ili kuzuia kemikali ya zebaki na uchafu utokanaao na uchenjuaji kuingia kwenye mito ambayo inamwaga maji kwenye Bwawa la Bayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji huo ulikuwa unafanyika katika vilima vya Kwempasi na Nelusanga ambapo uchimbaji unaweza kutiriritisha majitaka na udongo kutoka juu ya vilima na kuingia katika bonde la Mto Kihara ambaoni moja ya chanzo cha Bwawa la Bayani linalotumiwa na wakazi zaidi ya laki 500 katika Wilaya ya Korongwe, Muheza na Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya watalaan ilishauri mwekezaji mzawa au mgeni anaweza kuruhusiwa kuchimba madini hayo kwa kutumia leseni ya uchimbaji mkubwa na kuweza kufanya tathimini ya kimazingira (*EIA*) na kuwashirikisha wadau wote muhimu kabla ya kuanza uchimbaji ili kuzuia uharibifu huo wa mazingira.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yosepher!

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri ameeleza sababu ya kufungwa kwa eneo hili la madini, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, ni utaratibu gani ambao wameuandaa baada ya manyanyaso makubwa kwa wananchi, baada ya unyanyasaji mkubwa kunyang'anywa mali kuumizwa, ambao ultokea kwenye eneo hili la madini. Wao kama Wizara wamechukua hatua gani kwa wananchi wa eneo lile, ambao walipata

manyanyaso makubwa baada ya kugundua madini kwenye eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri atuambie huyo mwekezaji mkubwa au mwekezaji mzawa, wao kama Wizara wameshamtafuta au wameshampata au wameshatangaza au ni lini atapatikana ili aanze uchimbaji ili wananchi wanaozunguka eneo lile waweze kunufaika nalo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Madini.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Yosepher kama ifuatavyo; kwanza hili la manyanyaso kama lipo na lilitanyika na watu walinyang'anywa mali zao ni muhimu tu tukatumia vyombo vyetu tulivyonavyo vya usalama kuititia Jeshi la Polisi malalamiko haya yaweze kuwasilishwa ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili je, tumetafuta muwekezaji naomba tu nimpe taarifa kwamba watanzania wengi sana ambao wameomba kuchimba kwenye maeneo hayo na nieleze tu kwamba Mheshimiwa Adadi tulienda pale SAkale tukafanya mkutano kwa wananchi na kwa watu ambao walionesha nia ya kuwekeza tumewapa taratibu za kufuata kwa sababu kwa kweli kuchimba pale ni kwenye mto ni lazima tuzingatie sheria ili tusije tukaharibu chanzo cha maji, kwa hiyo wako wengi tumewapa taratibu za kufuata ili waweze kuchimba kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani Mbunge wa Tunduru Kaskazini bado linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Madini.

Na.54

## **Kero za Wachimbaji Wadogo-Ngapa Mtoni na Muhuwesi**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa utekelezaji mipango yake pamoja na maelekezo ya Mhe. Rais ya kushughulikia kero za wachimbaji wadogo hususani katika maeneo ya uchimbaji ya Ng'apa Mtoni na Muhuwesi?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Madini Mheshimiwa Doto Biteko.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer Ramo Mataala Makani* (Mbunge wa Tunduru Kaskazini) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 inatambua umuhimu wa wachimbaji wadogo. Wizara kuititia Tume ya Madini inatoa leseni za uchimbaji mdogo ambazo ni maalum kwa watanzania pekee. Aidha, Juhudi hizo ni pamoja na kuwapatia na kuwatengea maeneo mbalimbali ya kuchimba na kuanzisha masoko ya madini katika mji wa Tunduru ambapo Soko la Madini lilitengeneza tarehe 27 Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwasaidia wachimbaji wadogo Mkoa wa Ruvuma na Wilaya ya Tunduru mwaka 2012/2013 Serikali ilitenga eneo la Mbesa lenye ukubwa wa hekta 15,605.30 kwa GN Na. 25 la tarehe 22 Februari, 2013 kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya shaba na jumla ya leseni ndogo 441 zilitolewa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya leseni kubwa za utafiti ambazo ziliikuwa hazifanyiwi kazi kufutwa, Wizara ya madini kuititia Tume ya Madini imetenga eneo la Ng'apa

Mtoni kwa ajili ya shughuli za wachimbaji wadogo wa madini ya vito lenye ukubwa wa hekta 7,548.59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika eneo la mto Muhuwesi uchimbaji unafanyika kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Madini za Mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004. Aidha, kila mmiliki wa leseni ya uchimbaji ndani ya Mto Muhuwesi anatakiwa kupata vibali kutoka mamlaka husika (*NEMC* na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini) kabla ya kuanza kufanya shughuli za uchimbaji madini ndani ya Mto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani*.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali lakini pia niipongeze Serikali kwa hatua mbili hizi ya kwanza ya kutufungulia soko la madini Tunduru Mjini hali ambayo imeweza kuboresha shughuli na biashara ya madini kwa ujumla kiasi cha kuwaongezea kipato wachimbaji wadogo Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru lakini na Serikali kwa ujumla. Pia pongezi kwa kututengea maeneo katika eneo la Mbesa lakini pia kwenye eneo la Ngapa Mtoni. Nina maswali mawili madogo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uboreshaji uliokwishafanya ambaao ni mzuri na umetuletea mafanikio makubwa bado ziko changamoto kwenye maeneo ya afya, usalama na mazingira na changamoto nyingine zinazohusiana na ugawanaji wa maeneo kwenye maeneo makubwa yaliyotengwa na Serikali. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kwenda kwa wananchi hawa kuwasikiliza kwa karibu sana na kuratibu changamoto zao na kuzipatia majawabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili wanawake ni mahodari sana wa kuunda vikundi na kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za ujasiriamali ni mahodari sana kwenye ujasiriamali na kuunda vikundi na kujishughulisha katika mambo ya ushirika.

Je, wakinamama wa Tunduru watasaidiwaje na Serikali kuweza kuboresha shughuli za uchimbaji mdogo na kwa kuitia vikundi na njia mbalimbali za ushirika ili kuweza kujiboreshea vipato wao wenyewe na kuboresha kipato cha Halmashauri ya Tunduru?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Madini Mheshimiwa Doto Biteko.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunazipokea pongozi hizo alizozitoa na nieleze tu kwamba katika pongozi hizo na yeye anastahili pongozi kwa sababu na yeye ni sehemu ya mchakato huo na nieleze tu kwamba sisi kama Wizara ya Madini na mimi binafsi niko tayari kurudi tena Ngapa kule kukutana na wananchi wa Tunduru kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu kuwasaidia wakina mama nieleze kwamba wakinamama kuitia Chama chao cha Wachimbaji Wanawake - *TAHOMA* wamekuwa wakifanya juhudhi mbalimbali za kuweza kutafuta maeneo kwa ajili ya kuchimba na kutafuta usaidizi wa aina mbalimbali, Wizara tunaendelea kushirikiana nao kwa karibu lakini katika eneo la Tunduru wapo wanawake wanaofanya vizuri sana pengine kuliko hata wanaume, kuna mama mmoja pale anaitwa Mwajuma ameajiri wanaume zaidi ya 40 wanachimba kwenye leseni yake, kuna mama mwingine pale anaitwa Debora Mwikani naye ameajiri wakina baba wengi wanafanya kazi pale, nieleze tu kwamba uchimbaji kwa kweli kinachohitaji ni nidhamu ya matumizi na wakinamama wameonesha nidhamu ya matumizi kwa kiwango kikubwa na kwa kweli nitumie nafasi hii kuwapongeza wanawake kwa kushiriki kwenye shughuli za uchimbaji madini na tunaamini kuitia wanawake uchumi wa madini utatutoa nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri tunaendelea swalilinalofuata na la mwisho kwa leo linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Na. 55

## **Kutokamilika Miradi ya Visima vya Maji – Hanang**

**MHE. DKT. MARY M. NAGU** aliuliza:-

Je, ni lini miradi ya visima vya Waranga, Dumbeta, Endamudagya, Gidika, Murumba na Hirbadaw itakamilika na kuanza kusambaza maji kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji Mheshimiwa Aweso.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Michael Nagu Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto ya maji katika vijiji vya Waranga, Dumbeta, Endamudagya, Gidika, Murumba na Hirbadaw, Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilichimba visima vitano (5) vyenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 45 kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha visima hivyo vinatoa huduma ya maji kwa wananchi, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kupitia Programu ya Usambazaji Maji Endelevu Vijini na Usafi wa Mazingira imetenga Kiasi cha Shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya Dumbeta, Waraga na Hirbadaw. Aidha, jumla ya vituo 30 vya kuchotea maji vitajengwa katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika visima vingine vilivyobakia vya Gidika, Endamudagya na Murumba utafanyika katika mwaka ujao wa fedha 2020/2021.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri kwa kazi iliyofanyika na inayotegemewa kufanywa nilikuwa nauliza kwamba katika visima hivyo vimewekwa nguvu ya *solar* ili kusukuma maji lakini bahati mbaya Hanan'g ni eneo ambalo muda wote halina jua. Je, wanafanya nini ili usambazaji huo uwe unawasaidia wananchi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swali la pili ni kwamba wakala wa visima ulijaribu kuchimba visima katika kijiji cha Gidamwai au Basodomi pamoja na kijiji cha Gauloli lakini kwa sababu walileta mashine yenyewe uwezo mdogo wa kuchimba kwenda chini na Hangan'g iko kwenye Bonde la Ufa. Je, ni lini na Wizara iliahidi kwamba ingeleta mashine hizo kuja kuchimba visima hivyo na wananchi walipewa moyo? Naomba njue ni lini visima vya wakala mashine zawakala wa visima zitakuja Gauloli pamoja na Basodomi ili kuwachimbia hao watu ambaa wamepewa moyo? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo mawili kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji.

**NAIBU WA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Mama yangu Dkt. Mary Nagu kwa kweli ni mwana mama supavu na amekuwa mpiganaji hasa katika Jimbo lake la Hanang' na namuomba Mwenyezi Mungu mwanangu siku moja awe kama yeye kutokana na kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa ninachotaka kukisema tumefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha wananchi wanapata maji lakini kama unavyojua utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na uwepo wa nishati lakini eneo lake kule kumekuwa na hali ya baridi kubwa sana. Sasa kama sisi Wizara ya Maji tutafanya mawasiliano ya karibu kabisa na wenzetu wa Wizara ya Nishati katika kuhakikisha maeneo yale hayana umeme yapelekwe umeme haraka ili wananchi wake waweze kunufaika na huduma hii muhimu sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala zima la uchimbaji wa visima hususani kwa wakala wetu wa uchimbaji wa visima *DDCA* maji ni uhai na sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatupo tayari kupoteza uhai wa wana Hanan'g nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya saa saba tukutane ili tufanye mawasiliano ya karibu na wenzetu wa *DDCA* waende kumchimbia visima vyake ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge huo ndio mwisho wa maswali niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wenye majibu mafupi hasa Wizara ya Mambo ya Ndani, Mawasiliano na Wizara ya Madini.

Nina matangazo wageni waliopo Bungeni asubuhi hii wageni waliopo Jukwaa la Spika, tuna wageni 121 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaao ni wakinamama wajasiriamali kutoka Taasisi ya *Voice of Women Entrepreneurs Tanzania* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na kiongozi wao Ndugu Maida Waziri. Naomba msimame popote mlipo hao hapo karibuni sana na huu ndio ushahidi ambaao Mheshimiwa Waziri Doto amemalizia kusemea sasa hivi kwa upande wa madini hawa ndio wakinamama wanajishughulisha na masuala ya biashara hapa nchini, ahsanteni sana karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa wageni watatu wa Mheshimiwa Kangi Lugola Mbunge Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi ambaao ni familia yake kutoka Mwibara Mkoani Mara Ndugu Marieta Lugola, Ndugu Diana Msaki na Ndugu Nancy Msaki, karibuni sana kwetu Mwibara sisi majirani karibu na Bariadi. (*Makofii*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa William Tate Olenasha Mbunge Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaao ni wapiga kura wake kutoka Ngorongoro wakiongozwa na Mheshimiwa Makko Sinandei, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Angelina Mabura Mbunge Naibu Waziri Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi ambaao

ni mjambe kutoka Shirika la *Robetus Swiss* Ndugu Daniel Kalimbia karibu sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Juma Aweso Naibu Mbunge Naibu Waziri wa Maji ambaye ni ndugu yake kutoka Pangani Mkoa wa Tanga Ndugu Omar Janja karibu sana.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Ali Salim Mbunge ambaye ni rafiki yake kutoka Musoma Mkoa wa Mara ndugu Peter Chuwa ahsante sana ndugu Chuma karibu sana. Pia kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Catherine Ruge, Mbunge, ambao ni rafiki zake kutoka Zanzibar Ndugu Fatuma Ahmed, Ndugu Laitat Masoud na Ndugu Ummi Salim, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi Mbunge ambaye ni mdogo wake kutoka Mjini Arusha Ndugu Eline Mayanga, ahsante karibu sana. Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Hassan Masala, Mbunge wa Nachingwea ambao ni Viongozi wa Taasisi ya *Door of Hope* kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Clemence Mombeki na Ndugu Amina Lukanga, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Abdallah Chikota ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mtwara Vijijini kutoka Mkoa wa Mtwara Ndugu Nashiri Pontya karibu sana. Ehee karibu sana Mtwara kluchele mhh!

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rose Tweve Mbunge ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dodoma hapa ambao ni Dkt. Emmy Mbilinyi na Ndugu Angel Mbilinyi karibuni sana. Pia kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Mollel Mbunge ambao ni wanasheria na watetezi wa haki za watu wenye ulemavu SHIVYAWATA kutoka Mkoa wa Dar es Salaam ambao ni Ndugu Novath Rukwago na Ndugu Steven Fulgence hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Hamidu Bobali ambao ni Viongozi wa Taasisi ya *PWB* kutoka India, chance

na Tanzania Ndugu Purva Gupta, Ndugu Maina Sharma na Daudi Chanila karibuni sana kwetu.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge ambao ni Diwani na mtumishi wa Serikali kutoka Mkoa wa Iringa Ndugu Isidory Kiyenge na Alphonce Yohana, karibu sana. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Kakunda kutoka Kampuni ya Ushauri wa Ujasiriamali na Biashara ya *TRUMARK* ya Jijini Dar es Salaam Ndugu Agnes Mgongo, Ndugu Nelson Abichi na Ndugu Venance Angelo karibuni sana. (*Makof*)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo tunao wanafunzi 83 na walimu watatu kutoka shule ya sekondari ya *Mvumi DCT* ya Jijini Dodoma mko wapi wanafunzi karibuni sana na walimu wetu kwa mafunzo haya someni kwa bidii ninyi ndio tunawategemea hapo baadaye. Hayo ndio matangazo.

Lakini nina tangazo la Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* Mheshimiwa William Mganga Ngeleja Mbunge ambalo linasema anaomba niwajulishe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba kesho Jumamosi tarehe 09 Novemba, 2019 kutakuwa na mechi za kirafigi za soka na *netball* kati ya *combine* ya Watumishi wa Umma na Bunge sport club, michezo hii itachezwa katika uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 09.00 alasiri na wote mnakaribishwa hayo ndio matangazo niliyokuwa nayo hapa.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao kwenye orodha yangu huku sikuwa nimepewa karibuni wageni mnaotokea Mbeya wa Mheshimiwa Sophia karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge hayo ndio matangazo. Katibu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Mwongozo!

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Nitaanza Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa huyo aliyesimama karibu na wewe na yeye ni mwongozo au mashauriano, Mheshimiwa Gipson. Mheshimiwa Mwamoto Balozi huyu hapa Mheshimiwa Anatropia umesimama kwa muongozo ehee umesimama kwa shughuli ipi sasa aha! Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Senator Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 ambapo sitaki kuisoma, lakini ni kwa jambo ambalo limetokea humu asubuhi. Wakati Waziri wa TAMISEMI anajibu swali namba 40 linalohusu hasa suala zima la uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na jibu la nyongeza, swali lake liliuliza: "kwa sababu Serikali ilishatoa siku tatu kwa ajili ya kukata rufaa kuanzia tarehe 6 hadi 9," lakini kwa bahati mbaya kabisa kwa chama ambacho nakiheshimu sana na ninakiamini sana, kwa maana ya pamoja na Wabunge wake kimeamua kujitoa katika uchaguzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, navishukuru vyama vingine ambavyo kwa kutumia busara vimeamua kusubiri siku ya rufaa ambayo ni siku ya mwisho ya rufaa ambayo ni siku ya kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata mwongozo wako, kwa mujibu wa kanuni na Sheria na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, endapo chama fulani kikiamua hata kwa kutokuheshimu tu Katiba ya mtu kuchaguliwa au kuchagua kikaamua kujitoa, je, kanuni inasemaje?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi nasimama kwa mujibu wa kanuni hiyo hiyo 68 (7) na mwongozo wangu unatokana na swali hilo hilo namba 40; ila langu litakuwa kwenye mlengo mwingine.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mmeumia eeh!

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu Waheshimiwa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba 40 lilikuwa linahusiana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Jana Mheshimiwa Mwenyekiti wa CHADEMA ambaye tunamheshimu sana alitangaza kwa kujitoa kwa chama chake kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hoja siyo hiyo, kitendo cha kujitoa kinaambatana na vurugu ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakagenda amesema amefukuza mpangaji kwenye nyumba kutokana na hilo hilo. Jana nimeona kwenye TVvijana wa CHADEMA wa Mbozi wameenda kufyeka shamba la Msimamizi wa Uchaguzi na vitendo hivyo vinaendelea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakongwe tuna historia ya chama hicho kugomea chaguzi. Mwaka 2008 Mheshimiwa Marehemu Chacha Wangwe alipotangaza kugombea Uenyekiti CHADEMA ilitokea tafrani na matokeo yake yakatokea ambayo yalitokea; mwaka 2015 Mheshimiwa Zitto Kabwe alipotaka kugombea Uenyekiti wa CHADEMA, ilitokea tafrani wakapelekea kumfukuza kwenye chama; mwaka 2018 walipotakiwa kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti, wamegomea huo uchaguzi na mpaka sasa hivi wana barua nne za onyo za Msajili wa Vyama vya Siasa kwa ajili ya kutaka kugomea uchaguzi wa Mwenyekiti wa chama chao. Kwa hiyo, tuna historia ya chama hiki katika kugomea chaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kuitaka Serikali iseme inachukuwa hatua gani kwa historia ndefu ya chama hiki kugomea chaguzi ambazo zinagharimu pesa nydingi za Watanzania? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu ni katika Kanuni ya 68. Leo wakati Mheshimiwa anajibu swali la miundombinu, kuna mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza hasa ya ajali barabarani. Kumekuwa kukitokea ajali hasa za bodaboda, wanapogongwa wanajikusanya na kuanza kumshambulia yule aliye gonga. Hii imetokea sasa ni zaidi ya mara tatu na sehemu nydingine wenye magari wamejehuriwa na ku haribu mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka mwongozo wa Mwenyekiti ili Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alitolee tamko kwa sababu imekuwa sasa ni kero. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nasimama kwa kanuni 68(7) nikijielekeza katika swali lili lojibwa na Naibu Waziri, swali la 40 Ofisi ya Rais, TAMISEMI na hususan nikijielekeza kwenye uchaguzi unaoendelea au uchafuzi unaokuja kuendelea kwenye Serikali ya Mitaa; na maswali yangu ya msingi yakiwa; taratibu za ufanyaji kazi Maafisa Watendaji wa Kata zinajulikana, majukumu yao ya kufungua ofisi yanajulikana, lakini tangu kulipoanza zoezi la kuchukuwa na kurejesha fomu, watu wakaamua au kujipa likizo au kwenda likizo. Malalamiko hayo hayo yametolewa Bungeni na Wajumbe, lakini pia tumeongea na Mheshimiwa Waziri kumpa hiyo taarifa na akatoka na tamko kwamba wafungue ofisi, kitu ambacho hakikufanyika na wakijua ni kinyume na kanuni na taratibu; na tumesema hapa hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kauli ametoa tena Mheshimiwa Naibu Waziri akielekeza kwamba kuna watu wanafanya fujo. Sasa sisi hatuelewi, kama kuna watu wameghadhibika ambao wengine sio wanachama wa CHADEMA au siyo wapigakura au hata wanachama wa CCM, wanaamua kufanya vitendo vyta kihuni kuonesha kwamba ni wapinzani wanafanya; nataka nipewe mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viongozi wa TAMISEMI ambao waliona matatizo yanaendelea, ambao tuliwapa taarifa ya uvunjifu wa kanuni ambazo zilipitishwa kwenye Bunge lako na hawakuchukuwa hatua mpaka tunafikia leo, tunaamua kujitoa kwenye uchaguzi wakati wao wakiwa kwenye nafasi walishindwa kuchukuwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.  
*(Makofii)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nasimama kwa Kanuni ya 68 (7), mwongozo wangu unakwenda kwenye swali namba 53 ambalo lilijibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni utaratibu wa kawaida, wachimbaji wadogo wanapogundua madini, machimbo hufungwa na wanaondolewa na wanapewa wawekezaji wageni. Sasa naomba mwongozo wako, huu utaratibu Serikali itauacha lini; ili sasa badala ya kuwaondoa wachimbaji wadogo, wawe wanawaelimisha na kuwfanya waendelee na machimbo ya madini wanufaikie wao na familia zao?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio Waheshimiwa walioomba mwongozo kutoka kwangu, lakini sote ambao tumekuwa humu ndani tangu asubuhi, mtakumbuka kwamba swali Na. 40 limeulizwa na Mheshimiwa Josephine Monko. Wengi waliosimama wameingilia kwenye swali hilo. Chaguzi hizi zina kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Ndassa ameuliza, kwa maelezo yake; kama siku ya rufaa, tarehe 9 ni kesho, kwa nini yatokee haya ambayo ameyaelezea ambapo nisingelipenda nirudie; na sheria zinasema nini katika hali hiyo?

Mheshimiwa Mlinga naye ameellezea kitu ambacho ameona kwenye runinga watu wenyewe hasira wanaenda kufyeka mashamba ya watu na wengine, kama Mbunge moja humu ndani kasema kamwonyesha mlango mpangaji wake. Sasa haya yanachukuwa sura gani? Naona hayo katika uvunjifu wa sheria za nchi; na hili la bodaboda la Mheshimiwa Mwamoto, kwamba wananchi wanapoamua kujichukulia sheria mikononi; kama hayo ndiyo kweli kwamba ajali imetokea bila hata kujua mwenye kosa ni mwenye bodaboda au yule waliyegongana naye, wanajikusanya kwa umoja wao wana-bodaboda wanamshambulia wananchi mwingine.

Mheshimiwa Theonest, ni hilo hilo swali Na. 40 kama kiingilio tu, lakini lengo ni yale ambayo wamesemwa na Waheshimiwa Wabunge walitangulia; Mheshimiwa Ndassa na Mheshimiwa Mlinga.

Mheshimiwa Mbarouk, kwa maelezo ya swali la Mheshimiwa Waziri wa Madini kuhusiana na uchimbaji wadogo, kwa nini wanaachwa wanaletwa wachimbaji wakubwa? Yana utaratibu wake, lakini nadhani yanahuusu Serikali zaidi.

Wewe kama hukuridhika na majibu ambayo Serikali imetoea, pamoja na kwamba halikuwa swali lako, lakini bado una fursa ya kuweza kuliuliza ukapata nafasi nzuri zaidi ya kupewa majibu na Serikali naue utatoa ushari kama unaona kwamba kile kinachofanywa na Serikali kwa wananchi wetu ambao ni wachimbaji wadogo kwenye maeneo ambayo wanapewa wachimbaji wakubwa, utaweza kufanya hivyo. Huo ndiyo mwongozo kwa Mheshimiwa Mbarouk.

Sasa kwa yale ya Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Theonest,

nadhani Serikali ipo hapa, naomba tusaidiane, nianze na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mwenye dhamana ya kumsaidia Mheshimiwa Rais anayeongoza Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kwamba llani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 4 ambayo ni Mkataba kati ya Watanzania wote na Serikali ya Awamu ya Tano, inasema bayana kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano imeelekezwa na CCM katika Ibara hiyo kuhakikisha kwamba inatumia nguvu zake zote kuhakikisha mambo manne makubwa yanatekelezwa. Jambo la nne ni kuhakikisha tunaendelea kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao mchakato wake umeanza na kwamba kumekuwa na matukio yanayoripotiwa ya kuwepo changamoto katika uchaguzi, changamoto hizo zinatatuliwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nchi yetu ya Tanzania inaongozwa na katiba na na sheria mbalimbali ambazo zimetungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vyovypote ambavyo vinaashiria, ama hakuna uchaguzi ama kuna uchaguzi; vya kujatarisha amani na usalama wa nchi yetu, kuhatarisha maisha ya wananchi, ama kuhatarisha mali za wananchi, naliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jonh Pombe Magufuli haitatao fursa wala haitanyamaza kutochukua hatua mahsusizi za kudhibiti vitendo vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako tukufu niwaarifu Watanzania wote kwamba Jeshi la Polisi Tanzania tayari tumeshajipanga kuhakikisha kwamba uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuanzia wakati huu wa urejeshaji wa fomu, wakati wa kusubiri rufaa, wakati wa kampeni na wakati wa kupigakura na wakati wa kusubiri matokeo kutangazwa,

kuhakikisha kwamba hakuna Mtanzania yeote kwa mtu mmoja mmoja ama kupitia vikundi ama kupitia Vyama vya Siasa vilivyo hapa nchini, kufanya fujo; iwe ni kudhuru watu wengine ama kuharibu mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ambayo yameanza kujitokeza likiwemo hili la Mbozi na matukio mengine ambayo ninazo taarifa kwamba Chama kimojawapo cha Siasa kimejitoa katika uchaguzi, ni imani yangu kwamba chama hicho kinaweza kikawa na mipango ya kuvuruga amani na usalama wa nchi hii. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa onyo kwamba hakuta kuwa na nafasi ya Chama chochote cha Siasa kupanga na kuratibu na kutekeleza mipango inayovuruga na kuvunja na kuhatarisha amani ya nchi hii. Serikali tumejjipanga kutumia nguvu zote kuhakikisha kwamba hakuna amani na usalama wa nchi hii kuvurungwa na Chama chochote cha Siasa. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape *comfort* Watanzania kwamba kuna viashiria vya kuvunja amani, vingine ambavyo dalili zake zimeanzia humu humu Bungeni kupitia Mbunge ambaye ameanza kufukuza wapangaji. Wasishangae tukaanza kuchukua hatua, kwa sababu Wazungu wanasema *charity beginnings at home*, tukaanza hapa Bungeni kuchukua hatua kwa watu wa aina hiyo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, namwelekeza *Inspector General* wa Polisi...

**WABUNGE FULANI:** Ehe!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Katika mpango kazi ambao tayari wameshaupanga...

**WABUNGE FULANI:** Ehe!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Waanze kuchukua hatua kuanzia Mbozi...

**WABUNGE FULANI:** Eeh!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...ambako matukio haya yameanza na waanze kuchukua hatua kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye nitawapa jina lao ambaye ameanza kufanya viashiria vya kuvunja amani katika nchi hii na maeneo mengine yote.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Wasijaribu kuitikisa Serikali ya Awamu ya Tano, tutachukua hatua. *(Makofu/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawataka watumie kifungu cha 43 cha sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi. Pale ambapo wanahitaji kukusanyika kufanya jambo lolote, wafuate sheria. Pale ambapo watakataliwa, wafuate sheria za kukata rufaa wakisubiri majibu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania wote waendelee kuwa watulivu, Serikali ya Awamu ya Tano ipo pamoja nao na wale ambao watataka kuvunja amani na utulivu wa nchi hii tuko vizuri sana, kiberiti kimejaa njiti,

hakuna mahali kitatikiswa na hakuna mahali ambako tutatetereka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhehimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwa yale mengine, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI waliojibu swali Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kuna hoja hapa zimetolewa, naomba nitoe kauli kwa niaba ya Serikali na nianze na hoja ya kujitoa ya Mheshimiwa Ndassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tuna vyama 22 vyenye usajili wa kudumu na chama ambacho kimejitoa ni kimoja. Kwa hiyo, niendelee kuwapongeza vyama vingine ambavyo vimeendelea kubaki katika mchakato huu kwa sababu nchi ina vyama vingi na kimoja hicho kikiendelea kujitoa siyo mbaya sana.

Mheshimiwa Wenyelekeza, vile vile nijibju tu hoja kwamba, kanuni za uchaguzi zimetolewa mwezi wa Nne pale katika Ofisi ya TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jafo na Vyama vya Siasa vilialikwa, nakumbuka vizuri Mheshimiwa Salim Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu wa Zanzibar wa CHADEMA alikuwepo na hizi nakala walipewa. Vile vile tuliwapa kitabu kingine cha mwongozo wa mafunzo kwa wapigakura na wagombea, nacho walikabidhiwa na kitabu cha tatu ni ratiba ambayo inaonyesha kila tarehe na tukio lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizi ambazo zimetolewa zilielekeza pia kwenye kanuni kwamba kama inatokea vyama wamechukuwa nafasi ya kugombea katika Mtaa, Kijiji au Kitongoji, wakiwa wengi wataendelea kwenye mchakato wao, lakini ikitokea vikachukua vyama viwili vikahalishwa kuteuliwa kugombea, mchakato utaendelea.

Kwa hiyo, maeneo yale ambayo watakuwa wamejitoa, mchakato utaendelea na uongozi utapatikana na hao ni viongozi halali kwa mujibu wa mwongozo, kanuni, taratibu na Katiba Ibara ya 145 na 146(2) itaendelea kutekelezwa kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna hoja ya pili ambayo inazungumzwa kwamba Ofisi zimefungwa. Kama nilivyosema wakati wote kwenye Bunge hili kwamba haya ni maneno ambayo kwa kweli ukienda mtaani hayana uhalisia. Tuna vyama 22, chama kimoja ndiyo kinasema kwamba ofisi zimefungwa, vyama vingine vinasema zoezi linaendelea lakini mchakato huu haujafika mwisho tunaendelea nao. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba hizi ni tuhuma ambazo haziwezi kuthibitika...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Tumetuma watu kwenye mikoa yote ...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Hizo ni taarifa za kupotosha.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo haliwezi kuthibitika, ofisi zetu ziko palepale. Ikumbukwe ofisi za mitaa, vijiji na vitongoji ndiyo ofisi ambazo huduma zote hutolewa...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Kama kutoa barua za aina mbalimbali, miradi ya maendeleo...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Sasa huwezi kufunga ofisi kwa kauli...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Kwa hiyo, jambo hilo sio kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho ambayo imezungumzwa hapa...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Kama hamtaki basi bwana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, kaa chini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mimi niwape moyo Watanzania na nitumie nafasi hii kuwaambia Watanzania kwamba baada ya uchaguzi wale waliojitoa tunawatakia kila la kheri. Kama mtu ameamua kuchukua mpira ameweka kwapani timu iliyobaki uwanjani itapewa pointi kama kawaida na maisha yataendelea na huo ndiyo utaratibu ambao utafanyika. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba baada ya tarehe 24, TAMISEMI tumejipanga, Chuo cha Hombolo kimejipanga, Wenyevit wetu wa Mitaa wa vyama vyote ambao watachaguliwa na kupata fursa hiyo na vitongoji na wajumbe wao watapata mafunzo, watasimamia miradi ya maendeleo chini ya Dkt. John Pombe Magufuli. Kama kuna mtu atagomea maendeleo tunao utaratibu wa kutunga sheria ndogo na bahati nzuri zitakuja hapa TAMISEMI, kazi lazima ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani hiki kibiriti kimejaa sana. Niwaambie Watanzania kwamba hawa viongozi wa vyama hivi na huu utaratibu wao wa kujitoa ni haki yao na wamefanya vizuri kuanza mapema kwa sababu dalili ya mvua ni mawingu, hii ni *trailer*, picha inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

#### **KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu ya ushauri kwa Serikali kuhusiana na Mapendekazo ya Mpango. Nimeshaletewa orodha ya wachangiaji wa leo kwa mujibu wa Kanuni zetu. Nitaanza na hawa wafuatao; Mheshimiwa Munde Tambwe atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia Mpango huu leo Siku ya Ijumaa nikiwa mtu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa pongezi zangu za dhati kwa Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutekeleza mpango kwa asilimia karibia 80. Wamefanya kazi kubwa sana ambayo Watanzania wote wanaiona. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Mpango, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na *management* nzima ya Wizara ya Fedha kwa kuratibu mpango huu na hatimaye kutekelezeka kwa kiwango kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafaniko haya yamedhihirika wazi kwa kazi kubwa inayofanywa na Rais wetu pamoja na viongozi wote. Kwanza kabisa kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kiwango kikubwa lakini pili Serikali hii imedhibiti matumizi mabaya ya fedha ambapo ilikuwa inasababisha fedha za Serikali zinazopatikana kutoonekana lakini leo hii Watanzania wote wanaona fedha yao inakwenda wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuweka nidhamu ya watumishi ya Serikali hatimaye kuzilinda hizi fedha na kuzifikisha mahali husika. Miaka iliyopita fedha hizi zilikuwa zinakusanywa lakini kiwango kikubwa zilikuwa zinaliwa na watu wachache lakini katika Serikali hii ya Awamu ya Tano

hilo limedhibitiwa, maendeleo tunayaona, kazi inaonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kuhusu miradi mikubwa iliyofanywa na Serikali kwa kutumia mpango huu wa Serikali. Serikali hii imeweza kujenga reli, wenzetu walikuwa wanabeza kwamba haiwezekani, leo Dar es Salaam – Morogoro reli imekamilika, inakuja Morogoro – Makutupora na kwenda Tabora – Kigoma – Mwanza – Uvinza – Kaliua – Kalema mpaka Rwanda. Pongezi kubwa kwa Serikali. Hiki kitu kitaacha *legacy*kubwa kwa Serikali ya Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, hakitasahaulika milele na milele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango katika mpango wake ni vyema akaweka bandari kavu pale Tabora kwa sababu Tabora ndiyo njipanda ya safari zote hizi tunazozitaja hapa. Mabehewa yakitoka 20 au 30 Dar es Salaam yakafika Tabora yanakatwa 10 yanayokwenda Mwanza, yanakatwa matano yanayokwenda Kigoma, yanakatwa mangapi yanayokwenda Mpanda lakini pia tuna karakana kubwa ya ukarabati wa reli pamoja na vichwa vya treni. Kwa hiyo, nikuombe sana kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Mpango, pale Tabora kunafaa kabisa kwa bandari kavu kwa sababu ni njipanda ya nchi zetu jirani za Maziwa Makuu za Kongo, Rwanda na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu kwa ununuzi wa ndege, imefanya kazi kubwa sana. Nilikuwa napitia taarifa miaka 30 iliyopita kabla Rais, Dkt. John Pombe Magufuli hajaingia madarakani hatukuweza kununua hata ndege moja leo ndani ya miaka minne tumenunua ndege saba na ndege ya nane inakuja. Hii ni pongezi kubwa na histora kubwa ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuanzisha mradi mkubwa wa umeme ambao una megawati 2,100. Mradi huu ukikamilika naiona Tanzania imekuwa Malaysia, imekuwa

Uturuki, naona maendeleo yatakayokuja kwa kasi kwa kupata umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze elimu bure; watoto wetu kule vijiji sasa wanasona, hata ukitafuta *house girl*/kumpata ni shida. Yote haya ni matunda mazuri ya udhibiti wa pesa za Serikali, ukusanyaji wa pesa za Serikali hatimaye imeweza kuwasomesha bure watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yametapakaa, hata kama kero bado ipo lakini kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano inaonekana. Watu wakumbuke tu historia kwamba ndani ya miaka 50 ilikuwa vipi na ndani ya miaka minne imekuwa vipi. Tumefanya kazi kubwa sana, tunastahili kumuunga mkono Rais, kumpongeza na kumtia moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu, tumeunganisha mikoa, wilaya lakini sasa tunakwenda kwenye vijiji na mitaa. Vilevile viwanja vyta ndege vimepanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati tunachangia jana mpango hapa, Mheshimiwa Silinde, leo hayupo, alisema kuna mambo mengi hayajatekelezwa akasema hasa Bandari ya Bagamoyo hajajengwa na ipo kwenye Mpango. Mimi nimwambie, hatuwezi kutekeleza mradi ambao una masharti ya ajabu ajabu na ya hovyo. Masharti yanayosema tukianza kujenga Bandari ya Bagamoyo, Tanga isijengwe, Dar es Salaam isipanuliwe, Mtwara isijengwe, leo tukubali tu kwa sababu ni kwamba kipo kwenye Mpango; kwani Mpango ni Msaafu au ni Biblia, si kitu ambacho kinaweza kurekebishi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimtoe wasiwasi, miaka mitano bado, hii ni miaka minne. Hii nchi ni ya kwetu wote, Mheshimiwa Silinde ni mzalendo, ni Mtanzania, alete mwekezaji ambaye hana masharti Bandari ya Bagamoyo itajengwa. Hatuwezi kujenga bandari kwa masharti ya aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa sana wote tumeona lakini na mimi niongelee kidogo tu suala zima la Serikali za Mitaa. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kazi tunayoifanya hapa ni kazi kubwa sana, tunajadili Mpango wa Serikali utakaotupeleka kwenye bajeti yetu, itakayowasaidia Watanzania kupata dawa, kusomesha watoto wetu, kujenga vituo vyta afya, kujenga barabara na kadhalika. Leo anainuka Mbunge anaanza kuongelea vyeo tu, yaani hapa ni vyeo tu, watu wanawaza vyeo hawawazi Watanzania. Mimi niwaombe sana tujadili Mpango wa Serikali tuisaidie ili iweze kutuletea bajeti nzuri itakayosaidia wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua sheria na taratibu zipo, sisi hapa ni Wabunge; kama kuna mtu kaonewa, kadhulumiwa aende kwenye vyombo vyta sheria akatoe malalamiko yake na sheria itafuata mkondo wake na sio kuja kwenye Mapendekezo ya Mpango kuanza kuongea habari za vyeo tu. Tukae tukifikiria Watanzania na tusifikirie hivyo vyeo kwa muda wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mapendekezo yangu kidogo kwenye Mpango wa Maendeleo. Niiombe Serikali kama inawezekana kipindi kijacho uchaguzi wa vitongoji, vijiji, Madiwani, Wabunge na Rais hebu ufanyike siku moja. Mimi nadhani itakuwa ni vizuri zaidi kuliko kupanga baada ya miaka minne uchaguzi huu, baada ya miaka mitano uchaguzi huu. Kwanza inaigharimu Serikali kwa sababu tunapitia uchaguzi mara mbili, tunaweka mawakala mara mbili na tunatoa semina mara mbili. Kwa hiyo, mimi naona hakuna haja ya kumaliza pesa za Serikali, ni vyema uchaguzi wote ukafanya siku moja na mambo yakaisha na tutakuwa tume-save pesa ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wenzetu wameitwa na Mheshimiwa Jafo kupewa kanuni za uchaguzi waende wakazitangaze kwa watu wao wakawaeleweshe kanuni hizi zinataka kufanya nini hawakufanya hivyo kwa sababu pesa zao zote za ruzuku zimeshapigwa, hawawezi kusafiri Tanzania nzima kwa wanachama wao kwenda kuwaelimisha kwamba

uchaguzi unataka moja, mbili, tatu. Naibu Katibu Mkuu alikuwepo pale kwa Mheshimiwa Jafo wakati anatoa hizo kanuni, hawakuzifuata kanuni hizo. Sasa kama wameonewa basi niwaombe waende mahakamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee suala zima la tumbaku. Tumbaku ni zao linaloingizia Serikali Pato kubwa la Taifa kwa sababu linauzwa kwa fedha za kigeni. Niiombe sana Serikali iweke mkakati maalum na wa makusudi wa kuhakikisha inalikomboa zao hili la tumbaku. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi, Waziri Mkuu binafsi ameonesha jitihada kubwa sana katika suala hili lakini Wizara ya Kilimo na yenyewe pia imefanya kazi kubwa sana. Hatimaye tumeposta mnunuzi anaitwa *BAT* (*British American Tobacco*). Nimwombe sana Waziri wa Kilimo mnunuzi huyu aje kwa muda husika ili tumbaku ile isikae muda mrefu na kuanza kuharibika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kesi nydingi za *FCC*. Niiombe Serikali kumaliza kesi hizi ili sekta hii ya tumbaku iweze kufikia malengo iliyojiveka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo pamba na sisi Tabora tunalima pamba. Niishukuru Serikali kwa kuweka bei elekezi. Safari hii Serikali isingeweka bei elekezi naamini kuna wakulima wangeuza pamba mpaka 400, 500 na 600 lakini Serikali ikaingilia kati ikaweka bei elekezi pamoja na kwamba bei elekezi pia ina changamoto kidogo. Kwa hiyo, niiombe Wizara husika ianze kukaa na wadau wa pamba mapema kujadili mfumo bora na safi wa kuweza kununua pamba yao. Niombe hiki kikao cha wadau kisiwe mara moja kwa mwaka kiwe mara kwa mara ili kupata mawazo na ushauri mpya ili kuweza kuboresha zao hili la pamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango niiombe Serikali tuna Shirika letu la *TTCL*. Shirika hili kwa kweli haliendi vizuri kutohana na ukosefu wa fedha, shirika hili linadai Serikali madeni mengi, zaidi ya...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tambwe kwa ushauri wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mkuya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Maulid Mtulia ajiandae.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wetu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliendesha gurudumu hili la maendeleo hapa Tanzania. Ameonesha weledi mkubwa hususan katika kuweka usimamizi mzuri kabisa wa rasilimali zetu lakini kurejesha nidhamu ya kazi hususan kwa watumishi wa umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri pamoja na timu yote. Kwa kweli mpango hadi kufikia hapa tunaletewa sisi na tunasomewa na kuona kwamba kila kitu kimepangika basi siyo kazi nyepesi, ni kazi ngumu lakini tumeweza ku-manage na kufika leo kwa mujibu wa ratiba ilivyopangwa. Pongezi zenu sana na katika kipindi hiki kwanza nampa pole sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango kwa baridi lakini naamini ata-manage kuchukua maoni yetu haya, haitamuathiri *of course*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu kwanza naomba nitoe maoni ya ujumla. Mpango wetu ni mzuri umepangika na unaeleweka vizuri lakini kidogo naomba katika yale maeneo ya usimamizi ama maeneo ya tathmini ni lazima sasa tuweke wajibu wa kila mdau katika mpango ule. Ukitosha sasa hivi utaona ni wadau wachache wamewekwa pale lakini naamini kwamba kila mmoja wetu

kwa nafasi yake ana nafasi kwa ajili ya kutekeleza Mpango wetu wa Maendeleo lakini vilevile ana nafasi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wenyewe wa Mpango wa Maendeleo. Kwa hiyo, naomba utakapokuja Mheshimiwa Waziri au hiyo *version* nyingine itakayokuja ambayo ndiyo itaweka *frame* ya bajeti yetu, wadau wanaohusika katika utekelezaji na tathmini waelezwe kwa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge hatukutajwa katika Mpango kama *as if*sisi wajibu wetu tu ni kutoa *recommendations* hapa lakini *actually* sisi tuna wajibu wa kusimamia na kuchukua maelekezo haya na kuwapelekea wananchi tunaowawakilisha. Katika changamoto moja ilioainishwa humu ni kwamba wananchi hawaelewii kwa kina kuhusiana na Mpango huu, sisi kama Wabunge, mbali ya kutoa *recommendations* hapa lakini tuna wajibu wa kuchukua haya maoni na kila kitu na kuwapelekea wananchi ambao ndiyo tunaowawakilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi wenyewe wana wajibu wa kutekeleza Mpango huu. Kwa hiyo, nashauri wadau wanaohusika waelimishwe vizuri kuhusiana na mpango na sisi kama Wabunge tuna kazi hiyo lakini tuna kazi vilevile ya kupitisha bajeti hapa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango. Kwa hiyo, hili ni suala *technical* ambalo nadhani litakwenda kufanyiwa kazi wala halina shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni dogo tu, hizi *projects* zilizoainishwa humu kuna ujenzi wa *campus* ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kwa upande wa Zanzibar. Nadhani ili hili likae vizuri, *campusile* ya Zanzibar sasa hivi inaitwa Kampasi ya Karume. Kwa hiyo, naomba tukiandika tuwe tumeiandika vizuri kwamba sasa hii *campus* ya Zanzibar siyo *campus* ya Zanzibar ni ya Karume naimeekwa hivyo kwa umuhimu wake. Kwa hiyo, lazima tu-*take note on that*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika maeneo *specific*. Pengine katika miaka miwili, mitatu iliyopita wakati

tunachangia Mpango wengi wetu hususan sisi Wabunge ambao tunatoka Zanzibar tuli-*take note* kwamba Mpango haukuainisha kitu chochote ambacho kinahusiana na Zanzibar. Inawezekana majibu yalikuwa ni kwamba Zanzibar wana Mpango wao, *that's good* lakini Mpango huu wa Maendeleo una *areas of support* kwa Zanzibar na nadhani ni muhimu tukazieleza ili sasa katika *improvementya* Mpango iwe imeainishwa vizuri. Kuna maeneo ambayo hakuna namna lazima yaingie kwa sababu ndiyo wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya uwekezaji (*investment*); inawekana kabisa siyo jambo la Muungano, lakini *international cooperation* ambayo ndiyo msingi wa kupatikana *EFDI's*, ni suala la Muungano. Sasa ikiwa tutaangalia ku-*enhance International Cooperation* kwa maana ya mashirikiano ya kimataifa bila ya kuangalia upande mwingine katika *context* ya uwekezaji, hatuwezi kufanikiwa. Huu Mpango wa Taifa una wajibu vilevile wa kuangalia maeneo ambayo yanavuka yanakwenda Zanzibar. Hayo maeneo tunapenda angalau yawe yameainishwa katika Mpango huu, siyo lazima katika utekelezaji wa moja kwa moja, lakini katika mipango yetu ni lazima yaoneshwe kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingine tunaona kuna makongamano ya wawekezaji yanafanyika, lakini tukiuliza pengine labda ushiriki wa Zanzibar uko wapi, utaambiwa hili siyo jambo la Muungano, lakini *international cooperation* pale ni jambo la Muungano na ni jambo ambalo linabebwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo hatuwezi kukwepa kwa namna nyingine yoyote, ni lazima tushirikiane kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusiana na biashara, ni vizuri Mpango wetu huu wa mwaka 2020/2021, unaangalia hasa kuimarisha biashara kimataifa pamoja na biashara kikanda. Biashara (*Inter Trade*) kwa maana ya Tanzania Bara na Zanzibar bado imekabiliwa na changamoto

kubwa sana hususan pale ambapo biashara ama pale ambapo bidhaa zinazozalishwa Zanzibar zikitaka kuja sasa Tanzania Bara angalau ku-access soko, zinakabiliwa na changamoto kubwa. Biashara ya kikanda, biashara ya kimataifa haitaweza kuimarika kama biashara ndani ya nchi, ndani ya pande mbili itakuwa inakabiliwa na changamoto. Hili lipo katika wajibu wa *outline* ya Mpango huu ambao tunauelezea na hili ni lazima liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa nadhani Jaku aliuliza swali kuhusiana na changamoto hizi za biashara lakini majibu mepesi, majibu ya moja kwa moja yanayotelewa ni kwamba haya mambo tunayapeleka katika Kamati ya SMT na SMZ. Unajua vitu vingine viko katika *capacity* yetu, ile Kamati inakutana siyo mara nyngi na kwa wakati mmoja hatuwezi kuainisha changamoto zote zinazoukabili Muungano wetu. Pengine mambo mengine sisi kama watendaji tunafaa sana tusaidie hawa viongozi wetu, siyo lazima twende katika Kamati ile, lakini sisi katika *capacity* yetu tumeteuliwa kwa sababu ya kuwa na *capacity* ya kusimamia maeneo yetu. Tunaweza kabisa kuyachanganua bila ya kupita katika kamati, katika *cooperation* zetu, katika Wizara zetu na taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hii inawezekana si moja kwa moja kwenye Mpango, lakini Mpango una wajibu wa kuhakikisha kwamba hata ule Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar na wenyewe unaendelea na unafikiwa ili kuleta matumaini mazuri ya maendeleo kwa Watanzania wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni utalii, tunashukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *bold vision* hii ya kununua ndege zetu. Ndege pamoja na *benefits* nyngine, ndege hizi zinatumika katika kutangaza utalii, lakini hakuna ndege hata ambayo *at least* ina nembo ya utalii kwa upande wa Zanzibar. Hakuna! Shirika la Ndege la Tanzania ni Shirika la Muungano. Kwa hiyo ni wajibu hata basi tu kuwe na *connotation* labda *Stone Town* au karafuu. Yaani

angalau tuwe tumebeba dhana ya utalii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hilo halipo. Kwa hiyo tunaomba utalii siyo jambo la Muungano lakini *tools* za utalii zinabeba Muungano wetu. Tunaomba basi angalau *consideration* hiyo iwepo na iwe inatekelezwa. *Presence* ya Zanzibar katika Shirika letu tuwe tunajua kwamba *this is ours*, tuwe tuna ile *sense of ownership*. Tunapongeza sana hizi hatua lakini tunajua kwamba *obligation* hii ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya umeme tulipiga sana kelele kuhusiana na VAT. Nashangaa mambo madogo kama haya tunachukua muda mrefu sana kulumbana katika nyumba hii, lakini hatimaye hilo limekuwa tunaishukuru sana Serikali. Gharama za umeme bado na Mheshimiwa Waziri amekuwa akisema mara nyingi kwamba hilo jambo linafanyiwa kazi. Linaendelea kufanyiwa kazi, linaendelea kufanyiwa kazi kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini wananchi wa upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaumia na maisha. Mpango huu wa maendeleo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hautakuwa mpango *successful* kama kwenye sehemu nyingine katika Jamhuri.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Mpango uliopo mbele yetu. Nami nitachangia hasa ule ukurasa wa 11 na 12, idadi ya watu na mwenendo wa umaskini wa Taifa letu na viashiria vya umaskini kwa ujumla wake. Nimetafakari kwa kina baada ya kuusoma Mpango wote na huu wa miaka

mitano nikarejea kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba Mpango huu umejikita zaidi kwenye Dira ya Maendeleo ya 2020-2025, Malengo Wndelevu ya 2020-2030 na Mpango huu wa miaka mitano na huu wa sasa kuanzia 2016/2017-2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alituasa na imekuwa ni msingi wa kimaadili wa Taifa letu kwa baadhi ya wosia mbalimbali za Mwalimu Nyerere. Kati ya maneno ya Mwalimu Nyerere ni kwamba, siyo maneno, falsafa ya Mwalimu Nyerere ni kwamba ili tuendelee (maendeleo) Mpango, unatengeneza Mpango wako ili uendelee vizuri tunahitaji watu, tunahitaji ardhi, siasa safi na uongozi bora. Uongozi ukisoma kwenye malengo endelevu ya dunia ni uongozi shirkishi. Mpango unaanzia chini unaenda juu lakini kwingine maeneo mbalimbali unakuwa *vice versa*, unaweza ukaenda *horizontal*, au unaweza ukatoka juu ukaenda chini lakini hasa kushirikisha watu wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wetu ili ufanikiwe lazima msingi uimarike zaidi, hata nyumba yako ukijenga ili iweze ikasimama imara msingi ni jambo muhimu kuliko jambo lingine lolote. Msingi ulio imara katika kuhakikisha Mpango huu unafanikiwa inaelezea hapa katika mambo matatu inasema suala la usalama, amani, ulinzi na utengamano wa kijamii. Utengamano wa kijamii, jamii inapokuwa pamoja inafikiri pamoja, inashirikiana pamoja kwa sababu maendeleo ni yao. Dunia ya leo mpango au jambo lolote lenye tija limewekewa vigezo vikuu vinne, kigezo cha kwanza ni kukuza utu wa mwanadamu, utu! Kigezo cha pili ni utulivu wa fikra (*piece of mind*); kigezo cha tatu ni rasilimali muda; na kigezo cha rasilimali fedha. Unaweza ukakopa fedha, deni la Taifa limefikia triliioni 52.3 sawa na utazilipa kesho lakini huwezi ukakopa rasilimali muda, muda ukishaondoka umeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2002 tukiwa viongozi wa vyama tulisema ili tushirikiane na Serikali yetu vizuri, Mzee Mangula akiwa Katibu Mkuu wa CCM lazima tuandae Chuo cha Kitaifa cha Kuandaa Viongozi. Viongozi

hawaokotwi kwenye majalala, viongozi huandaliwa. Naona hata *debate* inayoendelea sasa hivi ya namna gani ya umoja wa Kitaifa ukizingatia kwenye wimbo wetu wa Taifa ambao tayari tulishaandaliwa, je tunautumiaje. Kutumia hekima, umoja na amani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye malengo endelevu ya dunia imeelezea kwanza lengo la kwanza namna ya kuondokana na umasikini, la pili linazungumzia kuhusu njaa, la tatu linazungumzia ustawi wa jamii na afya na afya ndiyo rasilimali kubwa, utajiri mkubwa kuliko wote wa binadamu. Ukitabu Joshua Bin Sira, Sura ya 30:16, utajiri mkubwa kuliko wote kwa mwanadamu ni afya yake. Halafu unaenda ya nne inayozungumza nini, elimu bora, sawa, shirikishi kwa wote (*quality*) ili jamii iweze ikajitambua vizuri. Ukienda ya tano unazungumzia akinamama, usawa wa jinsia na unajua kama rasilimali na hasa akinamama ukiwapa uwezo zaidi ile *electromagnetic force* inayotoka kwenye mioyo yao ni tofauti na ya wanaume na hii ni sayansi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi iliyofanyika miaka 300 iliyopita inajaribu kuchambua hisia ambazo zimekuwepo ulimwenguni zaidi ya miaka 5,000 iliyopita kabla ya Kristo kuhusu *electromagnetic force* ya hisia, kunuia na kunena. Hisia, kunuia na kunena (*electromagnetic force*). Hata sauti za akinamama zinavyozungumza tu ni tofauti na za wanaume hasa kwenye ile nguvu ya mioyo yao namna ya kuifanya jamii iweze ikashiriki maendeleo yao pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu huu ni mwaka wa takribani wa 57 wa uhuru, rasilimali viongozi iko wapi? Huwezi ukasema kazi waliofanya labda Baba wa Taifa, akaja Mzee Mwinyi, akaja Mkapa, akaja Mheshimiwa Kikwete, na sasa hivi tunaye Mheshimiwa Magufuli, ni uongozi shirikishi na uongozi endelevu wa pamoja. Rasilimali viongozi ukiangalia hata *debate* inayoendelea, majibu yanayotoka kuhusu umoja wa Kitaifa yanatolewa majibu badala ya kutolewa majawabu yaliyo sahihi kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Najiuliza kwa mfano, mimi Mbunge wa Vunjo, Mbunge wa Vunjo maendeleo nayaangalia pale kijijini kwangu namna

gani ile jamii naishirikisha kwenye *msaragambo*, kwenye mitaro yao, kwenye masuala yao ya elimu, masuala yao ya afya, namna gani wanashiriki kwenye maendeleo yao endelevu ya kila siku ambayo ni jamii inakaa pamoja wanaona fulani ndiyo anayefaa kutuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi Mbunge wa Vunjo niliyepata kura 73% ya wapiga kura wote pale Vunjo, yaani wagombea wote wa Chama cha NCCR Mageuzi ambaao tulishawaingiza wamesajiliwa 1,008 hakuna mwenye sifa hata moja wameondoa wote, wote, kwamba hawafai na ni halmashauri yote ya Wilaya ya Moshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo maendeleo endelevu shirkishi ambayo Mbunge yuko tofauti na Madiwani, Madiwani wako tofauti na Wenyeviti wa Vijiji. Hayo maendeleo tusilichukulie hilli jambo ni jepesi jepesi, soma lengo la 16 la malengo endelevu ya dunia. Linasema ili ku-transform the world lazima kuwe na *justice, piece and strong institutions*, tuwe na haki, amani na mifumo imara na endelevu. Siyo majibu yanayotoka hapa, unachonua ile *electromagnetic force*. Tulichukulia amani ya Taifa letu, amani ya Mama Tanzania na leo ni Ijumaa, Mtume Mohammed (*Swalla Allah Alayh Wasalaam*) anatuhusia, ukiona uovu unatendeka zuia, ukishindwa kuzuia kemea, ukishindwa kukemea onesha basi hata hasira, onesha basi hata chuki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe tu Serikali kwa nia njema na Mpango huu ulivyoeleza, ili uweze ukawa endelevu na nzuri tukubali kuridhiana Taifa hilli ni letu sote. Vyama vyta Siasa ni vikundi tu katika jamii lakini vyama vyta siasa vitasambaratika lakini Tanzania itabaki kuwa hii moja. Mama Tanzania apewe upendeleo na tumrutubishe zaidi aweze kunyonyesha kizazi hiki na vizazi vijavyo, amani yetu ipewe kipaumbele kuliko kitu kingine chochote. Tunazungumzia umasikini huku, watu wanakata mashamba unasikia mahindi yamekatwa, chuki inajengeka na mahali penye chuki panakuwa na woga na mahali penye woga amani inatoweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba chonde chonde, ili haya yote tuweze tukayafanya kazi vizuri na yakawa ni shirkishi kwa wote bila migongano ya aina yoyote, niombe viongozi, siasa safi na uongozi bora, ukimsoma kiongozi, usome Yakobo 3:18 anakuambia "Amani ni tunda la wapenda amani wanadolifia", na hiyo mbegu ni ipi! Mbegu yenye ni ipi, ni haki na uadilifu, haki na uadilifu. Sasa tuone kizazi hiki tunarithisha nini vizazi vijavyo ili Mpango wetu huu wa kuondoa umaskini huu kila Mtanzania ashiriki. *Let say, pale Vunjo kwa mfano, wanamchukia Mbatia, ana sura mbaya, hawamtaki na nini, lakini kumchukua Mbatia kusisababishe wana Vunjo wasishiriki kwenye maendeleo ya Taifa lao la Tanzania.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno yanayosemwa tusiyachukulie wepesi wepesi, *TCD* iliipoanzishwa na Mzee Mkapa ilikuwa ni ya kuleta jamii kwa pamoja. Vyama vilivyo na wawakilishi Bungeni, tukae, tuzungumze, tuishauri Serikali na Katiba yetu. Wabunge tukae tuishauri Serikali, tuisimamie Serikali vizuri.....

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mtulia Maulid, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia Mpango huu. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya. Nitakuwa sijafanya sawa kama sitampongeza sana Jemedari wetu, Mheshimiwa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ufanisi mkubwa katika kipindi kifupi cha miaka minne ya utendaji kama Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tuliona mbali na tuliona ile kasi kwa mbali kabisa tukajua kwa mwendo huu wa Mheshimiwa Rais haya yanayotokea sasa tulyajua kwamba yatakuja kutokea. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa aliyofanya na kwa kututengenezea njia ya kupita katika kujadili Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie maendeleo ya watu, kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu na nataka nijikite wenye eneo la mazingira. Katika mazingira hapa sisi maeneo ya mijini kule tunasumbuliwa sana na mafuriko, mito inakuja kuharibu miundombinu na wakati mwingine Dar es Salaam kuifanya inasimama kabisa. Kwa hiyo, katika hili napenda nijikite mfano mzuri katika Mto Msimbazi na mito mingine mingi ya Dar es Salaam. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri tunapokwenda kutengeneza Mpango huu tutolee macho katika ile mito inayotusumbua na hasa Mto Msimbazi. Najua kuna mipango inaendelea na najua kuna bajeti kubwa ambayo haiendani na uhalisia wa jambo lenyewe, lakini naamini Mheshimiwa Waziri atatupitisha vizuri hapa ili tukija kwenye bajeti tutokee vizuri tusikae hivi hivi, lazima tuje na suluhisho na hasa ninachozingatia ni kwa ajili ya kutengeneza mto na kulipa fidia kwa wananchi waondoke lile eneo tulitumie kisasa na kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mazingira wezeshi, sisi watu wa Dar es Salaam pale tuna mpango wa kutengeneza barabara za kuondoa msongamano na kupunguza foleni. Mpango mzuri sana na kwa kweli tunaipongeza sana Serikali yetu na kwa kweli katika hili tumenufaika nalo sana kwa maana ya barabara, *fly over* Mfugale pale, hapa Ubungo, nyingine itakuja Magomeni, nyingine itakwenda Mwenge, nyingine zitasambaa. Kwa kweli tunapokwenda tunategemea sasa kwenye bajeti hii itakayokuja jambo hili lipewe uzito mkubwa kabisa ili tutakapoondoa msongamano na foleni Dar es Salaam tunakuza uchumi. Watu wakiweza kupita kutembea kurudi

kufanya mambo yao kwa wakati uchumi wetu utaongezeka bila wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nisisitize katika ile mipango yetu ya kipaumbele mitatu, lazima tuweke fedha tuhakikishe tunamaliza kwa wakati. Kujenga Bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere tukisuasua faida haitapatikana, itachelewa kwahiyo tuhakikishe tutakwenda kwa *speed*. Kujenga *standard gauge* tukisuasua reli inachelewa kufika Dodoma hatutapata matunda. Tukiwahi kufanya hivyo maana yake na uchumi wetu utachemka na hata mapato yetu yataongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechungulia ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi katika kifungu cha 160(A), Serikali ilielezea ujenzi wa viwanja vya michezo cha Mwanza na cha Mbeya kwa hiyo, tusiondoke hapa lazima tufanye jambo. Mheshimiwa Rais anawapenda sana wasanii, anawapenda wana michezo. Lakini vilevile ukienda kwenye llani yetu ya Chama cha Mapinduzi, Fungu 162 tunazungumia ujenzi wa *Arena* wa jengo la changamano la michezo na ambalo hili nitafurahi sana tukilijenga Dar es salaam kwa ajili wasanii wako wengi, iddai ya watu wako wengi na jengo kama hili limejengwa Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jengo ambalo unaweza ukafanya ukumbi, ukafanya boxing, ni jengo ambalo ukaondoa ukaja uwanja wa mpira mkacheza, ni jengo ambalo ukaondoa ukafanya *stage* watu wakafanya burudani zao, miziki, vijana wakafanya Tamasha na hivi, ni jengo ambalo la kisasa. Na Mheshimiwa Rais aninavyomjua mie, vijana wake hawa anawapenda kweli kweli na sisi tumsaidie hili jambo lifanikiwe kwasababu ni jambo ambalo linagusa watu wengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la Utawala Bora; nimemsikiliza sana Mwenyekiti hapa, Mzee wangu Mzee Mheshimiwa Mbatia amezungumza mambo mazuri sana lakini mimi ninachosema tu, watuonyeshe mifano hawa wazee, waonyeshe mifano. Chama cha Mapinduzi

ndiyo chama pekee kimeonyesha demokrasia pana tunapofika mambo ya uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vingine hawana hiyo demokrasia. Wakati mwingine mambo haya yanawaharibikia kwasababu viongozi ni wale wale wa tangu tumeanza vyama vingi ni wale wale hawawapishi wengine sasa jamani kama utaratibu ndiyo utakuwa huu basi hata nyie wenyewe tu kujifanyia mabadiliko kwamba toke fulani, aje fulani, atoke fulani, hawa vijana mnawandaaje? Sasa viongozi wa vyama vya upinzani wanazeeka na wengine watakufa na vyama vyao kwasababu hakuna *succession plan* sasa anakuja kwenye Serikali ya Mtaa sehemu ambayo sisi tumeweka utaratibu, tumeweka Sheria, tumeweka miongozo wanafikiri Serikali ya Mtaa itakwenda kama wanavyofanya wao kule, haiwezekani. Huku kwenye Serikali za Mitaa kuna taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, watu wakijitoa mimi naona wameogopa aibu tu kwasababu pale kwangu tulikuwa na mitaa 52 na hawa walijitoa wana mitaa miwili nilikuwa na hamu nao sana. Nilikuwa na hamu nao tuje kuwanyoosha. Wewe mitaa imepunguzwa, kwa mfano, kwangu kuna mitaa 20 tunakwenda kupiga kura sasa si ndiyo vizuri hiyo mitaa 20 ushinde yote ili uonekane mmenifanyia figisu. Mngeniachia mitaa mingi ningeshinda yote, mmeniachia 20 nimeshinda yote 20 hamna, wana mitaa miwili na kuna maeneo mengine mfano kwa Ndugu yangu pale Mheshimiwa Deo Ngalawa kule hawakuchukua hata form wanalamika nini hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti ukienda kwa Kalanga kule wamekimbia, hapa kwa ndugu yangu hapa James Millya hapa wamekimbia sasa wakati mwingine lazima haya mambo tuyaangalie halafu mtu anakuja anasema kujenga amani, amani yetu, amani vipi? Sisi tunaolinda amani ndiyo unatusukumia tunafanya fujo na nyie mnaokata mahindi ya watu mnaonekana nyie ndiyo mnapenda amani, hili haliwezekani kwasababu kama nyie ndiyo mnakata mahindi ya watu, nyie ndiyo mnaokwenda kuvunja nyumba za watu,

nyie ndiyo mnawafukuza watu kwenye upangaji halafu mkigeuka mkija hapa mnajisema nyie ndiyo mnalinda amani na siye tunafanyakazi ya kulinda amani usiku na mchana tunaonekana ndiyo tunaokuja kuleta vurugu hili jambo siyo *fair*. Nilikuwa nataka Mwenyekiti lazima awe *fair* asiwe anakionea tu Chama cha Mapinduzi, lazima tuwe *fair*. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo sijalieawa, tuna shida gani pale Liganga na Mchuchuma? Liganga na Mchuchuma tuna shida gani pale? Pale tunakwenda kutengeneza umeme wa Makaa ya Mawe, pale tunakwenda kutengeneza chuma, hivi ulimwengu wa sasa bila chuma viwanda hivi si vitakuwa viwanda *juice* tu?

Mhesheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani sasa Mheshimiwa Dkt. Mpango aje ahakikishe tunakwenda kukwamuka pale Liganga na Mchuchuma kwasababu kwanza ule umeme unaotumika kwa ajili ya kutengeneza viwanda *juice* chuma tutaungeteneza pale kwenye Makaa ya Mawe. Kwa hiyo, ni jambo ambalo lina faida kubwa sana. Na tukianza kutengeneza chuma hata viwanda vikubwa vikubwa vitakuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani yetu ya Chama cha Mapinduzi imeelezea kufufua Shirika la uvuvi TAFICO. Mheshimiwa Dkt. Mpango nilikuwa naomba sasa tuje kwasababu tukifufua Shirika letu hili la uvuvi *by automatic* hata ile dhana ya kununua meli za uvuvi itapatikana. Tukishanunua meli za uvuvi viwanda *juice* samaki vitapatikana, tunakwama wapi? Kama tumeona kwenye Ndege, cha kwanza tulifufua Shirika la Ndege, tukishafufua Shirika la ndege tumeleta ndege na huku kwenye uvuvi tufufue lile Shirika letu la uvuvi tukishafufua Shirika letu la uvuvi tunakuja sasa na kununua meli za uvuvi hapo mimi nafikiri tutakuwa tumekwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuja jambo lingine, tumeendelea sana kwenye mambo ya afya sasa hivi lakini lazima sasa tuje na uta...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Sanga lakini ngoja nianze na Mheshimiwa Mbilinyi, Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia mpango huu. Lazima tukubalien kwamba hakuna mpango wa maendeleo bila Utawala Bora na Demokrasia na wakati naendelea kuchangia naomba tu ikumbukwe kwamba, nadhani wote tunakumbuka kwamba mwaka jana nilifungwa Gerezani kwa takribani miezi mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako kwamba Mahakama Kuu ilitengua hukumu ile na ilisema kwamba mashitaka yalikuwa batili, mwenendo wa kesi ulikuwa batili na hukumu ilikuwa batili na hivyo kuthibitisha kwamba nilikuwa nimefungwa kisiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kikipongeza sana Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Mwenyekiti wake, Kamati kuu yake pamoja na Viongozi wote kwa uamuvi wa busara waliofikia jana kujitoa kwenye uchaguzi ambaa badala ya kuwa uchaguzi uligeuka kuwa uchafuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbeya tuna Mitaa 181 hawa jamaa wametuengua wote wamebakiza wagombea 11 tu, Mitaa 181 halafu unasema eti wakakate rufaa na wapo wanajaribu kukata rufaa unakwenda unakuta Ofisi zimefungwa. Angalia sasa vipingamizi wanavyowawekea au sababu za kuwaengua; ukijaza na *pen* nyeusi wanasesma

ulitakiwa ujaze na *blue*, ukijaza na *pen* ya *blue* wanasema ulitakiwa ujaze na pen nyeusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kazi, mtu akiandika mkulima wanasema ulitakiwa uandike kilimo, akiandika kilimo wanasema ulitakiwa uandike mkulima sasa *you guys are joke! You are a joke* yaani mnafanya vitu vya ajabu kabisa na nawahakikishia mnachokitafuta mtakipata. Leteni Muswada Bungeni tunawaambia kabisa Serikali kwa sababu Bunge hili sijawahi kuona Mbunge ameleta Muswada halafu *u-proceed*. Serikali leteni Muswada Bungeni, Mheshimiwa Kangi wewe ndiyo kimbelembele wa kuleta utemi sijui uko wapi, walete Muswada mfute vyama vingi tuwe chama kimoja, kwani kuna shida gani? kwasababu ndiyo kitu mnachokitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hili nimeona Wabunge wengi wa CCM waliomakini hawajafurahia, tunaongea nao nje hapo. Yaani unaona kabisa hata *psychologically, facial expressions, body language* unaona na kwa kauli zao unaona kabisa Wabunge wengi waliomakini kwa upande wa Chama cha Mapinduzi hawajafurahia ukiachia wale kama jamaa yangu Mheshimiwa Waitara ambaye anatetea mkate. Hata ningekuwa mimi labda kwa sababu si kapinduka halafu kapewa mkate lazima alinde mkate vinginevyo anakatwa na Makonda kaanza kumuuingilia kule Ukonga kwa hiyo, lazima *dishliyumbe* kidogo, ayumbeyumbe ajaribu kutetea mkate. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unawavezaje watu...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...unawezaje kuacha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Sugu Ndugu yangu na taarifa ya kwanza ni kwamba Sugu ubunge wake ana jasho langu nimemtengeneza mwenyewe...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Weee mavi yako! Pumbavu wee!* [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ....nimefanyakazi kabla hujawa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, unasi kia maneno hayo naamini kwamba utachukua hatua lakini nimpe taarifa kwamba uchaguzi huu una Kanuni na viongozi wa CHADEMA walipewa taarifa mapema, CCM walijipanga, wao hawakujipanga kuandaa watu wao kwa hiyo kutueleza habari ilijojazwa, amejaza mtu mwagine Sugu anazungumza humu ndani shule inamsumbuia pia kwasababu aliyejaza *form* ndiyo anatakiwa a-clarify hicho ambacho anakisema humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpe taarifa kwamba Mheshimiwa Sugu kwamba sisi tunaendelea na mchakato na Kanuni zipo...

**MWENYEKITI:** Taarifa moja tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ...na utaratibu wa nchi hii ni kufuata Kanuni zilizopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Kwa hiyo,

maneno mengine yote yale hayatafuta utaratibu wa Kanuni na Sheria zilizopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa kabla sijakuhoji kuhusiana na taarifa hiyo, Mheshimiwa Sugu nakuheshimu sana, nakuomba ufute kauli ya neno uliyotumia, naomba tu ulifute naamini ulimi umeteleza tu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, unajua humu ndani sisi tuna-*discuss issue serious* za hii nchi...

**MWENYEKITI:** Naelewa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...halafu hawa watu...

**MWENYEKITI:** Hapana.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...wanaleta mambo ya kulinda mkate, nafuta kwa heshima ya Kiti...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...lakini vinginevyo hawa watu wana nanihii sana...

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...wanakera, *we are very serious* humu ndani...

**MWENYEKITI:** Unasemaje kuhusu na taarifa yake?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...mtu anakaa tu Ubunge, Ubunge, hivi Sugu asipokuwa Mbunge wa Mbeya ndiyo hii Nchi itananihii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...itakamilisha mambo yao yote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi unasema kuhusiana na taarifa unaikubali, unaikataa?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Siwezi kupokea taarifa hiyo haina maana kabisa.

**MWENYEKITI:** Haya endelea kuchangia sasa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tусiangalie tulipoanguka...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...tусiangalie tulipo...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hebu kaa tu, kaa tu, Mheshimiwa Waziri hebu kaa tu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini dakika zangu zinatunzwa, natumaini dakika zangu zinatunzwa.

Hebu tuwe wakweli, *Attorney General* yupo hapa, Waziri wa Utawala Bora hayuko lakini Naibu Waziri wa Utawala Bora yuko pale.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Changia tu hoja Mheshimiwa

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Changia tu hoja.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Nalihutubia Bunge linafanya fujo, kwa hiyo kwanza atolewe kwanza aliyefanya fujo yule...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...kama tunavyotolewaga sisi.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel hebu kaa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini usibishane na mimi. Changoa hoja yako Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kama Messi, *everybody* anataka, utafikiri Messi niko uwjanji. (*Kicheko*)

*Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu turudi kuwa serious kidogo kwenye mambo ya nchi tuisiangalie tulipoanguka, tuangalie tulipojikwaa. Yanayotokea haya kwa heshima zote, yanayotokea haya kwenye uchaguzi huu ni matokeo ya kauli ya Rais kwamba Mtendaji atakayemtangaza mpinzani wakati amempa gari, amempa mshahara, amempa sijui nyumba, sijui amempa nini atamfuta kazi, ndiyo matokeo haya. Unajua kauli ya Rais ni agizo. Kwa hiyo, ili twende sawa sawa... [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu hayo maelekezo ya Rais unayotaka kuiaminisha Kamati unaweza ukani patia mimi sasa hivi ukani letea hapa?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Of course*, najua utaratibu siwezi kuyaleta sasa hivi lakini ukinipa muda nitayaleta yapo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo una-*insist* kwamba unayo?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Yapo, naweza kuyaleta.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa mimi nakushi usiende kwenye *territory* hiyo, changia umalize mchango wako.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *I hope* dakika zangu zinatunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kimoja, humu ndani kwa *trend*, utaratibu ulivyo, utamaduni, mazoea wanaorudi humu ni asilimia 30 tu, asilimia 70 tunabaki nje na huko nje halni mbaya kuliko mnavyoweza kufikiria. Kwa hiyo, mnayo nafasi ya kurekebisha wakati mkiwa humu ndani kuinyoosha Serikali. Msipoirekebisha *70 percent/80 percent* mtabaki nje au niseme tutabaki nje tutakuwa hatuna tena pa kusemea kwa sababu ukisema nje unakamatwa unafungwa, angalau humu Bungeni tunayo nafasi ya kusema, hatutaki kusema sasa hivi. Kazi yetu sisi iwe kushauri siyo kusifia bila sababu. Unamsifia mtu kwa kitu ambacho hajafanya mpaka mwenyewe anashangaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amekuja kule Mbeya wanamsifia kwa jengo la radiolojia ambalo nimepambania mimi Mbunge kwa Katibu Mkuu wa Wizara.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...ili Bunge litenge fedha na Bunge likatenga fedha wanakuja wanamshukuru mtu mwингine badala...bajeti zinapitishwa humu ndani ya Bunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...kodi za wananchi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...hizi fedha za nchi hii zinazonunua ndege, zinazofanya nini...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukisoma Katiba yako na kwenye eneo zima la bajeti ambayo tunaanza mapendekezo haya mpaka itakapofikia kilele mwezi Juni, bajeti hiyo anayeanzisha mchakato kupitia mamlaka aliyopita ni Rais. Mipango hii ambayo tunaiongelea yote inawezesha pesa hiyo ije kwenye hicho chumba cha *radiology* ulichokisemea ni pesa ya Watanzania ambayo Rais amefanya kwahiylo anaposifiwa ni yeye, wewe ni *catalyst* tu ya kwenda kuhakikisha pesa inatumika vizuri.

Kwa hiyo, unapokuja kusema kwamba wanampa sifa ambazo siyo zake wewe mwenyewe ulipaswa umpe sifa kama walivyompatia wananchi wengine. Na Rais ni muungwana nilisikia siku ile alivyokupa nafasi ya kuongea kwa wananchi wa Mbeya kama Mbunge wao, heshima kubwa. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kwa kweli yaani sina tatizo na Rais, nina tatizo na hawa wapambe kwa sababu gani, Rais hata mimi nilimuunga mkono...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mwongozo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana muda umekwisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mwongozo ahsante.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia Kanuni ya 68(7) ninaomba tu mwongozo wako ili kuwa na uelewa wa pamoja kwasababu wakati Mheshimiwa Mbilinyi akichangia kiti chako kilibaini kwamba alikokuwa anatupeleka tulikuwa tunaelekeea kuvunja Kanuni ya 64 kwasababu alikuwa anataka kuhalalisha mchango wake kwa kushughulika na mamlaka ambayo Rais anayo lakini akiendelea kuweka matamshi ya Rais na kuyahalalisha katika maana aliyoukuwa anaitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulifanya vizuri kumuuliza kama anao huo ushahidi wa jambo alilolifanya lakini kwa mujibu wa Kanuni tulikuwa tunapenda kwa muktadha wa majadiliano leo, tujue *rulling* yako katika jambo hili imesimama wapi ili tuweze kujua na sisi Serikali tuwe kwenye *position* ya kujua nini ambacho kimeendelea kwenye *rulling* kwa kuzingatia mjadala ulivyoendelea leo.

**MWENYEKITI:** Uamuzi wangu ni kwamba maneno hayo yasiingizwe kwenye kumbukumbu za *proceeding* za Bunge kwenye *portion* hiyo ambayo niliisemea. Tunaendelea, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza nianze sana kwa kuishukuru serikali ya awamu ya Tano

inayoongozwa na Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri inayofanya juu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru Waziri Mpango na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nichukulie tu kwa mfano; kazi ambayo Mpango unafanya nichukulie tu kwenye Jimbo moja tu la Makambako acha nchi nzima ambako kazi inafanyika kubwa; mmeweza kutupa fedha nydingi ambazo hivi sasa wakandarasi wako *s/ite* wanafanya shughuli za kusogeza huduma ya maji kwa Wananchi Ikelu, Ibatu, Nyamande, Mtulingala shughuli hizo zinaendelea vizuri, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mmetupa fedha ambazo tunajenga hospitali pale ya Halmashauri ya Mji wa Makambako. Mmetupa fedha, shilingi billioni 1,500, juzi mmetuongezea tena shilingi milioni 500. Kwa hiyo, hospitali ile inakwenda vizuri. Pia mmetupa fedha tumejenga Kituo cha Afya pale Lyamkena. Kwa hiyo, napongeza sana na kazi mbalimbali ambazo zinaendelea kufanyika katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukienda kwenye suala hili la uchaguzi, kwanini watu wamejitoa, wanasema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa amezungumzia kwamba watu wasijitokeze kwenye ofisi. Siyo kweli. Nizungumzie tu kwenye Jimbo langu; kuna Kata 12. Kata saba hakuna mtu aliyejitokeza hata mmoja. Kwa hiyo, hata kabla hawajasema hili, tulishinda tayari Kata saba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa wameona mwelekeo wa nchi nzima. Hilo ni Jimbo moja. Muelekeo wa nchi nzima, wameshaona tayari ushindi haupo. Kwa hiyo, wakaona ni vizuri watangaze kwamba wanajitoa, hakuna jambo kama hiyo.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ehe, Mheshimiwa Sanga, hebu subiri.

## TAARIFA

**MHE. LUCIA M. MLLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nataka kumpatia taarifa mzungumzaji kwamba kwenye Kata zake 12 hawakujitokeza wagombea. Siyo kweli. Katika Kata zote walijitokeza Wagombea wa Chama cha CHADEMA. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga, unaikubali Taarifa au unaikataa?

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua huyu ni dada yangu sasa...

**MWENYEKITI:** Unaikubali au unaikataa?

**MHE. DEO K. SANGA:** Naikataa, siyo kweli. Siyo kweli! Nitampa tu mfano. Pale Ngamanga ambako palikuwa panaongozwa na CHADEMA hawakujitokeza kwa sababu tumejenga zahanati na wao wamekiri na Mwenyekiti yule ameacha. Kwa hiyo, napongeza sana kwa kazi ambazo zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na ndiyo maana nilisema wakati ule, kwa nini Rais huyu asiwe wa maisha? Narudia tena, sasa ili mipango ikamilike kwa shughuli ambazo zimeanza za reli, ndege na kadhalika, ni vizuri muda utakapofika 2025 aongezewe hata miaka mitano ili miradi iweze kukamilika vizuri.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Eeeh!

**MWENYEKITI:** Haya.

## TAARIFA

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa Taarifa kwamba naunga mkono kwamba Katiba ibadilishwe azidishiwe muda, pia na vyama vyatupi upinzani navyo vifutwe...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu kaa chini. Kaa chini! Mheshimiwa nitakutoa nje sasa hivi, kaa chini. Mheshimiwa Sanga, endelea.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama hivyo vitajifuta vyenyewe kwa sababu hawaelewi wanakwenda mbele au wanarudi nyuma. Vitajifuta vyenyewe. (*Makof/Kitengele/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa sababu sasa tumenunua ndege zaidi ya saba na tunataka angalau sasa viwanja vyote katika mikoa yetu viweze kuruhusu ndege kutua; kiwanja chetu cha Njombe ambacho hivi sasa mlituambia kwamba kiko kwenye mpango wa kutengeneza ili ndege zetu hizi ziweze kutua. Naomba tukamilishe kiwanja kile cha Njombe ili Wana-Njombe nao waweze kusafiri kwa ndege zao ambazo zimenunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo liko kwenye mpango ni juu ya Liganga na Mchuchuma. Liganga na Mchuchuma ikianzishwa na ikakamilika, uchumi wa Mkoa wa Njombe na uchumi wa Taifa utaongezeka kwa asilimia kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo, sisi tunaotoka Kusini tunategemea sana pembejeo aina ya mbolea ya *DAPOna Urea*, ndizo tunazotumia sana katika mazao yetu; na mbolea hizi ziko katika bei ya juu. Pamoja na kwamba kuna bei elekezi, tunaomba tuwe na mpango shawishi kwa wawekezaji waweze kujenga viwanda vyatupi mbolea katika

nchi yetu, angalau vitapunguza bei za mbolea na kuwa chini hasa mbolea ya *DAPO* na *Urea*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia juu ya kukamilishwa kwa maboma, nami naunga mkono. Tuna maboma ambayo yamejengwa na wananchi, Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wabunge, likiwepo Jimbo la Makambako. Tumejenga maboma mengi; tuone namna ya kutenga fedha kukamilisha maboma haya, mengine yameshaezekwa, yanashubiri tu kupigwa ripu na kukamilisha na kadhalika ili maboma haya yaweze kukamilika kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna miradi mikubwa, mmojawapo ukiwa wa maji, ule wa mkopo nafuu wa fedha kutoka Serikali ya India ambaao utakamilisha miji karibu 28. Katika miji hiyo 28 na Njombe, Wanging'ombe, pamoja na Makambako ipo; tunaomba miradi hii, wananchi wanashubiri kwa hamu sana ili kuweza kutatua tatizo la maji katika Mji wetu wa Makambako na mahali pengine ambako miradi hii itapitiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la ujumla ambalo nilitaka niseme, hili nalirudia tena; Mheshimiwa Dkt. Mpango, katika mipango ambayo umekuwa ukiipanga; ya miaka mitano na huu ambaao tunaujadili hapa sasa, endelea, songa mbele. Kazi yako ni nzuri, unakwenda vizuri, Watanzania wanakutegemea. Wanategemea sana kwa mipango hii ambayo tunaijadili hapa. Mungu akubariki na akuongoze na amlinde Rais wetu ili kusudi tuweze kukamilisha miradi hii. Mawaziri wote ambaao wanafanya kazi yako, wanafanya kazi nzuri na ndiyo maana shughuli zinakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Sanga. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Leah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Daniel Mtuka, ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa maoni yangu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuniwezesha katika kuchangia mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutokukubaliana/kukataa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani yaliyoko ukurasa wa sita kwamba Serikali imezifilisi Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzinyang'anya vyanzo vya mapato na kuzifanya omibaomba kwa Serikali kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani kwa sababu mapato ya Halmashauri zaidi ya asilimia 95 yalikuwa yanatumika katika matumizi ya kawaida. Nikiri kwamba pamoja na Serikali kuchukua vyanzo hivyo, Serikali hili imerithi madeni mengi ambayo ni malimbikizo ya mshahara na matumizi mbalimbali ya watumishi kutoka katika Halmashauri hizi. Serikali imerithi madeni ya wazabuni wa Halmashauri ambapo Halmashauri zilikuwa zinakusanya na kutumia fedha kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuchukua baadhi ya vyanzo hivi, kwa sababu mambo mengi mazuri yameweza kufanyika. Mwanzo asilimia hizo nyingi zilikuwa zinatumika kwa wachache, lakini sasa hivi fedha hizi zinatumika kwa wananchi wengi ambao pia ni sehemu ya Halmashauri. Watumishi ni sehemu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba mishahara ilikuwa inalipwa mpaka tarehe 5 ya mwezi unaofuata lakini sasa hivi mishahara inalipwa mapema sana, siyo zaidi ya tarehe 25. Vilevile zaidi ya shilingi bilioni 20 zinapelekwa kwa ajili ya elimu bure, hakuna watoto wanaorudishwa majumbani. Pia mikopo ya elimu inatolewa kwa wakati, inatolewa miezi miwili kabla na ongezeko la wanafunzi wanaolipwa limeongezeka kutoka 100,000 mpaka 128,000. Hatuoni migomo kwa wanafunzi wa vyuoni. Wametulia, wanasoma bila maandamano yoyote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri madeni ya watumishi na ya wazabuni yamelipwa kwa kiasi kikubwa. Fedha za miradi ya maendeleo zimepelekwa kuimarisha miundombinu kwa wananchi wetu. Kwa mara ya kwanza nimeona Mkoa wa Simiyu Vituo vya Afya vinatoa huduma ya upasuaji, mpaka Zahanati na Vituo vya Afya dawa zimejaa. Hayo yote ni sehemu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mapendeleko katika Mpango, kwamba Serikali iweke mpango mahsus sasa wa kuhakikisha madeni ya watumishi yaliyohakikiwa yote yanalipwa; na maboma ya maabara na majengo mengine yakamilishwe ili kuwepo kwa thamani ya fedha ili maabara hizo pia zitumike kwa kadri ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri pia maboma ya madarasa ya sekondari, Serikali inakamilisha, lakini sasa Serikali iweke mpango mahsus wa kuajiri wahandisi wa kutosha wa ujenzi. Kwa sababu wahandisi wengi wameenda TARURA na wahandisi wa majengo katika Halmashauri hawapo. Fedha nydingi za miradi ambazo zimekuwa zikipelekwa zinatumika na mafundi ambao ni *local*/ambapo inasababisha miradi mingine haitekelezwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie upande wa miradi ya maji. Nakiri kwamba Serikali inapeleka sana fedha nydingi kwa ajili ya miradi ya maji kiasi kwamba mimi nashindwa sasa kusema fedha ziongezwe au zisongezwe kwa sababu fedha kwanza zinazopelekwa hazijaleta tija. Miradi mingi imekamilika lakini haitoi maji. Fedha nydingi zinapelekwa, miradi haitoi maji, mingine inatoa maji siku tu ya uzinduzi. Kwa hiyo, Serikali pamoja na kuwa tumezipa mamlaka za maji vijijini tuhakikishe upungufu uliokuwepo sasa unafanyiwa kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizokuwepo ni usanifu mbovu, usimamizi mbovu na utafiti mbovu. Haiwezekani Wilaya ya Muleba yenye vyanzo vya uhakika vya maji, lakini miradi yake inakamilika halafu haitoi maji. Kwa hiyo, hapo nakiri kulikuwa na usanifu mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa pia na upungufu wa wahandisi wa maji. Serikali iweke Mpango madhubutii wa kuhakikisha inaajiri wahandisi wa maji wa kutosha. Vile vile utafiti pia ulikuwa mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya nchi hii yanatofautiana. Kuna maeneo ambayo *water table* iko juu, mengine *water table* iko chini. Kwa mfano, Mkoa wa Simiyu kuna maeneo ambayo *water table* iko chini sana, lakini inapelekewa miradi ya visima virefu. Kuna maeneo mengine hata ukichimba maji hata Lukale maji yale hata kwenye maabara ya maji hayakubaliki kwa sababu ni chumvi. Naiomba Serikali iweke mpango kwa kufanya utafiti mzuri na kupeleka miradi kulingana na maeneo. Kwa mfano, Wilaya ya Meatu kuwepo mpango wa kupeleka mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu, naiomba Serikali iweze kuusaidia Mji wa Mwanuzi ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu. Kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa maji. Bwawa lile limejaa matope kiasi kwamba hata maji yale hayawezi kutibiwa, hayawezi kupampiwa katika matenki, ni matope matupu. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji afike Wilaya ya Meatu akashauriane na wahandisi na wataalam waone namna gani wanavyoweza kuunusuru Mji wa Mwanuzi, kwa sababu hatuna chanzo kingine cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipewa mradi wa visima nane, lakini vimefeli kwa sababu *water table* iko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Leah. Ushauri mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Kishimba (Profesa) na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naungana na Wabunge wenzangu kuchangia Muswada huu wa bajeti yetu ya 2019/2020.

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, Mawaziri, Naibu na Watendaji Wakuu wote wa Serikali kwa kazi kubwa sana wanazofanya na vile vile nawapa pole kwa kazi kubwa na mafanikio yanaelekea kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuiondoa elimu ndani ya maendeleo, lazima twende nayo. Kwa hiyo, nasimama sehemu ya elimu peke yake. Suala hili la ajira tusijaribu kuitupia Serikali lawama, ni vizuri tutafute ufumbuzi ambao unaweza ukatusaidia aidha kuipunguza kwa nusu au kuimaliza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza chini kabisa. Utaratibu huu wa watoto wa shule kwenda asubuhi, kama hatuna nafasi za kazi, ni vizuri tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu wake yuko hapa, aufikirie upya hasa kwa watu ambao ni wakulima, wafugaji na wafanyabiashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wanaamka saa 12.00 kwenda shulen. Wakifika shulen wanaanza kukimbia mchakamchaka. Baada ya mchakamchaka, saa 3.00 wanaingia darasani. Mpaka kuja kuanza masomo ni saa 4.00. Kwa nini watoto wasiende shulen saa 5.00 wakiwa wamefanya kazi nyumbani ambapo tunatarajia kuja kuwarudisha huku wakimaliza *University*? Watakuwa wamefanya kazi nyumbani mpaka saa tano wataenda shulen, watarudi kutoka shulen saa 10.00 au saa 11.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli binadamu wote ni sawa, lakini Watanzania wote sio sawa, hilo ni lazima tukubaliane. Utaratibu huu wa kwenda asubuhi shulen ni utaratibu wa Uingereza na nchi za Ulaya. Nchi za Ulaya bwana na bibi wanafanya kazi na hawana kazi nyingine pale nyumbani. Wanaondoka na watoto wao wanawaacha shule. Mume au mke anapowahi anampitia yule mtoto au watoto anarudi nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Ulaya kuna tishio la barafu. Barafu inaweza ikapiga London siku tatu, huwezi

kurudi nyumbani au kutoka ndani. Kwa hiyo, kumwacha mtoto nyumbani au kumwacha anafanya kazi, hakuna kazi yoyote Ulaya ya kufanya, ni lazima uwapeleke shule. Sisi tunazo kazi za kufanya, kwa nini watoto wetu wasiende shuleni saa 5.00 mpaka saa 6.00 wakiwa wamefanya kazi huku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna watoto wanaosoma shule za kutwa za msingi zaidi ya milioni nne mpaka tano. Wakifanya kazi masaa manne nyumbani wakazalisha kilo moja moja ya mahindi, mtama au mpunga, tutakuwa tumeinua uchumi wetu lakini watoto wetu watakuwa wamepata elimu ya kutosha; ili watakapomaliza *University*, tunapowalazimisha wajitegemee, hawatakuwa na tatizo lolote la kurudi kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni suala hilo hilo la elimu. Wizara ya Elimu, mara kwa mara namsikia Mheshimiwa Waziri anapambana na watoto watoro, lakini kwa utafiti na maoni tunayoyaona hapa, watoro ndiyo watu waliofanikiwa kwenye maisha. Kwa nini sasa Wizara ya Elimu isianze mtaala wa watoro? Iwe na mtaala wa watoro na mtaala wa watu wazuri. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Leo hii tumeshuhudia watu watoro wakifanya maendeleo makubwa sana. Leo tuna wanamichezo na wanamuziki na bahati nzuri na humu Bungeni tuna zaidi ya Wabunge 50 ambaao ni watoro lakini wana mafanikio makubwa sana. Kwa ridhaa yako kama utakubali nitaje hata kumi... (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Wataje.

## TAARIFA

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Silanga.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Kishimba yeye ni sehemu ya mtoro lakini alifanikiwa sana kuchenjua dhahabu pamoja na mwaka 1992 kuanzisha ununuzi wa pamba hapa nchini lakini alikuwa mtoro hakumaliza shule ya msingi. (*Makofi/ Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa jirani unasemaje na taarifa hiyo?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeah, naiunga mkono. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maneno haya yanaweza kuwa kama ya utani lakini mimi nimekwenda darasani nimefika darasa la nne, nimeelewa kitu wanachofundisha huku kina faida maeneo fulani naenda kuanza shughuli zangu kwa nini mimi nakamatwa? Mimi nimeishia darasa la nne nikagundua ndani ya elimu kuna faida ya kitu fulani na kinawenza kupata faida muda huu, nikaenda kuanza *procedure* na kile kitu, kwa nini mzazi na mimi tukamatwe kurudisha shuleni tuendele miaka 20 isiyo na faida? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Child labour.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anayesema hapa ni *child labour*, je, *old labour* inasemaje? Maana utaratibu wote huu tunaohangaika ni wa Ulaya. Ulaya baada ya miaka 18 mtoto anakuwa mali ya Serikali na mzee baada ya miaka 60 unakuwa mali ya Serikali unatunzwa lakini sisi ni wewe na wanao sanasana *university* anachokunyan'ganya ni pesa na mifugo yako anakurudishia mtoto, inatupa wakati mgumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ubaya gani Wizara ya Elimu ikawa na mitaala ya watoro na Walimu wa wale watoro wawe ni wale watu walitoroka shuleni ambao wameonesha mafanikio. Kweli mimi ni darasa la saba lakini Christopher Columbus aliyevumbua America safari yake ilikuwa kwenda

India lakini akapotea kwa utoro akavumbua America. Mbona wote tunaenda kuomba pesa America nani anayewakataa Wamerikani kuwaita ni watoro. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la elimu ni lazima kabisa Wizara ya Elimu ifanye utafiti kwa vitu vingi sana. Leo hii VETA yetu kuna simu zaidi ya milioni 10 Watanzania wanazo lakini *VETA* haina mtaala wa kutengeneza simu. Leo tuna biashara mpya zimepatikana za madalali, hakuna Chuo cha Madalali lakini wako mtaani na wanaendesha shughuli zao wao *VETA* vitu walivyon'gan'gania haviko kwenye soko. Kwa hiyo, naomba sana sana Wizara ya Elimu waendelee kufanya mdahalo na wananchi ili tujaribu kujikwamua kwenye tatizo la ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, leo hii usipopeleka mwanao shule unashtakiwa lakini mtoto akipata kazi wewe hakutumii hela huwezi kumshtaki. Tunaomba Wizara ya Elimu na Wizara ya Ustawi wa Jamii watuletee sheria hapa ili mzazi anaposomesha mtoto wake anapomuomba pesa au anapopiga simu watoto hawapokei wawajibike kisheria. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunahangaika kweli Majimboni, wazee wanakwenda *TASAF* mtoto yuko Dar es Salam ana maisha mazuri, kila siku unasikia ana *birthday*, mzazi aliyetumia ng'ombe nyngi sana kumsomesha mtoto anateseka. Haruhusiwi kwenda Polisi kulalamika na haruhusiwi kwenda Dawati la Jamii haiwezekani. Tunaomba Mheshimiwa Waziri lete huo Muswda, mbona wewe wanapofika *form six* unawakopesha, unawawekea na riba wanapopata kazi unawakata, mimi mzazi nina kosa gani kumdai mwanangu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wazazi tuijandae kutoa radhi? Kwa nini mimi nijiandae kulalamika na kutoa radhi kwa nini Serikali isitusaidie, Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko hapa atusaidie, kwa nini tuwe tunalalamika, nitamlaani mwanangu, kwa nini nitoe radhi? Mwanangu nimemsomesha na nimemtunza kwa nini nijiandae kuja kutoa

radhi badala ya Serikali kunisaidia sheria ndogo ili mtoto asipopokea simu, hakutoa pesa mimi niende Polisi ili apate *Polisi Order* anitumie pesa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zoezi hili Serikali wameanza wao wenyele ruhusu na wazazi ili mtu unaposomesha shule njue na mimi kwamba nina *investkuliko* sasa hivi naambiwa tu kwamba elimu unamwachia urithi wa kwako wewe, sasa urithi gani huo huyo amepata maendeleo yake wewe unabaki unazubaa kijijini, hauna chochote. Maneno haya tunayaongea kama mzaha lakini wazee kule vijijini wana shida nydingi sana...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Kishimba kwa mchango wako. Huyo ndiyo Profesa Kishimba nilimuita. (*Makofi*)

Nilimuita Mheshimiwa Mtuka lakini amesema yeye anajiandaa kwa jioni. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Janeth Masaburi.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Mpango katika hakika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi kwa zawadi ya uhai aliyonijalia na kuweza kuniruhusu kusimama katika Bunge lako Tukufu leo hii. Nichukue fursa hii kuwapongeza au kuipongeza Wizara ya Fedha ikiongozwa na Dkt. Mpango, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, viongozi wote na watendaji walioko katika Wizara hii. Kipekee nipongeze Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa kukusanya ambapo wamewekwa rekodi kubwa katika mwezi wa Septemba. Hongera sana, kazi nzuri imefanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpandwa, Dkt. John

Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa kwa utashi na uthubutu wake kwa kufanya uamuzi wa kimapinduzi bila woga au kuchoka ambapo ameipeleka nchi katika mageuzi ya kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Kazi kubwa amefanya akisaidiwa na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote wamekuwa wakionekana wakifanya kazi kubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kifupi cha miaka minne Mheshimiwa Rais ameushangaza ulimwengu. Mheshimiwa Rais amefanya mageuzi makubwa hapa nchini kwa kuanzisha miradi mikubwa wezeshi kama miundombinu ya reli (*SGR*), ujenzi wa Bwawa la Mheshimiwa Nyerere, ununuzi wa ndege 11 ambapo saba zimeshawasilishi hapa nchini, ufufuaji wa Shirika la Ndege, ujenzi wa meli za abiria na mizigo katika maziwa yetu, tuliamua tumefika hapa na kazi inaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Dar es Salam utakuta ujenzi wa madaraja ya juu, kuna *interchange* Ubungo kazi inaendelea, ujenzi wa barabara nane kazi inaendelea Ubungo - Kibaha, ujenzi wa madaraja yanayopita baharini (*Salender Bridge*), ujenzi wa barabara za lami katika maeneo mengi ya Kigamboni, Mtoni, Ilala pale Kariakoo miaka ya 20 iliyopita barabara zote zilikuwa ni chafu lakini sasa hivi barabara katika maeneo ya Kariakoo ni lami tupu, pongezi sana Serikali hii. Ukienda pale *Mission Quarters* barabara ni za lami na sehemu nyingine nydingi ambapo muda hauwezi kutosha kuelezea mambo mengi ambayo amefanya Rais wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashangaa kila Mkoa hapa Tanzania miradi inaendelea. Ukienda Mwanza utakuta lami zimejengwa katika Mkoa wa Mwanza na Wilaya zake, ukienda Tabora pale Toronto kama inavyojulikana kazi imefanyika, ukienda Katavi barabara za mitaani zote ni lami na taa za barabarani zinawaka. Kazi hii imefanyika Mikoa mingi sana Iringa, Mbeya, Arusha, Moshi kwa kweli mapinduzi makubwa yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njoo Makao Makuu Dodoma ardhi inalia kila kona. Nenda Mkoa wa Mara pale Musoma lami zimejengwa na taa za barabarani zinaendelea kuwekwa pamoja na miradi mingine ambayo inafanyika pale Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ardhi inalia kila kona, nchi yote watu wako *site*. Pongezi sana kwa timu yake ambayo inamsaidia wakiwemo waziri wa Fedha, Mawaziri wote wanafanya kazi kubwa mno na inaonesha kwamba wamemuelewa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa akifanya kazi kwa vitendo na kufuata matakwa halisi ya haki za binadamu kwa kutimiza mambo yafuatayo. Ametoa huduma za maji katika maeneo mengi, kwa mfano, mwaka 2015 alivyoingia madarakani upatikanaji wa maji vijijini ulikuwa asilimia 54 na sasa tunavyoongea ni asilimia 64.8. Kuna miradi 508 nchi nzima ya maji inaendelea, pongezi sana Serikali ya Awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji katika Mkoa wa Dar es Salam imeboreshwa kwa kiwango kikubwa. Hivi sasa Dar es Salam wanapata maji kwa asilimia 85, DAWASA imetumia zaidi ya shilingi bilioni 50 kutekeleza mradi wa maji na hivi sasa maeneo ya Pugu, Chanika, Kigamboni, Mkuranga, Ukonga, Kibamba, Mabwepande kazi ya kusambaza maji inaendelea. Haya yote yameweza kutekelezwa katika kutekeleza yale matakwa halisi ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosa huduma za maji ni uvunjifu wa haki za binadamu maana tumekuwa tukisikia kwamba Tanzania inavunja haki za binadamu lakini tunashangaa pale watu wanapokosa maji, huduma za afya huwa hatusikii kwamba haki za binadamu zinavunjwa. Mheshimiwa Rais wetu ametekeleza mambo mengi ambayo yamedhihirisha kwamba haki za binadamu zinatekelezwa. Kwa hiyo, naomba nipongeze Serikali ya Awamu ya Tano

kwa kutekeleza mambo ya msingi ambayo yanamgusa mwanadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka minne tu Mheshimiwa Rais Magufuli amezidi kutimiza matakwa halisi ya haki ya binadamu. Tukiongelea huduma za afya ameongeza fedha za bajeti toka shilingi bilioni 30 mwaka 2015 mpaka shilingi bilioni 270. Hiyo yote ni kutekeleza matakwa ya haki ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya afya 357 na hospitali za Wilaya 67, hii ni miaka minne tu. Siku za nyuma tulikuwa na hospitali 57 tu tangu kupata uhuru, haya ni mageuzi makubwa sana. Ujenzi wa Hospitali za Mikoa za Rufaa unaendelea Mikoa ya Njombe, Mara, Katavi, Simiyu na Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu amezidi kuwa mkarimu ambapo wamachinga na mama lishe sasa hawapati tabu. Wanafanya biashara kwa uhuru, wamepewa vitambulisho na wanajulikana walipo. Siku za nyuma walikuwa wakibughudhiwa na huu ni utekelezaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ni mlinzi mwaminifu wa rasilimali za Taifa. Yeye ni mtu mkweli kwa manufaa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janeth Masaburi kwa mchango wako. Katibu.

#### **NDG.NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI**

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Kuna tangazo moja muhimu, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanawake Wajumbe wa TWPG kuwa kesho tarehe 9 Novemba, 2019 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa *Nashera Hotel* kuanzia saa tatu asubuhi mnaombwa mhudhurie. Nadhani na sisi tuanzishe chama cha wanaume tutapata semina.

Kwa hiyo, Wabunge ambao tutaanza nao leo mchana, tutaanza na Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Mtuka Daniel Mtuka, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu na wengine tutafuata namna hiyo.

Kuna tangazo lingine, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) Dodoma linawaalika Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria katika Sherehe za Maulid ya kuadhimisha Mazazi ya Mtume Mohamed yatakayofanyika katika Msikiti wa Gaddafi Dodoma tarehe 9 Novemba, 2019. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Dkt. Ali Kakurwa, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, karibuni kesho.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi leo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendelezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa  
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na  
Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2020/2021**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Nilisoma orodha ya Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao; nilimtaja wa kwanza Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae. Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja iliyopo, hoja ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Kwanza niwashukuru sana vingozi wote wa Wizara ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuleta mpango huu wa kujivunia, Mpango ambao unasomeka na kueleweka vizuri, lakini Mpango ambao umebeba matakwa yetu Wabunge kama ambavyo tulipendekeza kwenye pendelezo la awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umegusa maeneo mbalimbali na miradi ya kimkakati. Miradi ya kitaifa ikiwemo ujenzi wa reli ya kati, ujenzi wa mradi wa umeme, mradi wa Mwalimu Julius Nyerere huko Rufiji utakaozalisha umeme wa megawati 2015. Pia ufufuzi wa ndege za Shirika la Ndege, ununuzi wa ndege mpya, mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ambao limepitia kwetu likitokea Uganda na vilevile kuendelea na kutoa elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo pia ujenzi wa barabara na miradi ambayo imekusudiwa kumaliziwa katika mpango huu. Sisi Tabora tunajivunia Mradi wanaomalizia sasa wa Maji

ya Ziwa Victoria, maji yanayochukuliwa kutoka Ziwa Victoria kuja Tabora imekuwa jambo kubwa sana kwetu na ningependa sana kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mpango huu umelenga kuendeleza na kukuza uchumi wa nchi yetu na kuwa kinara katika Afrika Mashariki na kwa kweli katika Afrika kwa kukuza uchumi wa asilimia 7.1, jambo hili sio rahisi na lilikuwa kama njozi tulipolififikiria hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imefanya mengi katika mpango huu uwezo wa kiuchumi na mimi nasema anayemulika nyoka anaanza miguuni mwake, sisi tumeguswa sana katika ukuzaji wa uchumi katika jimbo letu. Jimbo la Tabora Kaskazini limepata moja ya vituo vya afya na pia tumepata hospitali ya wilaya, vilevile hivi karibuni naipongezza Serikali kwa kunipa Chuo cha VETA na hili ni muhimu sana kwetu sisi kwa sababu jimboni kwangu kuna shule za sekondari nyingi na kuna shule za msingi nyingi lakini kuna *high school* moja tu ya Ndono, kwa hiyo vijana hawa watakaosoma VETA watatusaidia sana kukuza uchumi katika maeneo ya vijijini ambako ningependa pia kuipongeza Serikali kuleta mpango wa umeme wa REA. Umeme wa REA, ambao utakuza uchumi katika vijiji vyetu na wale vijana ambao tutawaandaa katika vituo vya VETA wanaweza kusaidia kukuza uchumi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 16 naipongeza Serikali kupanga kipaumbele cha hela za maendeleo na hela zimepangwa katika miradi ambayo itakuza uchumi. Katika ukurasa huu wameelezea vizuri sana jinsi ambavyo hela zitapelekwa kwenye miradi ya kimkakati kama reli, barabara, viwanja vya ndege na hivi karibuni tumemalizia *terminal III*. Naipongeza Serikali kwa sababu katika mradi huo walifikiriwa pia makandarasi wa nchini hapa, naomba ku-*declare interest* kwamba nilikuwa mmoja wa makandarasi waliojenga *terminal III* Kiwanja cha Ndege Dar es Salaam. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii inatoa ajira kwa wananchi Watanzania vilevile inaweka miundombinu

ambayo itadumu pia inakuwa chanzo cha mapato ya Serikali. Kumekuwa na maneno kuhusu ilipotolewa taarifa kwamba kwa kipindi fulani Shirika la Ndege uwekezaji mkubwa ule tulipata bilioni chache, lakini napenda kusema kwamba aliyetao maneno hayo kwamba ndege imeingiza hela kidogo hakuwa na uga mpana wa busara yake kwa sababu ndege inafikiriwa yenyewe, sisi tulipokuwa tunawekeza kwenye ndege ilikuwa na maana ya ndege iwe chanzo cha mapato mengine. Kwa mfano kuleta watalii, kuebeba mizigo vilevile kuonyesha kwamba sisi Tanzania tuna uwezo, wanasema watu *the bigger the castle the stronger the can*, kuonekana kwamba tuna ndege zetu pia thamani yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali katika Mpango huu imeelezea kuendelea kujenga na kumalizia hospitali za wilaya na vituo vya afya. Pia ukurasa wa 74, Mpango huu umeeleza jinsi ya kushirikisha sekta binafsi na hapo ndipo nami na-*declare interest* kwamba mimi pia ni mwajiri na katika Mpango huu Serikali imesema itawahuisha sekta binafsi katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba jambo kubwa linalotusumbua Mheshimiwa Waziri afikirie jinsi ya kurahisisha ufanyaji wa kazi yaani *easy of doing business*. Hii itatusaidia sana sisi waajiri wa Tanzania, tunalo tatizo kubwa la *SDL* kwamba kila mwajiri anamlipia kila mfanyakazi kiwango cha asilimia 4.5 cha mshahara wake kama tozo ya ujuzi na hii inatusumbua sana kwa sababu ni moja ya mambo yanayofanya sisi Tanzania tusiwe na ile fursa ya *easy of doing business* na kila mwaka tunaporomoka, kwa hiyo hatuwezi kushindanishwa katika ajira za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunaomba sisi waajiri kwamba ni bora *SDL* hii, tozo hii ya ujuzi ipunguzwe kutoka asilimia 4.5 ikaribie asilimia 2.0 na hii itatusaidia sisi kupata kazi katika maeneo mengine, lakini ni vigumu kupeleka wafanyakazi wako kutoka hapa kwenda kufanya kazi Uganda au kufanya kazi Kenya kwa sababu *wage bill* yako itakuwa kubwa kuliko wenzetu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumelilalamikia sisi waajiri ni *Worker's Compensation Fund*. Tungependa tozo hii ya malipo ya mfanyakazi kuumia kazini ikadiriwe au ifikiriwe kutoka na uwezo wa shirika au mwajiri kwa mfano kama mwajiri anafanya kazi za hatari na *likely hood* uwezekano wa mfanyakazi kuathirika atozwe tozo kubwa kwa sababu ya kuweka akiba baadaye. Pia kuna kazi za salama kabisa na hazina tatizo na kwa kweli historia ya kazi hizo haijapata kuleta matatizo kwa wafanyakazi wake, kwa nini atozwe sawasawa tozo ya *worker's compensation*. Wakati Mfuko huu umeanzishwa kulikuwa na utafiti unaofanywa ili kuweza kugawa madaraja ya *Worker's Compensation Fund*, tozo ile ya asilimia 1.0 mpaka asilimia 2.0 kutegemea shughuli na utendaji wa mwajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mpango huu umeendelea kufikiria kukuza kuendelea kulipia shule bure, elimu bure ya msingi yaani darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Hili ni jambo muhimu, liliopoanzishwa lilionekana kama haliwezekani, lakini Mpango huu unathibitisha kwamba jambo hili litaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia hayo tu. Ahsante sana, (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige kwa mchango wako. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa mwaka 2020/2021. Kwanza kabisa niipongeze Serikali yangu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa mambo makubwa ambayo kipindi cha miaka minne tu tunaona mambo yamefanyika makubwa sana sina haja ya kuyataja wenzangu wameyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende ukurasa wa 23 wa Mpango kwa maana ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango

wa Maendeleo. Nizungumzie kidogo eneo la kilimo, niwapongeze sana Bodi ya Korosho kwa maana ndani ya Wizara ya Kilimo, wanajitahidi sana sana kusambaza mbegu, madawa pamoja na utaalam wote unaohusika katika uzalishaji wa korosho. Sisi Manyoni ni wachanga lakini wanaendelea kutusaidia sana lakini na maeneo mengine ambayo hasa wanalima korosho. Bado tatizo liko kwenye mazao mengine, nikizungumzia Mkoa wangu wa Singida sisi tunajulikana kwa kilimo cha alizeti kwa hiyo ni mkoa ambaao ni *giant* kwa uzalishaji wa alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri sana Wizara ya Kilimo inapotokea kwamba mkoa ule ambaao ni hasa *chief producer* wa zao fulani wapeleke nguvu basi kwenye mkoa huo, hasa kwenye mbegu, masoko tuna tatizo kubwa sana. Singida tunalia sana suala la mbegu sana tu tunachanganywa sana upande wa mbegu, kuna mbegu sijui zinaitwa *Hyssun* lakini bei ni kubwa sana zinauzwa kilo moja Sh.35,000, nilizungumza hata kipindi kilichopita. Kwa mkulima wa kawaida ambaao tunategemea hawezি kumudu gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye sekta ya elimu kwenye mapitio haya haya. Nijikite zaidi kwenye ukarabati wa shule kongwe za sekondari. Naipongeza sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano imezikumbuka shule hizi zilikuwa zimeathirika sana lakini sasa ukienda kwenye shule nyingi hizi 87 zote zingine tayari ukarabati umeshakamilika, zingine ziko kwenye hatua za mwisho, naipongeza sana Serikali imefanya jambo kubwa sana pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu tu niongezee kidogo hapo, tunazo changamoto ndogo, kuna hawa jamaa wakala wa majengo ya Serikali *TBA* wanapewa tenda hizi za ukarabati za ujenzi, nadhani wajipange kwanza. Tusiwape tenda tena hapa kwa sababu wametuvurugia maeneo mengi sana kwenye ukarabati na kwenye ujenzi, wajipange vizuri, kwa sababu ni shirika la Serikali wanatuaibisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine niliyoiona kwenye maeneo haya, kwa mfano kwenye shule kongwe hizi, naomba sana shule hizi zinavamiwa Serikali ijitahidi kutenga fedha pia kupima maeneo haya, ni fedha ndogo tu. Kwa sababu tunao *surveyors* kwenye mikoa huko na halmashauri tuwatumie hao hao, wapime watoe hati na kuweka pia hata wigo ili lisivamiwe shule hizi. Tulipita siku moja shule ya Sekondari ya Mirambo kule hali ni mbaya sana uvamizi yaani usiku wanapita watu yaani ni vurumuai, hakuna utulivu wa masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Mpango wenyewe ambao unatarajiwa twende ukurasa wa 66,snizungumzie kidogo suala la misitu na nyuki. Profesa mmoja anaitwa Dos Santos Silayo anasema ingeigharimu dunia triliioni 38 dola za Kimarekani kutengeneza oxygen ambayo *Ingewa-supply* na kuwafaa binadamu kwa miezi sita kwa dunia nzima, ni gharama kubwa sana. Triliioni 38 karibu triliioni 40 *USD* dola kutengeneza *oxygen*, suppose kama miti ingekuwa haipo kwamba sasa *oxygen* inatengenezwa ni triliioni karibu 40 kwa miezi sita tu tena kwa binadamu tu sio wanyama wengine, fikiria hiyo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Dokta mmoja anaitwa Anne Marie anasema kuwa mtu mmoja huhitaji miti hai saba hadi nane imtolee *oxygen* kwa mwaka mzima. Nataka kuzungumzia umuhimu wa kutunza misitu yetu siyo *oxygen* tu na vyanzo vya maji. Manyoni kule sisi tuna Mto mmoja anaitwa Kizigo ambao unaungana na miti 18 ambayo inapeleka kwenye lile bwawa la Mwalimu Nyerere kule Rufiji. Sasa mazingira haya yanaanza kuharibiwa, Sheria ya Misitu, Na.14 ya mwaka 2002 na *regulations* zake za mwaka 2005 zinatoa asilimia 52 kwenye zile *categories*, maana kuna *categories* zimetajwa pale kwamba kuna misitu ya watu binafsi, kuna misitu ya vikundi, kuna misitu ya vijiji, kuna misitu ya Serikali Kuu, kuna misitu ya Serikali za Mitaa na kuna *general land*. Sasa misitu ya vijiji inachukua asilimia 52 kwenye sheria hii ina-*provide* na tunawaachia wanavijiji ndio watanze misitu hiyo. Hii ni hatari, wame-*prove failure*, misitu mingi inateketea

kupitia kwenye vijiji, tuiangalie sheria hii upya vinginevyo tutajikuta tuna jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu hawa wanavijiji hawana elimu yoyote, unamkabidhi asilimia 52 ya misitu yote ya nchi nzima, hapana. Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye vipaumbele waliangalie upya hili la misitu, sheria hii tuibadilishe, tujaribu kuangalia makundi mengine, nadhani Serikali Kuu ive na dhamana ya kutunza misitu hii, hawa waombe tu kibali kwa sababu ni watumiaji washirikishwe, lakini waombe kibali ila mwangalizi awe Serikali Kuu na sheria iseme hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inakwenda vizuri naona kampeni kubwa kwenye uchaguzi ni kufanya kazi. Kwa hiyo kampeni kubwa ya Chama cha Mapinduzi imeshafanyika, tunasubiri tu tarehe 24 vijana wachukue nafasi zao, 2020 Mheshimiwa Rais na Serikali yake na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tuchukue nafasi zetu kwa sababu tayari kampeni zimeshafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono Mpango huu ni mzuri sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtuka kwa mchango wako na ushauri, tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Joel Makanya, ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru Mwenyezi Mungu. Kwanza nianze na kumpongeza sana Dkt. Mpango kwa kuleta Mpango mzuri. Nimpongeze pia Dkt. Kijaji, nipongeze Makatibu na watendaji wote wa Wizara hii ambaa wametuletea Mpango wetu na kutuwasilishia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania ambaye kwa kweli ameweza kutekeleza mambo mengi sana ikiwepo miradi ya ujenzi wa reli ya kat, mrazi wa kufufua umeme, kuimarisha ndege, ujenzi wa meli, ujenzi wa jengo la abiria na miradi mingi tu ambayo kwa kweli hii inaonesha ni jinsi gani llani ya Chama cha Mapinduzi inavyotekelze. Sioni ajabu kuona kwamba watu wengine wameweza kuacha kuchukua fomu au wamejitoa katika chaguzi kwa sababu, miradi mingi sana imeonesha jinsi gani ambavyo tumekuwa makini Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kutoa pongezi kwa mpango huu mzuri ambao umewasilishwa. Na hii ni pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato, kudhibiti matumizi mabaya ya fedha, kuweka nidhamu kwa watumishi, kwa kweli haya ni mambo ambayo yamesababisha Serikali yetu kuweza kuendelea kufanya vizuri na kuendeleza miradi mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kuchangia mpango wangu, naomba nijikite katika urahisi wa kufanya biashara, *easy of doing busuness*. Niipongeze Serikali kwa kuanza kuweka usajili katika mitandao, kwa kweli hii ni kazi nzuri na inafanywa kwa urahisi, lakini wako wafanyabisahara wengi wadogowadogo ambao sasa hawawezi kutumia mtandao ambao ni akinamama, vijana; sasa nione tu Serikali inaweka mpango gani kuhakikisha wanawafikia hawa wafanyabiashara wadogowadogo ili na wao wasajili biashara zao. Maana pengine kumekuwa na urasimu mkubwa sana wa kusajili hizi biashara kama hawana mtandao, sasa Serikali imejipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wekeni mpango mzuri kuhakikisha kwamba, tunapata wafanyabiashara wengi ambao wanajasili biashara ili tuweze kupata mapato na tuongeze pato katika huu mpango ambao mmetuletea. Na ikiwezekana kuwepo na *stop centre* ili watu hawa wasiwe wanansumbuliwa pengine wanaenda kwa afisa biashara, anaenda *TRA, BRELA, OSHA*, nini, sasa tuweke sehemu moja

*then baadaye Serikali iweze kutengeneza mkakati wa kuhakikisha wanagawana hayo mapato. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na mpango wetu. Pia naomba ujikite kuona umuhimu wa kutenga pesa ya utafiti kwa sababu, katika miradi mingi sana tumeona yaani tumetembelea kwenye vituo vingi vya utafiti na tuna watafiti wazuri sana katika sekta nyingi hazifanyi vizuri kwa sababu bado hatujaweka mkakati kuhakikisha tunatumia zile tafiti au watafiti wetu, ili sekta zetu zifanye vizuri. Sasa nilikuwa naomba Serikali iangalie umuhimu wa kutenga lile pato ile asilimia moja, ili ziende kenyé utafiti kwa sababu tumeona nchi nyingi zilizoendelea na zinafanya vizuri katika miradi yake wameweka kipaumbele katika tafiti. Sasa nina imani tukiweka tafiti zetu bado tutafanya vizuri sana na tutakusanya mapato mengi katika sekta zote katika Wizara zetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa naomba mpango wetu pia ujikite katika kuwekeza zaidi katika vyuo vyetu hivi vya VETA. Tukiwekeza katika vyuo vya VETA tutapata wataalam wa kuweza kuendesha viwanda vyetu vidogovidogo, tutapata mafundi mchundo na tuweze kuwawezesha vijana kuanzisha viwanda vidogovidogo na akinamama kwa sababu, tukiwa na viwanda vidogovidogo tukichukulia katika nchi kwa mfano India, China, unaona viwanda vidogovidogo ni vingi sana kwa hiyo, tukiwa na viwanda vidogovidogo tutapata uchumi mkubwa. Kwa hiyo, kama tukisaidia hawa vijana wakapata ujuzi na kuanzisha hivi viwanda vidogovidogo basi tutasaidia Serikali yetu kuwa na mpango mzuri wa kupata pesa na kukusanya pesa ili sasa tuelekee kwenye huo uchumi wa viwanda ambao ndio tumejitanao kwamba, sasa hivi tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini vilevile nilikuwa naomba kuna pesa huwa inakatwa *SDL* asilimia nne kutoka kwenye viwanda. Ni kwa nini sasa hii pesa angalo kidogo isipelekwe *SIDO*, ili *SIDO* waweze kuwakopesha vijana wetu waweze kufungua biashara wakipata yale mafunzo; hii nilikuwa natoa tu kama wazo langu kwamba, kwa Serikali ile

*SDL ya asilimia nne kutoka katika viwanda basi ipelekwe pia SIDO iweze kuwasaidia wanaoanzisha viwanda vidogovidogo.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba mpango wetu ujikite katika ujenzi wa barabara za kiuchumi zilizopo katika mikoa yetu. Ikiwezekana zijengwe kwa kiwango cha lami ili ziweze kuitika muda wote kwa sababu nikichukulia mfano tu katika Mkoa wangu wa Iringa unakuta barabara nyingi sana za kiuchumi hazipitiki kwa muda wote. Wakati wa mvua kunakuwa barabara hazipitiki kwa hiyo, unaona kwamba, kwa mfano labda ukienda kule Mufindi malori yanakwama hata wiki nzima, Kilolo malori yanakwama, lakini pia tunao uchumi mwingine kwa mfano tukiimarisha uchumi katika Mbuga yetu ile ya *Ruaha National Park* nafikiri tunaweza tukapata ongezeko kubwa la watalii na tukaongeza pato la Taifa na pato la mkoa pia. Lakini Ikiwepo na kuongeza TARURA pesa kwa sababu TARURA ndio sasa hivi wana kazi kubwa kuhakikisha kwamba, barabara za vijijini zinapitika muda wote na zinajengwa kwa kiwango cha lami. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee katika mpango wetu. Katika miradi ya kimkakati nilikuwa naomba kwamba, miradi hii ya kimkakati ya kuongeza tija na mapato sasa tijikite kuwasaidia wakulima, wafugaji, wavuvi kwasababu, hii miradi ya kimkakati katika kila halmashauri ipo, sasa iangaliwe. Kama kuna halmashauri ambayo ina wakulima wengi basi ile miradi ya kimkakati ijikite katika kuwasaidia wakulima. Kama kuna wavuvi halmashauri basi ijikite kuhakikisha kwamba, wavuvi au wafugaji wanasaidiwa ili kusaidia pato katika halmashauri zetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa tu mfano kwenye sekta ya uvuvi unaona mapato yamepanda kutoka bilioni 21 mpaka bilioni 72 kwa hiyo, hapo kuna ongezeko kama la bilioni 51 na mapato ya samaki nje ya nchi bilioni 379 mpaka bilioni 691 na bado sasa hapa hawajaweza kuwezeshwa vizuri. Niko katika Kamati ya Kilimo, tunatembelea wavuvi wana changamoto nyingi sana, kama tukijikita kuwasaidia

hawa wavuvi wakafanya vizuri sana tutatengeneza mapto mengi ambayo yatasaidia nchi hii na tutaweza kuweza kusaidia mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo niseme kwanza vilevile niipongeze Serikali kwa kuweza kutoa pesa katika halmashauri zetu kwa ajili ya kuwakopesha akinamama, vijana na watu wenyewe ulemavu, lakini niombe hizi pesa wanavyopewa bila kupata elimu bado hatujawasaidia. Kwa sababu, hizi pesa unapowakopesha unakopesha zirudi na wengine wakope, lakini tuna imani wafanye vizuri zaidi wawe na biashara kubwa ambapo katika biashara zao tutasaidia sasa kuleta pato, walipe kodi kwa wingi ili tuweze kusaidia nchi yetu kuongeza pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo ni kuwashukuru sana. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kusaidia Tanzania na amsaidie Mheshimiwa Dkt. Magufuli, ili mwakani wanaosusa wasuse tuendelee kufanya vizuri zaidi, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Joel Makanya na Paschal Haonga jiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu pamoja na watendaji wote katika Wizara hii ya Fedha kwa kuandaa muelekeo huu ambao ndio dira ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaokuja wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyopitia hotuba ya Waziri cha kwanza naomba nianze kugusia changamoto ambazo ameweza kuzielezea, lakini pia niipongeze Serikali kwa kuweza kukusanya mapato haya ya ndani kwa wastani wa asilimia 88.7 ambapo ni muelekeo mzuri sana katika utekelezaji wa bajeti. Ni kweli kabisa moja ya changamoto

ambayo Waziri alieleza ni kuhusiana na tozo katika sekta isiyo rasmi imechangia kiasi kiasi fulani kwenye kushusha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tumeiona pia hata katika halmashauri zetu kwamba, kile kiwango ambacho ni *fixed* wanacholipa ukikilinganisha kwa siku ni kidogo tofauti na hela ambayo imezoleka. Kwa hiyo, nitoe ushauri kwamba, Serikali ijaribu kuangalia namna bora ambayo itaenda kutumika katika kutoza sekta isiyo rasmi kwa sababu wanatofautiana madaraja kutokana na biashara wanazofanya na faida ambazo wanapata. Kwa hiyo, kuweka *rate* moja kwa watu wote hii nafikiri tuibadilishe tuangalie aina ya biashara na tuwe na *rate* tofauti tofauti angalau sasa hii itatusogeza pale ambapo tulikuwepo kuliko tunashuka chini. Niipongeze Serikali kwa kurasimisha bandari bubu, kama ilivyoelezwa na pia kuendelea kudhibiti uvujaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo mwelekeo wa huu mpango umezungumzia masuala ya bajeti ambapo ni mapato na matumizi. Kwenye matumizi *to* matumizi ya maendeleo na ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze na suala la mapato yanayotokana na kodi, tumeona kwamba, Serikali iendelee kudhibiti hasa kwenye ukusanyaji wa kodi upande wa *import tax* ambapo bado kwa mfano juzijuzi tumeona kwamba, wizi wa bomba la mafuta kwenda kwenye ma-*tank* unafanyika. Sasa kama hiyo tu wananchi humu mtaani wanafanya wizi kama huo maana yake ni nini? Hiyo hata maeneo mengine Serikali itakuwa bado inaibiwa kwa hiyo, tuisihi sana Serikali iendelee kudhibiti. Na hicho tutaweza kufikia malengo ya mapato yetu ambayo yanatokana na kodi, lakini vilevile tuendelee kutanua *tax base*, ili tuweze kuongeza wigo huu ambao utasaidia kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi nyingine ambazo zinakusanywa na *TRA* kwa mfano *Property Tax*. Nikiangalia bado hatukusanyi vile inavyopaswa kwa sababu, tukichukua takwimu za nyumba zote ambazo ziko nchi nzima tulinganishe

na mapato ambayo yamekusanya lazima utaona uwiano hauendani. Niiombe *TRA* kwa sababu tuna watendaji wa kata, tuna watendaji wa mitaa, hebu tuwatumie katika kupata takwimu na kusaidia kufuatilia ukusanyaji wa mapato angalau kwa-*commission* ambayo itawa-*motivate* kuweza kukusanya sehemu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja sambamba na hilo kuna kodi la zuvio kwa wapangaji, *Withholding Tax on the Rent*. Kwa mfano inawezekana hata humu Wabunge wapo ambaao wamepangisha watu nyumba, lakini uliza ni nani ambaye amelipa *Withholding Tax*, hakuna. Kwa hiyo, wengi zaidi wanaolipa ni wa Kariakoo na maeneo ya mijini ambako tu *official*/ndio wanalipa *Withholding Tax*, lakini huku mitaani hii haikusanywi vile inavyopaswa. Kwa hiyo, niombe tutumie pia watendaji wetu wa mitaa, wa vijiji, wa kata katika kuchukua takwimu ni nyumba ngapi zinapangishwa, zina wapangaji, ili wakati mtu analipa kodi basi tuweze kukata hiyo kodi ya zuvio na *TRA* iweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapato ambayo hayatokani na kodi. Katika makisio ya mapato haya mwaka wa fedha 2019/2020 makisio yalikuwa ni triliion tatu bilioni 178 milioni 922. Lakini kilichonishangaza makisio kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa mapato yasiyotokana na kodi yanayokusanya na mashirika, taasisi na Wizara makisio yametoka kutoka hii trillioni 3.1 kwenda trillioni 2.7; sasa nitaomba waziri atueleze tunajua sawa hatujafikia malengo kamili, lakini kwa nini makisio haya yameshuka wakati Bunge na Serikali tunaendelea kuhimiza kwenye taasisi na mashirika ya Serikali kuendelea kutoa magawio kwa mujibu wa sheria ambayo *TR* ndizo ambazo anasimamia? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tutaomba uangalie hili na uweze kutupa mrejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine pia katika kuboresha mapato haya tukiangalia kuna tozo mbalimbali za Serikali nyingine hazijabadilika zina miaka zaidi ya 10 nyingine ni zaidi ya miaka 20. Sasa ni wakati muafaka wa Serikali ku-review hizi *rates* sambamba na kutengeneza

takwimu. Kwa mfano tu tozo ya mtu ambaye anaenda kuchukua *Loss Report Police* unalipa shilingi 500, hii 500 ina miaka mingapi ipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuangalia, lakini tunajua sambamba Sera ya Mapato ya Ndani inazungumzia suala la kuhuisha na kupunguza tozo na ada, lakini kuna wakati lazima tuangalie kuna nyingine tunashusha, lakini nyingine tuangalie namna bora ya kuweza kuzipandisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye Sera ya Mapato ya ndani; cha kwanza Mheshimiwa Waziri ameeleza ni kuboresha mazingira ya kufanya biashara, hii ni kusema iende sambamba na uwekezaji. Kwa hiyo, niombe Serikali iendelee kuhimiza watendaji ndani ya Serikali waendelee kufanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu, ili wafanyabiashara waendelee kufanya biashara kama ipasavyo, kuwa na kauli nzuri pamoja na malengo mahususi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo kuna suala la miradi ya kimkakati. Tuliweza kuboresha sheria ya ubia kati ya sekta za umma pamoja na sekta binafsi – *PPP*. Hebu Serikali iajaribu kuangalia kutengeneza mfumo mzuri ili twende kwenye *PPP* baadhi ya miradi na hapo tutaipunguzia mzigoto Serikali kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kenyet nishati ya gesi asilia kuna mikataba ile ya uwekezaji kwenye gesi imeshatengenezwa *modal* ambayo ndio inatumika mtu akitaka kuwekeza kwenye gesi asilia (*PSA – Production Sharing Agreement*). Kwa nini na huku kwenye *PPP* tusitengeneze *modal* ambayo itakuwa ina-guide katika kuingia hiyo mikataba ambapo itasababisha sasa watu kutokuingia mikataba ambayo itakuwa ni mibovu na haitanufaisha Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lile suala ambalo Mheshimiwa Rais anahimiza suala la *win-win situation*

tulitengenezee *modalambayo* itakuwa ni *guidance* ambayo itatuongoza kuingia kwenye *PPP*. Kwa mfano hapa umekusanya asilimia 88 tumekosa asilimia kama 12. Je, hii 12 tungekuwa kwenye *PPP* maana yake ingeenda kusaida katika hiyo miradi ya kimkakati kwa mfano, kuna hii Liganga na Mchuchuma ambayo tunajua kwamba, ni mradi ambao utanyanya viwanda vingi sana hapa Tanzania na ujenzi wa reli kutoka Mtwara mpaka huko Ruvuma. Sasa tupitie na tuwe *engaged* tusiogope, utawala bora umeboreshwa, tumeamka, tumejua kuangalia namna bora ya mikataba mbalimbali ambayo Serikali inaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la kilimo. Kilimo kinachangia asilimia 28 kwenye pato la Taifa, lakini bado tija yake ni ndogo. Tumezalisha tani milioni 16.8 lakini ukiangalia ule wastani kwa hekta uzalishaji bado uko chini sana. Kwanini iko hivyo, hatuna mbegu bora, pembejeo bado ni hafifu, jembe la mkono linaendelea kutumika, tulikuwa na kauli mbiu ya kilimo kwanza, sasa tukiongeza uzalishaji maana yake na Serikali itaongeza mapato kwa sababu, uzalishaji wenyewe tija ni huu wa kuwa kwamba, unakuwa na *yield* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo kuna uvuvi wa bahari kuu. Na wewe umewahi kuwa kwenye kamati ukaandaa ripoti Serikali namna gani itaongeza mapato; tuna Ripoti ile ya *Chenge I* na *Chenge II*, angalau tufikie zaidi ya triliuni 1.7 sasa hebu Serikali ijikite kwenye uvuvi wa bahari kuu. Ni kwamba, hawa samaki tunaachia nchi nyingine ndio wanawavuna, wanauzu, sisi tunakosa mapato; nimeona kwamba, Serikali imefanya upembuzi yakinifu kwenye ujenzi wa bandari ya uvuvi, lakini sasa tuongeze kasi katika utekelezaji wa mradi huu ambayo itakuwa imewaongeza ma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Richard Mbogo kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea, nilikuwa

nimemtaja Mheshimiwa Joel Makanyaaga akifuatiwa na Mheshimiwa Paschal Haonga na Mheshimiwa Abdallah Mtolea ajandae.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo Mwaka 2020/2021. Awali ya yote nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais wetu, mpendwa wetu Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kulifanya Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ye ye pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na timu nzima ya pale Wizarani kwa kazi kubwa wanayoifanya, kazi kubwa waliyoifanya katika kutuandalia mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni muendelezo wa Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ulioanza mwaka 2016/2017 unakuja kuishia katika mpango huu tunaojadili leo 2020/2021. Mpango huu unatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, chama ambacho ndio chama tawala; ilani ya uchaguzi imeeleza inataka kuwafanya nini Watanzania, kubwa inalotaka kuwafanya Watanzania ni kuwavusha Watanzania kutoka kwenye hatua tulionayo sasa na kutupeleka kwenye nchi ya uchumi wa kati, inataka kutuvusha kupitia viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii imepangiliwa vizuri sana na Wizara husika, kwamba, ili tuweze kufika huko, ili viwanda vyetu viweze kusaidia kuivusha nchi hii kutoka hapa kwenda kwenye uchumi wa kati ni lazima mambo fulani yawekwe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu uko vizuri kabisa, umejipanga vizuri kabisa kwamba tunahitaji tuwe na umeme wa kutosha, tuwe na umeme wa bei rahisi ili tuweze kuzalisha bidhaa zenyehi bei ambazo zina ushindani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali tuliyonayo sasa, tunazalisha mazao mengi; tunazalisha pamba na tunasafirisha pamba ghafi, lakini tunaweza tukasafirisha pamba ambayo imekuwa *semi processed* kwa kiasi fulani. Shida kubwa inakuwa wapi? Gharama ya uzalishaji inakuwa juu. Unakuta mtu anaona akinunua pamba ghafi akaenda kui-process mwenyewe, gharama ya ku-process kwake inakuwa ni ndogo. Kwa hiyo, anaona bora anunue pamba ghafi. Tukisema tui-process kidogo kuiongeza thamani, gharama inakwenda juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imeliona hili ikasema hapana, lazima tuwe na mkakati wa kuzalisha umeme wa kutosha na wa bei rahisi. Ndiyo ikaja na mpango mzima wa *Stiegler's Gorge*. Uzalishaji wa umeme wa *megawat* 2,115 ni umeme mwingi sana utakaosaidia kushusha gharama ya umeme na kuhakikisha viwanda vinapata umeme na kufanya kazi ya uzalishaji kuwa rahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaenda sambamba na mpango wa Serikali vilevile kuhakikisha kwamba wananchi wanapata umeme kote nchini. Mpango wa mwaka 2021 nchi nzima, vijiji vyote, vitongoji vyote wananchi wote wawe wamepata umeme ni mpango unaoenda sambamba na ujenzi wa *Stiegler's Gorge* ili umeme uwepo wa kutosha tusije tukajikuta tumesambaza umeme kwa maana ya nguzo na waya kufika kila sehemu lakini tunafika mahali fulani, umeme wa kuwapa wananchi unakuwa haupo. Kwa hiyo, naupongeza sana mpango huu, ni mpango uliokaa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la usafirishaji, kusafirisha malighafi kutoka sehemu moja hadi nyingine, kusafirisha *end products*, yaani mazao tunayozalisha katika viwanda vyetu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine pia ni kitu cha muhimu sana ambacho Serikali yetu imeliona na imelifanyia kazi nzuri sana. Tunaona barabara zetu nyingi sana zimebekwa lami sasa. Nchi yetu sasa hivi imeunganishwa kwa sehemu kubwa sana, jambo ambalo

linafanya usafiri unakuwa rahisi, mtu anatoka hapa asubuhi anajikuta jioni yuko Mwanza. Ni jambo lilikuwa siyo rahisi sana, unafikiria kwenda siku mbili tatu ukiwa barabarani, lakini mtu anatoka hapa kwenda Songea, kwenda Njombe, kwenda Mbamba Bay huko kwa muda mfupi sana. Tunaipongeza sana Serikali kwa jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, katika suala la usafirishaji wa bidhaa, usafirishaji wa mizigo mbalimbali tukaona kwamba reli ya katika ifanyiwe uboreshaji. Tukaja na wazo la *SGR* ambapo sasa tunaipongeza Serikali. Kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kimeshafika asilimia 63, ni jambo la kuipongeza sana. Kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutupora hapa Dodoma, nacho kimefikia asilimia 16. Tunaipongeza sana Serikali kwa hilo. Mipango yote hii inaonyesha jinsi gani Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba inakwenda na ratiba yake iliyojiwekea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la afya. Tukienda kwenye kitabu cha mwongozo wa Mpango ukurasa wa 17 kipengele cha 58, imeongelewa kwa uzuri kabisa na kwa kina, lakini mimi niseme kitu kimoja; afya ndio kila kitu. Tunahitaji wananchi wetu wafanye kazi ili waweze kuzalisha mashambani. Tunahitaji watu wetu wawe na afya bora ili waweze kufanya kazi viwandani. Kwa hiyo, suala la afya ni suala la muhimu sana, naipongeza Serikali. Hadi sasa tunazungumzia Vituo vya Afya zaidi ya 352. Hadi sasa tunazungumzia Hospitali za Wilaya 67 tumekwenda hatua kubwa sana. Naipongeza sana Serikali kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maboma. Wananchi wetu wamejitoa, wamefanya kazi kubwa sana huko vijiji. Wamejenga majengo ambayo wameshindwa kuyamalizia. Wanaweza kutoa nguvu zao wakasaidia kujenga, lakini inafika mahali fulani wanashindwa kumalizia. Naomba sana Serikali, hebu iangalie, hakuna Halmashauri ambayo haipendi kukamilisha haya maboma, lakini Halmashauri hazifanani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, hebu aliangalie hili kwa kina, Halmashauri ambazo hali yake siyo nzuri sana kimapato, zipewe *support* ya kumalizia haya maboma. Tunawavunja nguvu sana wananchi katika kazi ya kujitolea na kujenga maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu liko hivyo hivyo, nalo lina maboma ambayo ningependa kabisa nayo yafaniwe kazi katika mpango huo niliosema hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji haliko mbali na hivyo nilivyosema. Suala la maji kwa ujumla wake limetekelezwa kwa asilimia 82.6. Naipongeza sana Serikali. Pamoja na kwamba bado maeneo mengine, suala la maji safi na salama ni tatizo, lakini Serikali imefanya kazi kubwa sana, naipongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, ukienda kwenye kitabu cha Mwongozo kile ukurasa wa sita jedwali 1.2 linaonyesha uuzaaji wetu nchi za nje ulishuka kwa asilimia 4.2, lakini ununuzi wetu wa bidhaa kutoka nje ulipanda kwa asilimia 8.9. Hii maana yake ni kwamba tumeshindwa kusafirisha bidhaa kwenda nje. Nami mtazamo wangu ni kilimo. Kilimo kisiposimamiwa vizuri kikatuletea bidhaa za kutosha kusafirisha nje, basi hali hii itaendelea kujitokeza mwaka hadi mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, kuna suala zima la mabwawa ya umwagilaji sehemu mbalimbali, hebu Serikali ije na majibu yanayoelewka. Kuna mabwawa ya zamani, tumeshazungumza sana humu Bungeni suala la ukarabati wa mabwawa ya zamani. Serikali imekuja na mipango mingi sana kwamba watayaangalia waone ni namna gani wa kuyaboresha haya masuala. Basi iwe na kauli ya kusema ili huko kwa wananchi tujue nini cha kufanya. Mabwawa hayatengenezwi, maji hayapatikani, umwagilaji umeshuka chini na suala zima la uzalishaji wa kilimo unashuka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwanza kabisa kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pili nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa mkoa wa Dodoma kumkaribisha Mheshimiwa Rais kwa mikono miwili hapa Dodoma. Juzi alikuja kujandikisha pale Chamwino kwamba sasa ye ye ni mkazi wa Chamwino rasmi. Katika...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makanyaga kwa mchango wako mzuri na ushauri.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Mt Olea na Mheshimiwa Vedasto Ngombale, ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja kwanza hii ya kutotekeleza bajeti ya miradi ya maendeleo. Ni kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa haitekelezi ipasavyo bajeti ya miradi ya maendeleo kama ambavyo tunaidhinisha hapa Bungeni. Kama Wabunge tutakuja hapa Bungeni, tutapitisha bajeti, tutapitisha Mpango ya Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka Mmoja au Miaka Mitano, halafu ile bajeti kama haiwezi kutekelezwa, maana yake mwisho wa siku ni kuendelea kumpigia mbuzi gitaa ambapo kwa namna yoyote ile hawezu kucheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mdogo. Kwa mfano, bajeti ya kilimo ya mwaka 2017/2018, fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa au zilizoidhinishwa hapa Bungeni, ni shilingi bilioni 150.253 lakini

zilizotolewa ni shilingi bilioni 16.5 sawa na asilimia 11 tu. Kutekeleza bajeti kwa asilimia 11 hii kwa kweli siyo sahihi na hatuwatendei haki Watanzania kabisa. Kwa hiyo, ukienda mwaka mwengine 2018/2019 tulitenga shilingi bilioni 98.119 lakini fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 41.22 ambapo ni sawa na asilimia 42. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 fedha za maendeleo zilizoidhinishwa hapa Bungeni na Bunge hili Tukufu ni shilingi bilioni 100.527, lakini fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 2.25 sawa na asilimia 2.2. Kwa kweli miaka yote mitatu hii niliyotoa mifano kwenye kilimo hatujawahi kufikisha asilimia 50. Sasa sijui tunafanya nini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama hatuwezi kuweka kilimo kama ndiyo kipaumbele namba moja ambapo tunajua wote kwamba ndiko Watanzania wengi wamejajiri, zaidi ya asilimia 70, tunajua kabisa huko ndiko ambako hata pato la Taifa mchango ni mkubwa, lakini inaonekana kilimo siyo kipaumbele tena katika Taifa hili. Bajeti zenyewe ndiyo hizo tunatenga, lakini pesa za maendeleo hazipelekwi. Kwa kweli jambo hili linasikitisha sana na hatuwatendei haki Watanzania ambao kwa kweli wengi wapo katika eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunafahamu wote kwamba Watumishi wa Umma kwa muda mrefu sasa hawaajaongezwa mishahara. Serikali ya Awamu ya Tano hajjawahi kupandisha mshahara kwa Watumishi wa Umma. Mheshimiwa Dkt. Mpango anafahamu unapozungumzia Mpango wa Maendeleo wa Taifa, watekelezaji wa Mpango huu ni Watumishi wa Umma. Kwa mfano, unapozungumza leo watu wanaofanya kazi *TARURA*, au wanaofanya kazi *TANROADs* au wanaofanya kazi ya kufundisha Walimu au *TRA* na kwagineko, hawa watu ndiyo wataenda kuteleze Mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wamekata tamaa, kwa sababu gharama za maisha zinazidi kuongezeka, hajjawahi kuongezwa mshahara hata shilingi 100/=, hali ni

mbaya, halafu tunataka wakatekeleze Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hili jambo Serikali lazima itafakari vizuri. Haiwezekani! Kuna muda fulani kiongozi anasema kwamba kupanga ni kuchagua, tumeamua kuanza na *SGR*, tumeamua kuanza sijui na kununua ndege na vitu vingine, sasa hivi vitu hata wewe kwenye nyumba yako, unapojenga nyumba, huwezi ukaacha kuwanunulia watoto chakula eti kwa sababu unajenga, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Umma wamekata tamaa na hawa ndio watekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Sasa hawa wameshakata tamaa, mwisho wa siku tutakachopanga hapa Bungeni hakitatekelezeka kwa sababu watu wamekata tamaa na hili jambo Serikali lazima ijitafakari vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Awamu ya Tano, ndiyo muda sasa, bado mwaka mmoja. Sasa sijui hili jambo Serikali inaonaje, lakini kwa kweli jambo hili lazima atakapokuja ku-*wind up* Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie Serikali inafikiria nini kuhusu Watumishi wa Umma ambao hawajapandishwa mishahara kwa muda mrefu na ndio watekelezaji wa Mpango? Kwa kweli wanachozungumza kitu kibaya sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu au Watumishi wengine wa Umma wana maandamano au mgomo wa chini chini. Huu mgomo hawawezi kusema hadharani. Siyo rahisi, hawawezi kusema hadharani, lakini mwisho wa siku matokeo yake tunaweza tukayaona miaka inayokuja huko baadaye ambayo siyo mazuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nimejaribu kuangalia, ni kweli kupanga ni kuchagua, siyo jambo baya. Alipokuja Mheshimiwa Rais Mkoa wa Songwe, alikuja pale kwangu Mbozi, ameenda pale Jimbo la Vwawa, ameenda Tunduma, ameenda Momba, kote alikopita kero namba moja ilikuwa ni maji; kero ilikuwa ni barabara pamoja na mambo mengine. Wananchi wale hamna hata mmoja aliyesema Mheshimiwa Rais sisi tunafurahishwa sana na

ununuzi wa ndege. Hamna aliyesema tunafurahishwa sana na ununuzi wa ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za wananchi ni maji na ndio kipaumbele namba moja ambacho ukienda huko kwa wananchi wanalia. Hata wewe mwenye ni Mbunge, ukienda kule kwako, wananchi wanalia na maji; wanauliza kuhusu Vituo vya Afya, kuhusu Zahanati, kuhusu barabara. Sasa Serikali inaweza ikawa imeamua yenyewe kufanya kitu ambacho hawajafanya tathmini vizuri kwamba je, ndio mahitaji halisi ya wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri jambo moja. Nimeona kwenye Mpango hapa, nimesoma, Serikali inasema kwamba imenunua ndege nane na ndege nyingine kabla ya mwaka kwisha...

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, hebu sikiliza taarifa. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Haonga. Ununuzi wa ndege ni moja ya mikakati ya kuweza kuongeza mapato ambayo yataenda kutekeleza miradi mbalimbali ya huduma za Jamii ikiwepo maji ambayo ameyasema. Katika Mpango huu, maji yametengewa shilingi bilioni 686 ili kuweza kutekeleza miradi mbalimbali na Halmashauri yake inapokea zaidi ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya miradi ya maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo?

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Taarifa yake naona siyo msaada kwenye ninachotaka kuzungumza. Kwa hiyo, sijaipokea kwa sababu hajui hata Halmashauri yangu napokea shilingi ngapi, anabumbabumba maneno tu. Ni vizuri akafanya utafiti kabla ya kuzungumza. Namheshimu sana, lakini ajaribu kuangalia

namna tunavyopoteza muda Watanzania. Huu muda siyo wa Haonga, ni muda wa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hapa niseme tu kwamba ni kweli Serikali imesema inataka kununua ndege 11 na imetumia zaidi ya shilingi bilioni 700 na kitu. Kwa hiyo, maana yake ndege 11 zitakapokuja, kwa taarifa ni kwamba itakuwa ni zaidi ya trillioni moja na kitu. Hizi fedha zingeweza kupelekwa kwenye miradi ya maji, kwenye miundombinu ya barabara au kwenye vitu vyote vinavyowagusa wananchi, tungakuwa mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri, kwa mfano, kwenye Jimbo langu, hata wananchi wa Mkoa wa Songwe wanafahamu, wananchi wa Rukwa wanafahamu, wananchi wa Mkoa wa Katavi wanafahamu...

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka pale Mbozi eneo linaitwa Mloo, Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe, kuna barabara kutoka pale kwenda Kamsamba inayoenda...

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** ...Rukwa hadi kwenda Kibaoni. Hii barabara Serikali iliahidi kwamba ingeweza kultengeneza kwa kiwango cha lami. Sasa daraja wanasesma imeKwisha lakini ile barabara hajatengenezwa kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, tunaamini fedha nyngi zingekuwa zinapelekwa kwenye maeneo kama haya, lile eneo ni eneo la mkakati.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Haong kwamba tunavyoongea sasa hivi tunatoka naye kwenye kikao kule Ashera, tumeitwa na Wizara ya Kilimo kusikia maoni ya wadau mbalimbali. Yeye mwenyewe kwa kinywa chake amemshauri Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Serikali inunue ndege ya mizigo (*cargo*) kwa ajili ya kusafirisha mazao ya *horticulture*. Sasa namshangaa anafika hapa tena, anageuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Haonga, si tulikuwa na wewe pale, umesahau tena!

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote duniani wanaoyumba kwanza kwa mitazamo ya vyama, wanahamahama hawawezi kuwa na akili sawasawa.

**MWENYEKITI:** Hapana.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu tumsamehe tu, tumeshamsamehe, hajui alitendalo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, nakusihi sana, tutumie lugha ya kibunge. Huyu ni Mbunge kama wewe, amechaguliwa na wananchi wa Tanzania kwa eneo lake. Wewe sema tu, unaikubali taarifa hiyo au unaikataa?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikataa taarifa yake na asiwe anahama hama vyama, maana yake Watanzania hawatamwamini tena.

**MWENYEKITI:** Haya endelea kuchangia.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Kigeugeu! (*Kicheko*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii barabara ya kutoka Mloo, Mbozi pale, Mkoa wa Songwe kwenda Kamsamba, nadhani wewe unaifahamu hii, kwenda Kamsamba, kwenda Kinyamatundu kule Rukwa kwenda Kibaoni, Katavi, hii barabara...

**MWENYEKITI:** Sawa, lakini daraja je? Sema na daraja basi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumzia barabara, kama wewe umeliona daraja, nakushukuru, mimi nazungumzia barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni muhimu sana ambapo kule wanalima ufuta, mpunga, kahawa, mahindi, maharage, alizeti na wanalima mazao mengi sana. Barabara hii ingeweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami uchumi wa Mkoa wa Songwe, Rukwa na Katavi ungeweza kupaa. Sasa leo barabara hii imeachwa, tunafanya vitu vingine ambavyo kwa kweli kwa Watanzania wala siyo kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hii barabara ni vizuri Waziri Mpango utu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Ahsante sana, lakini na daraja ni muhimu sana na ndiyo maana Serikali imeona ianze na daraja hilo na baadaye ina mpango wa lami, utafika tu.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia ambacho hakipo. Huwezi ukazungumzia kitu ambacho kipo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedasto. Hapana, Mheshimiwa Mtolea halafu Mheshimiwa Vedasto.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Mpango huu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niishauri Serikali tupange kuwawezesha wavuvi kwa kuwapa mikopo, zana za kisasa ili basi waweze kwenda kuvuna katika bahari yenye kina kirefu. Hii ni moja ya sekta ambayo imesahauika kabisa, tofauti na sekta nyine wavyuvi ni kama bado hawajapata ule upendeleo wa makusudi wa kutenda kazi zao. Tukifanya hivi tutaongeza kipato cha watu wale lakini tutainua uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tupange sasa kusitisha uhamishaji wa mifugo. Kulikuwa na maamuzi sasa ya kuhamisha mifugo kutoka maeneo ya Ihefu (Mbeya) kuipeleka Mikoa ya Kusini hasa Mkoa wa Lindi. Mifugo ile sasa imekuwa mingi sana, nafikiri tupange kusitisha zoezi hilo na sasa tujikite na kuboresha miundombinu ya mifugo iliyopo pale. Tumepeleka ile mifugo hakuna mabwawa, malambo na utaratibu wa wapi inakaa na wapi isikae sasa kumekuwa na vurugu. Mimi nafikiri kwa tija bora ya mifugo ile tupange kuboresha miundombinu ili basi ile mifugo *productive*, hilo litawasaidia sana wale wafugaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye kilimo tuongeze sasa uzalishaji wa mbegu za mafuta. Ni dhahiri shahiri kwamba ukiacha uagizaji wa petroli basi kitu kingine kinachoagizwa kwa pesa nyingi za kigeni ni mafuta ya kula. Bado tunayo fursa ya kuzalisha mbegu hizi za mafuta ili basi tuweze kupata mafuta mengi ya kula ambayo yatapunguza kutumia pesa nyingi za kigeni kuagiza mafuta hayo kutoka nje. Hilo litakuwa ni jambo jema sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tupange pia kuwa na viwanda vya mafuta. Kwa mfano, sisi kule kwetu tunazalisha ufuta mwangi lakini hatuna kiwanda cha ku-process mafuta ya ufuta, ni kama tunazalisha kwa ajili ya kusafirisha ufuta ghafi kitu ambacho kwenye uchumi nafikiri hakiko sawasawa. Tukipanga sasa mpango wa kuwa na

viwanda nya ku-*process* ufuta, vitasaidia kupata hayo mafuta, kutengeneza ajira na kuinua uchumi wa watu wale. Lindileo tumetajwa kama Mkoaa wa mwisho, tunazalisha ufuta mwiningi tukiwa na viwanda vikubwa nya ku-*process* mafuta ya ufuta tutawezesha kupandisha uchumi wa watu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nafikiri sasa tupange kuwa na mtawanyo unaofanana wa uwekezaji wa viwanda. Tunajenga viwanda ni jambo jema na tunaenda kwenye uchumi wa viwanda lakini hivyo viwanda tumeona kama vinajikita sehemu moja. Serikali iangalie uwezekano sasa wa kutawanya, tuangalie kule zinakopatikana malighafi basi na viwanda vijengwe huko. Vitasaidia kutengeneza ajira lakini vitasaidia kujenga ustawi wa miji na kupandisha uchumi wa watu katika maeneo husika. Hilo litakuwa ni jambo jema sana kwa ustawi wa uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kusema ni kuhusu suala zima la uwekezaji. Tupunguze urasimu katika uwekezaji kwani bado kuna urasimu mkubwa katika uwekezaji. Sisi pale kwetu alikuja mwekezaji kutoka Marekani akitaka kuwekeza katika Bonde la Mto Matandu kwa ajili ya kilimo cha mpunga, ni uwekezaji wa zaidi ya dola milioni 50, uwekezaji mkubwa sana. Sisi Halmashauri tukashawishi Serikali za Vijiji tukatoa ile ardhi lakini kilichotokea basi alitokea tu dalali mmoja akaanzisha longolongo mwishoni yule mwekezaji akaondoka, nafikiri aliamua kuondoka kwa sababu ya urasimu. Serikali ijaribu kufuatilia tupunguze urasimu kwani uwekezaji kama ule ungefanyika ungewasaidia sana wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule uwekezaji wa miradi mikubwa kwa mfano *LNG* lakini kiwanda cha mbolea ni jambo jema kama Serikali ingehuisha utekelezaji wake. Limekuwa likizungumzwa lakini utekelezaji wake mpaka sasa naona ni kama umekwenda kwa kusasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na uamuzi wa kupunguza kwanza ushuru wa Halmashauri katika

yale mazao yanayolimwa na wakulima katika Halmashauri kutoka asilimia 5 mpaka 3 lakini ule uamuza wa kutotoa ushuru wa korosho umezi-*paralyze* Halmashauri zetu, Halmashauri zetu hali ni mbaya sana. Hii inachangia pengine hata kufanya wananchi katika Halmashauri uchumi wao kuwa chini na kutajwa kama maskini. Lindi na Mtwara tunazalisha korosho, mwaka jana ushuru ule haukwenda kabisa. Zipo Halmashauri zaidi ya asilimia 90 ya mapato yake zinategemea ushuru wa korosho. Kwa hiyo hilo nalo Serikali iliangular vinginevyo hawa watu ukisema ni maskini tu inakuwa kama hukuwatendea haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji. Tumekuja na mawazo mazuri kabisa ya kuanzisha Mamlaka ya Maji Mijini na Vijiini, ni jambo jema lakini sasa Serikali ipange kupeleka pesa za kutosha. Katika jambo ambalo bado linaguswaguswa ni suala la maji. Tuna Wakala huyu kwa mfano *DDCA* wa kuchimba visima bado kabisa kazi hajafanyika. Tuwaongezee pesa waweze kuchimba visima vingi na kufufua ile miradi ya siku nydingi ambayo imekufa ili basi wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama na hivyo kuinua uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Suala hili la hiki kinachoendelea ni jambo geni kwenye mchakato wetu wa demokrasia na uchaguzi. Ni jambo ambalo limeleta sintofahamu, tumestushwa na tume pigwa na bumbuwazi, kwa nini hili limetokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu hili ni jambo geni na Waswahili wa Pwani wanasema: "Mgeni kumpokea pengine kujichongea". Sasa hili limekuja tulikemee siyo jambo zuri baadaye litakuja litatusumbua sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi bado wanaendelea kuhangaika kufuata zile taratibu za kupata hizo haki. Tumejiandikisha majina baadaye ukaja uchaguzi wa kuteuliwa, hatukuteuliwa, tukaweka yale mapingamizi bado hatukupata hiyo haki, sasa hivi hatua inayofuata ni

kwenda kukata rufaa na rufaa inatakiwa ukakate Makao Makuu ya Wilaya. Sasa kwa jiografia ya Majimbo yetu kutoka vijijini kwenda Wilayani ni mbali sana kiasi kwamba zile siku mbili hazitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ina nia njema ya kuona hii haki inapatikana, niishauri Serikali iongeze siku kwa ajili ya kukata rufaa. Wananchi bado wanaona kwamba wanataka kutafuta hii haki, kama ambavyo mmeongeza siku za kuijandikisha basi ongezeni siku za watu kwenda kukata rufaa ili kuona wanapata haki zao ili tuweze kwenda kwenye kuchagua viongozi ambao wananchi wanawataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na orodha yangu na sasa ni Mheshimiwa Lolesia Bukimbwa, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na niweze kuchangia Mpango wa Taifa wa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa lile agizo lake la kwamba Halmashauri ziweze kuhamia kwenye maeneo yao ya utawala. Mimi kidogo kwenye Jimbo langu tumepata changamoto, baada ya kuwa tumehamia Nzela kwa kweli jiografia imekuwa ngumu sana. Wananchi wa Busanda walikuwa wanafuata huduma kwenye ofisi za zamani yaani ni karibu kilomita 40/50 hivi lakini sasa hivi inabidi waende zaidi ya kilomita 100 kwa ajili ya kufuata huduma. Naomba Serikali pengine itupatie Halmashauri nyingine ili wananchi waweze kupata huduma vizuri na kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilipo nimekuwa nikipata simu nyingi kutoka kwa Watendaji wa Serikali, Walimu Wakuu wa Shule lakini vilevile Watendaji wa Vijiji na Kata

wanapata shida sana. Jambo ambalo siku za nyuma angetumia siku moja sasa hivi inabidi atumie siku mbili aende Nzela kwenda kusainisha cheki arudi, alale mjini ili kesho yake aweze kupata huduma, ni shida sana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie suala hili. Hata ikiwezekana kwa kuwa mwanzo ofisi zilikuwa Mji wa Geita basi turudishwe hata kama ni Mji kama hatutapatiwa Halmashauri sasa hivi ili angalau wananchi waweze kupata huduma kwa ukaribu zaidi kama ambavyo Serikali inakusudia kusogea huduma kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la wakulima wa pamba. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwamba wananchi wameuza pamba yao lakini mpaka sasa kuna baadhi ya wananchi hawajaweza kulipwa haki zao, ni kilio kikubwa sana. Kwa hiyo, pia hilo naomba Serikali iweze kulifanyia kazi wananchi waweze kulipwa fedha zao kwa sababu wameuza pamba kwa mkopo sasa umeingia msimu mpya wanatakiwa angalau wanunue tena mbegu lakini wanashindwa kwa sababu hawajaweza kupewa fedha zao kutokana na mauzo ya pamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nilikuwa naomba kwenye Mpango huu wa Serikali katika suala la kilimo hasa mazao ya biashara Serikali iangalie uwezekano wa kuwekeza zaidi fedha nyingi kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. Kwa mfano, katika zao la pamba, Serikali iweke fedha nyingi kuhakikisha kwamba viwanda vya kuchakata pamba vinakuwepo ili hatimaye masoko ya pamba yawepo kwa sababu haiwezekani wananchi wanalima pamba ya kutosha lakini masoko hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na viwanda vingi vya kuchakata mazao, nina uhakika kwamba wananchi wataweza kupata fedha zao kwa wakati na hatimaye watu wengi watahamasika zaidi kuongeza ulimaji wa pamba kwa wingi. Kwa hiyo, katika bajeti ijayo kwenye kilimo, Serikali iwekeze zaidi kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya

biashara ili hatimaye kuweza kuongeza thamani ya mazao hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kweli inafanya kazi kubwa sana kwa sababu Mpango huu wa Miaka Mitano naufuatilia mwaka hadi mwaka na kweli mipango yake na utekelezaji vinaonekana. Kwa mfano, katika sekta ya afya tumeona jinsia Serikali ambavyo imeweza kutekeleza mambo makubwa sana yanayoonekana katika taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya, Serikali imetujengea zahanati na vituo vya afya pamoja na Hospitali za Wilaya lakini vilevile tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi katika sekta hii. Nitumie nafasi hii sasa kuomba katika bajeti tuangalie umuhimu wa kuweza kuweka bajeti kubwa kwa ajili ya kuajiri watumishi katika sekta ya afya kwa sababu upo upungufu mkubwa sana pamoja na kwamba tunajenga vituo lakini kama hakuna mtaalam wa kutoa huduma bado tutakuwa hatujatenda haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la umeme wa *REA*. Naipongeza sana Serikali kuona umuhimu wa kuwa na umeme vijiji. Wananchi wanaoishi vijiji wamehamasika sana kuhusiana na suala la umeme. Niombe Serikali iendelee kuwekeza fedha nydingi hasa kwenye upande wa kupeleka umeme vijiji kwa sababu vijiji ndipo ambako wanaishi wananchi wengi, asilimia kubwa ya Watanzania wapo vijiji. Tukiwekeza kwenye suala la umeme wa *REA* vijiji kwa wingi kabisa, vijiji vikapata umeme, mimi najua kwamba tutaweza kufikia ile azma ya Serikali ya Tanzania ya viwanda lakini pia tutaweza kufikia ule uchumi wa kati mpaka mwaka 2020 - 2025. Kwa hiyo, niombe sekta ya umeme ipewe kipaumbele kikubwa zaidi ili wananchi waishio vijiji waweze kupata umeme huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kila napokwenda Jimboni wananchi wanaulizia kuhusu umeme, kila mtu anataka umeme, kila kijiji kinahitaji kupewa umeme. Sina uhakika sehemu zingine lakini ni karibu kila sehemu katika nchi ya Tanzania sisi ambao tunatoka Majimbo

ya vijijini tunahitaji umeme. Tunaomba sana wanapopanga bajeti tuhakikishe suala la umeme lipewe kipaumbele cha kutosha ili wananchi walio wengi waishio vijijini wapatiwe umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi kabisa ni suala la barabara za vijijini. Mimi nazungumzia vijijini kwa sababu Jimbo langu ni vijijini. Bajeti ya *TARURA* haitoshi, tuongeze bajeti zaidi kwenye *TARURA* kwa sababu tukiwa na barabara nzuri vijijini tutawawezesha wananchi wetu kuweza kufanya shughuli zao na kuuza mazao yao vizuri na kwa wakati. Kwa hiyo, niombe tuongeze bajeti zaidi *TARURA* ambako ni barabara za mjini na vijijini lakini zaidi kwenye vijiji ambako ndipo kuna changamoto kubwa sana ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala la UKIMWI, tunafahamu kabisa kuna takwimu zinaonesha kwamba vijana kati ya miaka 15 mpaka 24 wanapata maambukizi makubwa sana ya UKIMWI lakini zaidi ya hapo asilimia 60 ya hao vijana ni watoto wa kike, jambo hili kwa kweli ni la kusikitisha. Kwa hiyo, naomba kwenye Mpango wa Taifa na bajeti tuone umuhimu wa kuwekeza mpango zaidi kuweza kunusuru suala hili hasa kupunguza maambukizi ya UKIMWI kwa vijana wetu ambao ndiyo Taifa tunalitegemea kesho na nguvu kazi ya Taifa. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie umuhimu, ikiwezekana tuendelee kuhamasisha zaidi masuala haya ya UKIMWI ili wananchi waendelee kujiepusha na na masuala haya ya UKIMWI. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu UKIMWI huu tunapoteza Taifa hasa vijana wetu, kwa hiyo, tuwekeze bajeti zaidi kuendelea na kampeni kuhusiana na suala hili la UKIMWI. Nasema hivyo kwa sababu miaka ya nyuma mara kwa mara kulikuwa na uhamasishaji sana kuhusu kuepuka suala la UKIMWI lakini leo hii tumepunguza kidogo hiyo kasi na ndiyo maana pengine maambukizi yameanza upya, yameongezeka zaidi kwa kipindi hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naipongeza Serikali hasa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa makusanyo ya fedha hasahasa kwa kielektroniki. Naomba tuendelee kuwa na msisitizo zaidi kwamba kila mtu ukinunua kitu uchukue risiti kwa sababu kuna wafanyabiashara wengine hawatot i risiti kwa hiyari hivyo tuendelee kuweka msukumo. Sasa hivi tumepunguza kidogo msukumo lakini tuendelee kama ambavyo Rais ameendelea kusisitiza, tuendelee zaidi kuhamasisha, kusisitiza kwa sababu wananchi wakilipa na kupata risiti, mapato haya yanaenda moja kwa moja kwenye Pato la Taifa yanaingia *TRA* kwa ajili ya mapato ya Taifa letu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kupitia Wizara hii iangalie namna ya kuendelea kusisitiza suala la kudai risiti na kulitolea msukumo mkubwa ili tuendelee kupata mapato zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kuendelea kusema kwamba Serikali aingalie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kwa mchango wako mzuri.

**MHE. LOLEIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofj*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Dkt. Christopher Chiza ajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia mpango wa mwaka 2020/2021. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu wa Miaka Mitano, nianze tu kwa kupongeza katika suala zima la elimu kwa sababu tangu Rais wetu alipoingia madarakani

alifanya elimu bure na wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne mwaka huu ndio wanafunzi ambao kwa kweli katika hiyo miaka minne wamenufaika na elimu bure. Kwa hiyo, napongeza sana jitihada hizi za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ni mzuri na tunaona ndani ya miaka minne pia iliyopita utekelezaji umekuwa ni mzuri kwa sababu ipo miradi ambayo kwa kweli wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Tunapongeza kwa jitihada hizi ambazo ni Mapinduzi makubwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano iliyofanya katika kuvalatea Watanzania maendeleo. Imani yangu kubwa ni kwamba miradi hiyo itakapokamilika Tanzania tutaelekea kabisa katika ule uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kupitia viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu wa 2020/2021 ningependa nizungumzie katika suala zima la Uwekezaji, tunafahamu Uwekezaji ni jambo zuri sana na kwa kweli nipongeze Wizara husika Mheshimiwa Angella Kairuki pamoja na Ofisi ya Waziri ya Mkuu nawapongeza sana kwa sababu tunaona kwa kweli baadhi ya vikwazo ambavyo tayari kwa sasa vimeondolewa na tumerahisha huduma ambazo sasa zinapatikana katika eneo moja badala ya ule usumbufu uliokuwepo hapo awali. Tunapoelekea kwenye uchumi wa kati ni dhahiri kabisa vikwazo hivyo vingeweza kupunguza kasi ya Wawekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia wawekezaji katika upande wa Maliasili, tunawahitaji sana, lakini ningependa kuishauri Serikali kwamba katika Mpango huu na hata tunaelewa kabisa kwamba tangu tumeweka *concession fees* kwa kweli pato limeongezeka kwa kiasi kikubwa sana makusanyo yamekuwa ni makubwa, kwa mfano tu *TANAPA* kwa Hifadhi ya Serengeti kwa kipindi cha tangu Julai mosi mpaka mwezi wa 10 walikusanya zaidi ya bilioni 49 na yote hii imewezekana kutokana na *concession fees* ambayo tulipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana na niwapongeze sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi hiyo

nzuri, lakini ningependa kushauri kwamba katika uwekezaji huu sasa tuangalie ni kwa jinsi gani tunapunguza hoteli nydingi ambazo zipo ndani ya Hifadhi zetu. Kwa sababu tunaelewa kabisa utajiri huu tulionao hata wenzetu wa jirani wanatamani wangekuwa nao na tunapoweka hoteli nydingi katika maeneo hayo wanyama nao pia wanakimbia kwa sababu ya kuona mazingira ambayo ni tofauti na yale waliyoyazoea. Kwa hiyo ningeishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, tunapokwenda huko labda sasa, tuone kwamba ndiyo tunahitaji, lakini waweke mazingira mazuri kwamba kupunguza hoteli ndani ya Hifadhi angalau zikajengwa pembezoni mwa Hifadhi ili basi wanyama wale waendelee kuwepo na hatimaye waendelee kuongeza pato la Serikali kama ilivyo pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia sana Serikali hili ya Awamu ya Tano kwa sababu katika suala zima la mikopo tumeona kwamba mikopo ya elimu kwa vyuo vikuu imeongezwa na ukiniliza kipaumbele changu ni kipi hasa katika Bunge hili, basi sifichi nitasema kwamba ni watu wenye ulemavu, watu wenye ulemavu. Kwa sababu gani nasema hivyo? Watu wenye ulemavu kwa kweli katika Awamu hii ya Tano Serikali imekuwa na jicho la ziada katika kuhakikisha kwamba wanatimiziwa mahitaji yao. Pia katika suala zima la Uongozi Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kweli ni Rais wa mfano na tunapongeza sana kwa hilo na nawapongeza pia hata Mawaziri ambaao kwa kweli wamekuwa na ushirikiano mkubwa sana katika suala zima la watu wenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sasa basi tuweze kupata viongozi wengi ambaao wanatokana na kundi hili la watu wenye ulemavu, napendekeza katika Mpango huu kuona ni kwa jinsi gani kwamba tunaongeza bajeti hii ya mikopo ili wanafunzi wenye ulemavu waweze kupata ruzuku badala ya mikopo, kwa sababu Waswahili wanassema ukimwona nyani mzee, ujue amekwepa mishale mingi. Mtu mwenye ulemavu mpaka anafika Chuo Kikuu kuna changamoto nydingi sana amezipitia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu katika nchi zilizoendelea wanatoa ruzuku badala ya mikopo kwa sababu hata anapomaliza Chuo Kikuu kupata ajira inakuwa ni ngumu sana, kwa hiyo kurudisha ile mikopo bado inakuwa ni ngumu na ni mzigo mkubwa kwake.

Kwa hiyo ningeomba kwamba hawa watu wenye ulemavu tuangalie Serikali ni kwa jinsi gani tunawapa ruzuku badala ya kutoa mikopo kwa kweli ambayo hapo baadaye kwao inakuwa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiamini Serikali yangu kwa umakini ilionao na ombi langu hili basi katika Mpango huu tunapoelekea tuone kwamba bajeti hiyo inazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu na hata wale watoto ambao wamezaliwa na familia za watu wenye ulemavu kipato chao kinakuwa ni duni. Naiomba Serikali tuone kwamba ni kwa jinsi gani tunawa-accommodate hawa watu wenye ulemavu na familia zao ili basi angalau ruzuku hiyo itasaidia, lakini kuona ni kwa jinsi gani sasa tunaboresha shule, naipongeza kwa kweli Serikali kwa sababu tayari imekwishaanza na matunda tunayaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado mimi kama Mwakilishi wao ninawasilisha ombi la kuona kwamba ni kwa jinsi gani tunaboresha shule zetu ambazo zita wa-accommodate na watoto wenye ulemavu. Kwanza kwa kuangalia katika ajira ambazo tayari wamekwishaanza kufanya, lakini tuongeze pia Walimu ambao wana ujuzi na utaalam wa kufundisha watu wenye mahitaji maalum ambao ni wanafunzi wenye ulemavu. Shule nydingi za vijijini bado miundombinu yake siyo rafiki kabisa, kabisa, kwa hiyo naiomba Wizara iangalie ni kwa jinsi gani miundombinu hii inawawezesha watoto wenye ulemavu hasa vyoo, imekuwa ni shida, wakati mwingine unakwenda vijijini ukienda kwenye hiso shule kwa kweli inahitaji moyo ambao kwa kweli ni mgumu kwa sababu watoto wale wanalazimika kwenda kwenye vyoo ambavyo wanatambaa, wakati mwingine akitoka kwa kweli anatia huruma na ni rahisi sana kupata magonjwa, kwa hiyo tuone ni kwa jinsi gani tutaboresha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la ajira kwenye Ofisi ya Waziri ya Mkuu, nimeona kwa kweli jitihada kubwa na natambua na nampongeza sana Mheshimiwa Jenista yeye ni mwanamke shujaa, jasiri kwa jicho lake la ziada ambalo amekuwa karibu sana na watu wenyewe ulemavu. Sasa naomba basi katika Mpango huu tuone ni kwa jinsi gani zile Taasisi au Wizara ambazo bado hazijatimiza asilimia tatu, asilimia tatu kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu tuzingatvie.

Ningeomba hata Bunge letu pia kwa kweli limekuwa la mfano na Mheshimiwa Spika popote alipo nampongeza sana kwa kazi kubwa kwa sababu miundombinu amekuwa ni mfano na wengi waje kuiga hapa, lakini sasa naomba pia katika suala la asilimia tatu, matarajio yangu ni kuona napishana na watu wenyewe ulemavu katika Taasisi yake ambayo kwa kweli watakuwa ni mfano bora na watatoa elimu ambayo itasaidia wengine pia ambao bado kwa namna moja au nyingine wako nyuma sana katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la uwekezaji, wawekezaji wanaokuja tumeona kwamba wanaajiri watu wengi na ajira zipo nyingi, lakini na wao pia asilimia tatu nayo izingatiwe pia ili watu wenyewe ulemavu wale ambao wamepata elimu, wamesoma waweze hizo ajira na hatimaye kuweza kujikomboa wao wenyewe na kusaidia familia zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza kwa sababu mimi ni mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na nimeshuhudia mengi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, kazi wanayofanya hasa kwa kuzingatia kwamba kitalu nyumba kinawasaidia sana, vijana wengi wamewezeshwa. Nawaomba sasa katika Mpango huu tuone ni kwa jinsi gani tunafika maeneo mengi zaidi katika nchi hii ili vijana tuweze kuwawezesha katika kilimo hasa kupitilia Mfuko wa Uwezeshaji wa Vijana, vijana wengi waweze kupata mikopo ambayo itawawezesha kujiajiri badala ya kutegemea ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayaona mengi kuptitia Kamati hii, vijana ambao wamewezeshwa na sasa hivi wengine mitaji yao imefika zaidi ya bilioni. Kwa hiyo kwa kweli tukiawezesha vijana wengi na maeneo mengi tukawafikia na pia tukawatumia hata baadhi ya Wabunge huku katika Majimbo yao, naamini kabisa vijana wengi sasa hawatokuwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mollel kwa mchango wako na ushauri wako.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia Theonest, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Chiza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nianze kwa kueleza changamoto ambayo wakulima wa Mkoa wa Kagera hususan Wilaya ya Karagwe waliipata, Karagwe na Kyerwa katika zao lao la kahawa. Nataka tunavyopanga Mipango tuone ni namna gani tunaweza ku-rescue changamoto wanazopitia hawa wakulima ambao wamekuwa miaka yote kahawa ni kipato chao ni uchumi wao wa muda mrefu, kahawa kwao ndiyo dhahabu na ndiyo *diamond*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyoongea, uchumi wa Mkoa wa Kagera, uchumi wa Wilaya za Karagwe na Kyerwa umeanguka kabisa. Kipato kidogo walichokuwa wanakipata husomesha watoto, kujenga, kutunza familia zao, kujenga nyumba kiliparaganyika. Soko la kahawa lilianguka lakini kama haitoshi, Serikali ikaanza kununua Kahawa kuptitia Vyama vyta Ushirika *KDCU*, changamoto ndiyo ilikoanzia, kabla ya hapo tulikuwa na wafanyabiashara kwa maana ya Makampuni yananunua kahawa, tumeona mikoa tofauti tofauti tukiangalia korosho, Makampuni yananunua korosho,

tukiangalia pamba, Makampuni yananunua pamba, tukiangalia mazao mengine alizeti, Makampuni yananunua alizeti, lakini ikija katika Mkoa wa Kagera mnaambiwa Makampuni yasinunue na badala yake ni Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika vinatupa bei gani? Msimu uliopita kilo moja ya kahawa inanunuliwa kwa shilingi 1,100. Mkulima ambaye alitarajia kujkwamua analea Kahawa kwa miezi sita anakuja kupewa shilingi 1,100 watu wamerudi kwenye umaskini, maisha yamekuwa magumu na takwimu ziko wazi. Takwimu za Mkoa wa Kagera miaka yote inaelekea kwamba ni mkoa unaozidi kurudi nyuma, zinatajwa Wilaya kama Ngara, zinaonekana ni kati ya wilaya tano za mwisho, tatizo ni nini? Watu wanalima, ardhii ina rutuba, tuna msimu wa kutosha, lakini mazao yetu yakifikia kuuzwa, Serikali inasema msiuze kuna bei elekezi, kuna shilingi 1,100. Tatizo ni nini? Kama korosho zinaweza kuruhusiwa makampuni kununua ni kwa nini kahawa zisiruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita 2017/2018 kahawa ilienda mpaka kilo moja kwa shilingi 2,000. Tunavyoongea leo 2018/2019 kahawa ni shilingi 1,100 kama nilivyokwishesa, changamoto imekuwa nini, ni kwa nini Serikali hajjawasaidia wakulima hawa? Tulisikia tamko la Mheshimiwa Rais kuitia Vyombo vya habari kwamba kahawa isinunuliwe chini ya shilingi 1,400 lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri, hakuna mkulima aliyeweza kuuza kilo kwa shilingi 1,400, tatizo ni nini? Tunaambiwa kuna tozo, ni tozo gani sisi hatuzifahamu na kwa nini tuumizwe wakulima? Kama uchumi wetu, uti wa mgongo wa wakulima wa Mkoa wa Kagera ni kahawa, kwa nini zao hili likianguka Serikali haiwazi namna ya kuwapa ruzuku? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tangazo la Serikali nimelinukuu hapa, ambalo lilionesha kwamba wangepewa ruzuku ya Sh.100 kwa mwaka uliopita, kwa kila kilo iliyouzwa, lakini ninavyoongea hapa, hakuna hata mkulima mmoja aliyewahi kupewa ruzuku hata ya senti kwenye kahawa alizouza, ni kwa nini tunafanyiwa haya, wakulima sisi wa Mkoa wa Kagera. Ni kwa nini watu wanakatishwa tama? Ni kwa

nini mnaamua kuturudisha kwenye umaskini, wakati Mungu ametupa ardhi, Mungu ametupa rutuba, Mungu ametuwezesha, ni kwa nini? Nataka nipewe majibu ni Mpango gani uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukivuka kwetu, ukisema Mlongo ni mpakani mwa kama kilomita mbili, ukitoka upande wa Tanzania ukaingia upande wa Uganda, nimekuwa *surprised* hata ya leo, kilo ya kahawa ninavyoongea inanunuliwa kwa zaidi ya Sh.3,000, lakini upande wa Tanzania ambao ni *just* kilomita moja au mbili inanunuliwa kwa shilingi 1,100 tatizo ni nini? Sisi wakulima tunasema minada imekuwa inaendeshwa Kilimanjaro, ndiyo kuna minada ya kahawa ambayo inapelekewa kwenye Soko la Dunia, ni kwa nini hiyo minada haifanyiki kwetu ambako sisi tunazalisha sana kahawa? Ni kwa nini wakulima wa Mkoa wa Kagera wanaonekana ni kama *second class*? Ni kwa nini wakulima wa Mkoa wa Kagera hawawezi kuonyeshwa thamani ya biashara ya zao lao la kilimo ambalo wamelitegemea muda wote? Nataka Serikali iniambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nime-*google* nikaona hata *prices* za dunia, nikaona kwamba iko around, mfano kama *arabica coffee* ni dola 2.85 ambayo ni *equivalent* na shilingi 4,835, ukija *robusta* inakuja kama dola 1.75 ambayo inaweza kuja mpaka shilingi 3,000, lakini sisi kwetu, soko halipandi na hatujui hiyo *KDCU* inashindanishwa na nani? Ukitaka kuleta *monopoly* kwenye soko ujue utawaumiza wale wakulima. Unavyoamua *KDCU* ndiyo wanaamua kununua zao la kahawa, unaua kabisa soko, ye ye atakachoamua ndiyo kitakachofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha, hawa wakulima hizo fedha wanalipwa kwenye akaunti, wanalipiwa kwenye akaunti benki, wanakopesha Chama, wanasubiri wiki nzima, wao wakishakusanya fedha watumiwe kwenye meseji waende wakachukue fedha. *it is not fair* haiwezekani, sisi watu wa Mkoa wa Kagera hatutaki, hili ni zao letu, tunataka litukomboe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, nimepitia bajeti ya kilimo, katika miaka mitatu *consecutively* nikaona ambavyo kilimo kimeenda kinashuka lakini na ukiangalia mchango wa kilimo katika Pato la Taifa unaona ni mdogo sana, inaoneshwa hapa kwenye taarifa ukurasa wa tano, kwamba mwaka 2016/2017, kilimo kimekua kwa asilimia 7.6. Mwaka unaofuata imekuwa asilimia 5.6, uliofuata ni asilimia 5.3. Kama hatuwekezi fedha ya kutosha kwenye sekta inayowaajiri watu wengi maana yake *we are likely kuwa-starve*. Ni sawa, tunaweza kuona tunafanya miradi mikubwa, lakini miradi hiyo mikubwa kama haigusi watu wengi, ni kupoteza muda na wananchi wanaendelea kuwa maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia kwenye hoja yangu ya mwisho, naombeni Mipango wanayoenda kupanga iguse watu wengi na siyo watu wachache. Wapange Mipango inayotekelzeza, waache *ku-bust* bajeti wakati bajeti haitekelzeza, *roughly* kwa miaka mitatu, bajeti ukifanya *estimate* imetekelezwa kwa asilimia 36 tu, kwa miaka mitatu ya bajeti ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi kwenye mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nataka kuwaambia hivi tunachokitengeneza leo kwa kuona Vyama vya Upinzani katika nchi ni *second class citizen*, tunavyotaka kuona kwamba kuna watu ni wazalendo wakiwa kwenye Chama Tawala, basi wao ni wazalendo, lakini sisi wengine siyo wazalendo, maneno kama kuunda jukwaa la wazalendo, Walimu wazalendo, tunataka kutengeneza kinachotokea South Africa, tunataka *ku-turn this country into a zone of phobic country*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *South Africa* unaona wanauana leo walianza kidogo kidogo kwamba huyu, huyu ni Mkaburu, sawa alikuwa na rangi yake, lakini leo nawaona hao hao weusi wanaanza kuuana wao kwa wao na sisi tunakotaka kwenda mtu ukionekana unaji-associate na Vyama vya Upinzani kama ni kazi utapoteza, kama ni *promotion* utakosa, kama ni kuhamishwa utahamishwa,

tunachokitengeneza ni nini? Tunataka ku-*burn down* hii nchi kwa sababu ya madaraka na nataka kuwaambia hakuna hali ya kudumu, *there is no situation which is permanent*, unawenza ukajiona leo wewe uko viti vya juu lakini kesho tutakutana benchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano ya kudumu, tuna mifano halisia, kuna watu walikuwa Mawaziri Wakuu katika nchi hii, leo tuko nao tunalalamika, msijione leo mmekalia viti vyekundu mkadhani mtadumu kuwa hivyo, tuisiangalie maslahi ya tumbo letu katika gharama ya nchi yetu, *no please*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie ni namna gani tunaweza kuwaunganisha Watanzania, tuangalie namna gani siasa zinaweza kutusaidia kuipeleka nchi yetu mbele, tupishane kwa hoja tusipishane kwa Vyama vyetu, tupishane kwa miono, tusipishane kwa maslahi, mimi ninachokiona hapa ni maslahi nani atabaki kwenye nafasi gani, nani atabaki azidi kuwa katika nafasi fulani na aonekane zaidi. Hayo mambo hayatujengi na hayo mambo hayataisaidia nchi, *we can torn this country into pieces* kama hatutobadilika, nataka niwaambie wanasiasa wenzangu tunaweza tukaamua ni aina gani ya nchi tunataka kuijenga, alioiacha Mwalimu Nyerere ambayo tunaonana sisi wote ni ndugu, sisi wote ni marafiki au nchi mpya ambayo South Africa leo wanalia, au nchi mpya ambayo Rwanda imewa-cost.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, Mipango siyo tatizo, Mipango ni matumizi, tutakuja hapa tutaongea, tutapewa posho, tutarudi Majimboni, lakini tukirudi bajeti imetekelvezwa kwa asilimia 20, Bajeti imetekelvezwa kwa asilimia nne. Nitoe mifano tena halisi kabisa kama muda utaniruhusu, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Kilimo, katika fungu la maendeleo ilitengewa bilioni 100, ni bilioni mbili tu ziliweza kutolewa, *imagine* tumekaa Bunge zima hapa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakumbusha Kanuni ya 60(9) tusirudie rudie yale ambayo tumeyasema au yamesemwa na wenzako. Tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Eng. Chiza. Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kupata nafasi hii, leo kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ambaye anajua la mtu ambalo liko ndani ya moyo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuniletea miradi, kuhusu afya nimepata vituo vya afya vitatu, na katika jimbo langu kuna vituo vitatu na vyote vimepata fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ile barabara ya Kwa Mkocho-Kivinje, ambayo nilipiga kelele kwa muda mrefu sana tangu awamu ile ya nne, *alhambullah* barabara imeisha, tunashukuru sana. Jambo lingine ambalo nashukuru sana kuna *VETA Chuo cha Maendeleo*, kimejengwa, kinaendelea vizuri sana, tunashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna mahakama ni nzuri kwelikweli, mahakama imekwisha, *Alhamdulillah*. Kwa hiyo, kwa kweli nashukuru, mengi ambayo nimeomba na niliyasemea katika Bunge hili, yametekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na waswahili wanasesma mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Sisi ni wanasiasa, kuna wakati jambo likiwa zuri lazima tusifie, lakini kuna jambo likiwa siyo sawasawa, lazima tukosoe, na hiyo ndiyo siasa, hakuna aliyekamilika katika dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba sana, sisi tuna Bandari Kilwa Masoko pale, sijaona katika mpango wako Mheshimiwa Mpango, kama bandari ile ambayo ina kina kirefu tena cha asili, sijaona katika mpango wako kama ipo na itekelezwe. Pia kuhusu habari ya maji, kuna mradi mkubwa sana, Mheshimiwa Mpango naona siku moja

tuliyokaa, nakushukuru sana Mheshimiwa Mpango, mradi wa maji ule umeingizwa katika mpango wa Mradi wa India, katika ile miji midogo 29 na ule upo, ni mradi mkubwa sana. Naomba utekelezwe na *Inshallah* utatekelezwa kwa sababu nimeona katika mpango wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja hayo, yote tunayopanga haya, kama hakuna utawala bora, kama hakuna utawala bora, sawasawa na kutwanga maji katika kinu. Tunakusifieni sana, kwa huduma za jamii mmejitahidi, lakini utawala bora, tatizo na ninamuomba Mheshimiwa Magufuli, aangalie katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imefika katika hali mbaya, mlanza kwa kutisha, nchi ikawa kuna utekaji mwingu, kuna mauaji mengi, mkazuia mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, hakika Watanzania tumetishika! Hapo mmefaulu sana katika utawala bora! Tumetishika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo, katika Wilaya yangu ya Kilwa, Jimbo la Kilwa Kusini, tumesimamisha wagombea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika vijiji 15 tuliviyosimamisha hata kijiji kimoja hakuna aliye...

**MBUNGE FULANI:** Kwa chama gani?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** *CUF* wewe huju?  
(*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameondolewa katika uchaguzi, kuna mtu mmoja kaondolewa, kuna Kijiji kimoja cha Nanjilinji wameondolewa, walisema wao hawajui kuandika kingereza na hawajui kusoma kiingereza! Sasa katika fomu pale unaulizwa, chama chako gani? *The Civic United Front*, Chama cha Wananchi, ndiyo ameambwa mmesema uongo! Ninyi mlisema kwamba hamjui kuandika kiingereza mbona mmeandika *civic*, wameondolewa sababu hiyo hiyo tu! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme, wametolewa wajumbe wangu 25 wa Kijiji cha Nanjilinji A kwa kuandika *The Civic United Front*, ninyi mnasema uwongo! Aa, jamani, sisi tumenkuu tu kadi yetu imeandikwa, sisi tukaangalia tukafuatoshua tu, aaa! Mmesema uongo! Wangeliandika *CUF*, wangelitolewa, kwa sababu hakuna chama kinaitwa *CUF*, wakiandika *The Civic United Front*, wanakwambia wewe ulikuwa hujui kuandika kingereza, hujui kuandika kingereza, inakuwaje kuwaje? Imefikia hivyo Tanzania kweli! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwingine ametolewa katika kinyang'anyiro, kwa kuandika Waziri, binti jina lake Fatuma Waziri Juma, basi katolewa kaambiya hatujui jina linaloitwa waziri, jina... *walah wabilah* nayo! Hakuna jina linaloitwa Waziri, waziri ni cheo! Katolewa, *walah wabilah watalah*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda wapi? Tunaweka pingamizi, tunaambiwa, pingamizi lako umeandika mwenyekiti, badala ya kuandika uenyekiti, huna sifa! Huna sifa, unaomba nafasi ya uenyekiti! Wengi, hata CCM inawajua, wameandika hivyo hivyo, wengine wameandika uenyekiti, wengine mwenyekiti, basi unaondolewa, kugombea kwa sababu umeandika mwenyekiti, aaa! Lengo si lilelile unayegombea cheo cha uenyekiti, sasa mtu unasemaje! Tuseme nchi hii imefikia hatua hii, kweli jamani! Kukosea neno moja, ndiyo unaondolewa katika uchaguzi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, cha ajabu sasa, twende leo wewe nani huyu, Mhagama wewe, twende mimi na wewe katika Kituo cha Msaidizi, tukachukue fomu za CCM, *walah wabilah*, wameandika vibaya kushinda sisi, lakini ninachojua, kanuni inasema, mteuzi atakuwa msaidi, na msimamizi masaidizi, alilitwa lkulu! Sasa mtu kaitwa lkulu, huyu anataka kusimama, hebu simama wewe. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge na hasa kwa kusilia kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwenye jimbo lake, na vilevile vazi lake zuri sana na linaakisi Shirika letu la Ndege Tanzania, kwa hiyo, anapongeza pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, hayo yote anayoyasema, Serikali imeshatoa taarifa, hao wote waliokuwa wanaitwa akina Waziri, wametoka Najilinji, walioandika kina Fatuma, walliondika uenyekiti, mwenyekiti, kama wanaona wameonewa, wakate tu hizo rufaa zitasikilizwa na mwisho wa kuzisikiliza ni kesho!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, ninaomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge, awe tu na subira, kesho, itampa matokeo yoyote yale ambayo yanaweza kuashiria hicho ambacho kimeonekana na ninamshukuru tu anakili kwamba kwamba, mtu amekosea kosa moja, kujaza fomu ya uchaguzi ni kama mtihani, ukikosea umekosea! Kwa hiyo, asubiri tu matokeo ya rufaa yatampa ukweli na uhakika wa kila kitu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara unasemaje kuhusu taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo taarifa, ye ye kaniweka sawa tu. Nimekuelewa, nimekuelewa sana, lakini na hili la kusema, *The Civic United Front*, maana yake hilo la kukosea ndiyo umekosea, ndiyo umeandika sawasawa, lakini kosa lako unaambiwa wewe hujui kingereza, kwa kuwa umeandika kingereza toka, wewe unasemaje hilo, wewe unasemaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu ni mpango maalum, ni mpango maalum! Naomba sana, naomba sana, sisi watu wazima! Mnakoipeleka nchi siyo sawasawa, mnatutisha, mtu pengine kafumaniwa tu, kaenda kukata shamba la mahindi, kafyeka fyeka siyo sababu ya uchaguzi mnasema, kakata sababu ya uchaguzi, pengine alimfumania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara ahsante sana, muda ndiyo huo, ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa Katani hayupo, Mheshimiwa Eng. Edwin Ngonyani.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunipa afya leo naongea mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi kubwa aliyoifanya na ninajua kazi hiyo inaakisi kazi kubwa inayofanywa na Serikali nzima ya Awamu ya Tano, ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, katika vipaumbele ambavyo umetuletea, kama rasimu, nimevisoma sana, umesheheni vyote, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niombe mambo machache, mengi yamesemwa na wenzangu, lakini ninayo machache, kama utapata nafasi uyaongeze katika vipaumbele vya rasimu hii ambayo umetuletea. Nianze na eneo la sekta ya kilimo, wengi wameongeaa, kwamba kilimo ndiyo kinachoibua na kuimarisha sekta ya viwanda. Nikuombe, sekta ya kilimo ikiunganisha maeneo yote matatu, kilimo cha mazao, ufugaji mifugo na uvuvi, vipewe kipaumbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ilivyowekwa kwenye mpango, nina wasiwaso haijaka vizuri. Katika eneo hili la kilimo cha mazao, ningeomba sana uliangalie sana eneo la pembejeo, hususani mbolea, lakini vilevile mbegu na viuatilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mbolea, ni kweli, tumeondo ruzuku, nikuombe hilo uliangalie upya. Kilimo, ndiyo kinachukua watu wengi zaidi na wengi wanaojihuisha na kilimo hawana uwezo wa kumudu bei ya mbolea ambayo sasa tunayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ya Awamu ya Tano, kama ambavyo imeweka kipaumbele kikubwa katika miundombinu, niombe muweke kipaumbele katika mbolea, mbegu, viuatilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tu, kwamba katika mbolea, tuna uwezo kabisa wa kuweka ruzuku kwa asilimia 100, kwa maana ya kwamba, wakulima wapate bure. Kama hilo haliwezekani, walau ukaweka bei kama shilingi elfu 10, kama ambavyo mkulima wangu, Kuhoa amependekeza katika meseji aliyoniletea leo, kwamba walau ukiweka hata shilingi elfu 10 kwa mfuko katika kilimo, utakuwa umewasaidia sana wakulima wengi sana ambao kwa kweli hawana uwezo wa kununua mbolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mbegu, hata Wizara ya Kilimo inafahamu, kwamba matumizi ya mbegu bora, ni kwa kiwango kidogo sana kwa sababu bei yake ni kubwa. Bei iliyopo katika mbegu wakulima hawaiwezi. Tunaishia kutumia mbegu zetu za asili ambazo hazina ufanisi katika uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ama tuimarishe taasisi zetu zinazozalisha mbegu nchini, tuingize fedha nydingi upande huo, badala ya kutegemea mbegu zinazotoka nje ama zinazozalishwa ndani, lakini zinazofadhiliwa na makampuni ya nje, bei muda wote itakuwa kubwa. Hebu tuliangalie lile eneo, kama tunaweza tukaingiza ruzuku ya kutosha, nina

uhakika mazao yatakayozalishwa katika kilimo, tukiondoa ruzuku, yatarudisha hasara ambayo unadhania utaipata ukiweka ruzuku katika eneo hilo, nikuombe uliangalie hilo kwa makini sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni maji, kipaumbele katika ulivyoviyorodhesha, hata katika eneo hili la maji nalo halijakaa vizuri sana. Nikuombe, jaribu kuliangalia kwa macho manne, matano, sita, hapo peke yenu mlipokaa una macho manne hapo, ya Waziri pamoja na Naibu, hebu ongezeni macho mengine katika eneo hili la maji. Najua mna sababu za msingi kukataa kuongeza shilingi elfu 50 kwenye mafuta, kwa ajili ya kuuongeza ule mfuko wa maji, ili utoke kutoka shilingi 50 uende shilingi 100, najua mna sababu za msingi, lakini hebu liangalieni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumelipigania sana hilo la kuongeza shilingi elfu 50 zaidi, siyo kwa sababu tunataka kuongeza bei ya mafuta, lakini tunataka maji. Kwa hiyo, kama kuna namna ya kutuwezesha kupata maji, angalia katika vipaumbele vyako na eneo hilo nalo liguswe kwa namna ambayo kwa kweli watanzania watafurahia maisha, hasa watanzania wa kijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la miundombinu, umeelezea kwa kirefu sana maeneo ya reli yanayoshughulikiwa, lakini hii reli ya kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay* kuititia Namtumbo, umeiweka chini sana ni kama umeificha hivi na kwa kweli ukiangalia kazi inayotakiwa kufanywa katika reli hii, inaonekana kabisa umeiweka pembeni. Yaani pamoja na kwamba umeandika sehemu ya kipaumbele, lakini *in reality*, nadhani bado haijaingia kwenye *matrix* yako kichwani mwako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe, tumeamua reli hii ijengwe kwa *PPP*, wenzangu waliotangulia wameeleza, kwamba fursa za wawekezaji binafsi wanaotaka kushughulika na hiyo reli wako wengi, lakini tatizo lipo katika masharti, liko katika masharti yanatakiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mliangalie hili kwa makini. Kwanza linapunguza matumizi ya fedha za Serikali. Tunatumia fedha kutoka sekta binafsi, hebu tujaribu kuangalia kama tunaweza tukapunguza masharti ili reli hii iweze kujengwa. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mpango, reli hii ukiikamilisha ukaipitisha pale Namtumbo ikafika mpaka Mbamba Bay na hatimaye ikafika Liganga na Mchuchuma, itajiedesha yenyewe na gharama zake zitarudi haraka zaidi. Kwa sababu mzigo ulioko katika hiyo *corridor* mwingi sana; ukiacha ile chuma ya Liganga na Makaa ya mawe ya Mchuchuma kuna madini mengine mengi sana ikiwa ni pamoa na Uranium ya Namtumbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi madini ya *Uranium* yanashindikana kuchimba kwa sababu bei ya Uranium iko chini sana. Kwa sababu ya gharama zilizopo za usafirishaji, tukipunguza gharama za...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer Ngonyani*.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na uchangiaji wetu kwa leo, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ndio wa mwisho kwa leo. Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwa mchangiaji wa mwisho katika hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango. Napenda

kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli naipongeza sana Awamu ya Tano kwa maana ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mipango pamoja na Mawaziri wenzake kwa kazi nzuri ambayo wanaitendea haki Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tulipoenda kwenye uchaguzi mwaka 2015 tulikuwa tunawaahidi wananchi maendeleo. Kusema kweli, mimi binafsi Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, nikizungumzia katika Jimbo langu la Musoma, ingekuwa leo ndiyo tunaenda kwenye uchaguzi hasa tukiwa tunazingatia yale tuliyoyaahidi, basi naweza nikasema utekelezaji umefanyika kwa zaidi ya asilimia 95. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni ukweli usiopingika, hata unaposafiri barabarani utakutana na magari mengi ya nguzo kwa maana ya nguzo ya umeme, mabomba ya maji, lakini hayo yote ni mambo ambayo yanafanyika katika lengo zima la kuhudumia wananchi. Ndiyo maana hata ndugu yetu Mheshimiwa Bwege pale, ye ye mwenyewe ameshukuru na ameweza kusema wazi kwamba mambo ambayo yamefanyika katika awamu hii ni mambo ambayo ni ya wazi wazi kwa maana ya mambo ya kimaendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwasi wangu ni mmoja tu ambapo katika Mpango huu wa leo sijaona kama tumezungumza sana. Pamoja na juhudhi hizi kubwa za maendeleo tunazofanya, lakini bado mahitaji hata tungepeleka maji, hata tungetengeneza barabara pamoja na elimu, lakini mahitaji mwaka baada ya mwaka yapo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mifano michache. Pale kwenye Jimbo langu la Musoma, ile mwaka 2005

tulijitahidi sana kujenga sekondari karibu kila Kata, lakini ndani ya muda mfupi tu, leo kuna Kata ambazo zina sekondari zaidi ya tatu. Hapo ni kwamba mahitaji ya sekondari bado yako pale pale. Ukienda kwenye Shule za Msingi, leo unakuta kwa sababu ya ufinyu wa maeneo ya kujenga, pale pale tumezibananisha, ilikuwa ni shule moja, sasa ziko shule mpaka nne. Kwa hiyo mahitaji haya, mashaka yangu ni kwamba inaonekana hayatacaa yapungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajuliza, sijui labda hili watu wengi tunaogopa kulisema, maana nimejaribu kuangalia hata katika nchi za wenzetu zinazoendelea, suala la uzazi wa mpango; ni kwamba kwa namna ambavyo Watanzania tunaongezeka siku kwa siku, katika mtazamo wangu ni kwamba pamoja na juhudzi zote ambazo tutazifanya, lakini bado mahitaji yataendelea kubaki pale pale. Kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba, hata kama tunadhani kama hatulioni; nitoe mfano kwetu sisi watu wa Mara ambao tunaruhusiwa kuoa wanawake mpaka watano, maana yake ni kwamba familia zetu zinaendelea kupanuka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ninyi Wasukuma, upanuzi wa familia unaendelea siku hadi siku. Sasa hayo yote ukiyaangalia, kama hatuwezi ku- *address* suala la uzazi wa mpango ni tatizo ambalo ninaamini kwamba pamoja na juhudzi za awamu hii, lakini mahitaji bado yataendelea kubaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia wale wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba, maana kwa namna ninavyoliona ni tatizo la ajira. Wanafunzi wanamaliza Darasa la Saba, zaidi ya asilimia 50 wanaingia mtaani. Wanafunzi wanamaliza Kidato cha Nne, zaidi ya asilimia 70 wanaingia mtaani; wanafunzi wanamaliza mpaka Vyuo Vikuu, zaidi ya asilimia 80 hakuna kazi. Hii yote, katika mtazamo wangu ni kwamba wanafunzi wote hawa wanakosa ajira kwa sababu hawana *skills*. Yaani asilimia kubwa ya wanafunzi hawana mafunzo yoyote yanayoweza kuwawezesha hata kujajiri. Hali hii ni hali ambayo inaendelea. Sasa nini kifanyike katika huu Mpango wa muda mfupi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali awamu hii, ilianzisha mpango wa kuchukua wanafunzi wengi au vijana wengi kwenda JKT. Kusema kweli wale vijana wamekaa kule miaka mitatu na wamejifunza mafunzo mbalimbali; mafunzo ya ukakamavu na badhi ya mafunzo mengine labda ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika mtazamo wangu, Serikali inapaswa iongeze nguvu zaidi. Nini kifanyike? Moja, wale vijana wanaoenda JKT, kwanza waendelee kuchukuliwa wengi zaidi, nami nakubali kwamba wakae miaka mitatu. Pia katika kipindi cha miaka mitatu hiyo wajifunze mafunzo mbalimbali; ujasiriamali, mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kila mwezi tuwe na utaratibu kama tunawalipa mshahara, lakini fedha hizo tunaziweka kule. Hata kama tungekuwa tunawawekea shilingi 200,000/=, baada ya miaka mitatu, yule kijana atakuwa na pesa zisizopungua shilingi milioni saba. Sasa ile siku tunapomwambia sasa kijana umemaliza miaka mitatu JKT, hebu nenda kaendeleee na maisha, tafsiri yake ni kwamba akiondoka pale na shilingi milioni saba na huku ameshajifunza mafunzo mbalimbali, lazima atapata mahali pa kuanzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, baada ya miaka mitatu tunawaambia, tunawachukua wachache Jeshini, wachache Polisi, halafu wengine tunawaambia wakaanze maisha. Kwa kweli tunawapa ugumu wa maisha. Hii sioni kama inawasaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akaliangalia na hilo aliweke katika Mpango tuone namna ya kuchukua vijana wengi zaidi kwenda JKT wakajifunze, lakini mwisho wa siku waondoke na chochote, waondoke na ujuzi ili wakaanze maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naona na lenyewe tunahitaji kuliweka katika Mpango, tunajitahidi sana kuwasomesha vijana mpaka kwenye elimu ya juu.

Tunapowapeleka mpaka kwenye elimu ya juu, kuna baadhi ya *degree* ambazo vijana wakitoka nazo kule ukimleta kwenye maisha ya kawaida anazidiwa na kijana ambaye ametoza *VETA* au mwenye *Diploma* ya Mifugo. Hii yote ni kwa sababu kuna baadhi ya *degree* ambazo kama hakupata ajira ya Serikali, hawezি kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kama ambavyo tumejitätahidi sana kujenga shule za sekondari, kama ambavyo tumejitätahidi sana kujenga Vyuo Vikuu, hebu tuwe na mikakati mahsusiy ya kujenga hivi vyuo katika maeneo yetu. Mfano Vyuo vya Mifugo, Vyuo vya Kilimo, Vyuo vya *VETA* na Vyuo vya Ufundji Uchundo. Tunadhani kwamba hawa vijana wanaomaliza Darasa la Saba, wanaomaliza Kidato cha Nne, wakiondoka na huo ujuzi, basi unaweza ukawasaida zaidi kwenda kuanzisha maisha kuliko katika hali ya sasa ambayo wanaendelea nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ndiyo maana vijana wetu wengi leo wakishamaliza hizi elimu mbalimbali, unawakuta tu wako Mitaani wala hawajui wafanye nini. Ndiyo maana sasa kila ukiwaliza kila kijana anazungumza hali ya maisha ni ngumu kwa sababu anashindwa namna gani anavyoweza kuendesha maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu mwingine ambao Mheshimiwa Dkt. Mipango aendeleee kuuweka katika mipango ni huu utaratibu wa uendelezaji wa bandari. Bahati nzuri tumeendeleza Bandari kama ya Dar es Salaam, ya Mtwara na Tanga. Ziko bandari ambazo leo zimesinzia. Ukienda kama kule Kanda ya Ziwa, pale Musoma bandari imelala; ukienda Mwanza bandari zimelala na ukienda Bukoba bandari zimelala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa najaribu kuangalia Serikali ilipoanzisha utaratibu wa *bulk procurement*, huu wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja. Katika utaratibu wake wa kudhibiti nadhani kama magendo na vitu kama hivyo na kuwa na mafuta bora; ilichokifanya, ilianzisha kwenye eneo moja tu la Dar es Salaam. Ikafika mahali

ikafanya vizuri, Serikali eneo la Tanga ikafika mahali wakafanya vizuri na Serikali imepeleka Mtwara, imefika mahali wamefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia kule Kanda ya Ziwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ulikuwa na hoja nzuri sana, muda ndio huo.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Kuna matangazo. Utawala wanaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge waliojiorodhesha kwa ajili ya zoezi la kulenga shabaha kuwa usafiri wa kwenda JKT Makutupora utakuwepo katika viwanja vya Bunge saa 1:00 asubuhi, kesho siku ya Jumamosi tarehe 9 Novemba, 2019.

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu kushiriki kesho kwenye zoezi hilo kwa sababu wenzetu wa JKT wamefanya maandalizi makubwa kwa ajili yetu. Pia tutashiriki katika uzinduzi wa Bendi ya Jeshi letu la Kujenga Taifa. Kwa hiyo, tutaondoka hapa saa 2:00 asubuhi, tujitahidi kuwa kwenye maeneo ya viwanja vyetu hapa.

Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya tangu asubuhi kipindi cha maswali na baadaye kwenye kutoa ushauri wa Mapendekezo ya Mpango.

Sina la ziada, bali kuahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 11 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.15 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 11 Novemba, Saa Tatu Asubuhi)*